# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO


## IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA

## IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA

### IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED

### IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU


### UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo.

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea. Hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka kwa lugha ya kiswahili hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasayansi kama kina Enstein, wasanii kama Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiuza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

Mwisho: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

## MAKOSA YA CHAPA

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa, Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswutu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146), Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa Fawqahum ila yawmil qiyama badala ya Fawqahum yawamal qiyama. Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu Jabal amil 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana.

Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa.” Kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin (a.s): **"Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu."** Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubalia yale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

1

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

Sura Ya Kumi Na Saba: Al –Israi.

Ina Aya 111, Imeshuka Makka, Isipokuwa Aya tano, na imesemekana ni nane.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu.

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَ وْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١﴾

1. Ametakasika aliyempeleka usiku mja wake kutoka Msikiti Mtakatifu mpaka msikiti wa mbali ambao tumevibariki vilivyo kandoni mwake, ili tumuonyeshe baadhi ya ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

## ISRAI

**Aya 1**

### MAANA

Ametakasika aliyempeleka usiku mja wake kutoka Msikiti Mtakatifu mpaka msikiti wa mbali ambao tumevibariki vilivyo kandoni mwake, ili tumuonyeshe baadhi ya ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

### MAANA YA NEON ISRAI

Maana ya neno Israi katika lugha ya kiarabu ni kutembea usiku. Makusudio ya neno ‘mja wake’ hapa ni Muhammad **(s.a.w.w)**. Msikiti mtakatifu ni ule ulioko Makka kwenye Al-ka’ba.

Anasema mwenye Rawhul-lbayan na wengineo: “Riwaya iliyo sahihi zaidi ni kuwa safari ya Israi ilianzia kwenye nyumba ya Ummu Hani, dada yake Ali bin Abu Twalib.”

Msikiti wa mbali (Masjidul-Aqswa) ni hekalu la Nabii Suleiman. Umeitwa msikiti kwa sababu ni mahali pa kusujudu, kutokana na neno la Kiarabu masjid (msikiti) lenye maana ya mahali pa kusujudu. Na umeitwa Masjidul Aqswa (msikiti wa mbali), kwa sababu ya kuwa mbali na Makka. Msikiti huo umebarikiwa kandoni mwake kwa baraka za kidini, kwa vile ni nchi ya mitume na kwa baraka za kidunia kwa mito na miti.

Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

Inawezekana ‘Yeye’ kuwa ni Mwenyezi Mungu kwa maana ya kuwa anamjua Mwenye kuamini na mwenye kukanusha tukio la Israi. Pia inawezekana kuwa ‘yeye’ hapa ni Muhammad **(s.a.w.w)** kwa maana ya kuwa anajua ukuu na utukufu wa Mwenyezi Mungu.

Imesemekana kuwa Israi ilikuwa usiku wa kuamkia tarehe 27 Rajab (mfunguo kumi), Na pia imesemekana ilikuwa 17 Rabiul-awwal (mfunguo sita).

## ISRAI KWA ROHO NA MWILI

Ulama wengi wanalitumia neno israi kwa safari ya Mtume **(s.a.w.w)** kutoka Masjidul-haram (Msikiti Mtukufu) ulioko Makka, hadi Masjidul-aqswa (Msikiti wa mbali) ulioko Baytul- muqaddas (Nyumba yenye kutakaswa).

Na wanalitumia neno Mi'raj (miraji) kwa safari ya kutoka Baytul-muqad- das hadi juu mbinguni. Wengine hawatofautishi baina ya maneno hayo mawili; wanatumia Miraji kwa kupanda mbinguni na Israi kwa kutoka Makka hadi Baytul-Muqaddas[1].

Wote wameafikiana kutokea tukio hili kutokana na nukuu za Qur'an na Hadith za Mtume. Lakini wametofautiana kuwa je, lilikuwa kwa roho tu bila ya mwili au kwa mwili na roho? Sisi tuko pamoja na wale wasemao lilikuwa kwa mwili na roho. Hapa tutazungumzia Israi – safari ya kutoka Msikiti Mtakatifu hadi Msikiti wa mbali, Ama miraji - kupanda juu mbinguni, mazungumzo yake yatakuja katika Juz; 27 Sura 53.

Wale wanaosema kuwa ilikuwa ni kwa mwili na roho wametoa dalili zifuatazo:

1. Israi ni jambo linaloingia akilini na dhahiri ya wahyi umelitolea dalili; pale aliposema Mwenyezi Mungu: "Aliempeleka usiku mja wake" na hakusema roho ya mja wake. Neno mja linatumika kwa roho na mwili; kama alivyosema Mwenye Mungu:

Je, unamuona yule ambaye anamkataza mja anaposwali? (92: 10). Misingi (usul) ya Uislamu iliyothibitishwa ni kuwa kila lililoelezwa na dhahiri ya wahyi na lisipingane na akili, basi ni lazima kuliamini.

Kama Israi ingelikuwa ni kwa roho tu, kusingelikuwa na mshangao wowote, wala washirikina wasingeliharakisha kumfanya mwongo Muhammad. Kuna Hadith isemayo kuwa Ummu Hani alimwambia Mtume mtukufu **(s.a.w.w)**: "Usiwaambie watu wako hilo, nahofia watakufanya muongo," lakini hakutilia maanani hofu ya Ummu Hani kwa kuona kuwa maadamu ni haki basi haina neno. Kwa hiyo akawatangazia watu wake aliyoyaona. Wakashangaa na wakampinga. Kama ingelikuwa ni kwa usingizi wasingelikuwa na mshangao huu.

2. Kwenda Israi kimwili na kiroho ni nembo ya kuwa kila mtu ni lazima ayafanyie kazi maisha yake ya kimwili na kiroho, sio upande mmoja tu.

3. Ni mashuhuri kuwa Mtume amesema: **"Nilipelekwa usiku kwenye mnyama anayeitwa Buraq."** Ni wazi kwamba Israi ya kiroho peke yake haihitajii kupanda mnyama wala chombo chochote.

Kwa mnasaba wa Buraq tutaashiria makala iliyo kwenye gazeti la Al-Jumhuriya la Misr, iliyoandikwa na Muhammad Fathi Ahmad, yenye kichwa cha maneno 'Madhumuni ya kisayansi ya Israi na Miraji,' Ninamnukuu:

Alipanda Mtume mtukufu mnyama anayeitwa Buraq. Kulingana na Hadith ni mnyama anayemzidi punda kwa kimo na yuko chini kidogo ya baghala. Hapo kuna somo kutoka kwa Mwenyezi Mungu tunapaswa tulitafutie maelezo Mwenyezi Mungu hashindwi kumchukua Mtume wake

---

1. Waswahili wamezoweya kutumia neno Miraji kwa safari yote ya kutoka Makka hadi mbinguni kupitia Baytul - Muqaddas - Mtarjumu.

kutoka Makka hadi Baytul-Muqaddas bila ya nyenzo yoyote ambapo Mtume angeweza kujikuta tu yuko kwenye mlango wa Masjidul-aqswa. Lakini Mwenyezi ambaye imetukuka hekima yake alipitisha kuwa kila kitu kiende kwa kanuni yake, bila ya mabadiliko wala mageuko.

Safari hii iliyokata masafa marefu katika kasi ya kushangaza, inahimiza akili ianzishe nyenzo mpya ya kwenda masafa marefu katika muda mdogo. Kisha tujiulize, ni kitu gani katika ulimwengu kinakwenda kasi zaidi kulingana na utafiti wa elimu? Bila shaka jibu litakuja bila ya kusita kuwa ni mwangaza ambao unakwenda kwa kasi ya 300,000 km. kwa sekunde moja.

Buraq aliyemtumia Mtume alitembea kwa kasi ya mwanga kwa sababu neno Buraq ni mnyambuliko wa neno Barq lenye maana ya mwako kama wa umeme (flush).

Kupitia majaribio ya kiakili katika uchunguzi wa anga za juu, binadamu ameweza kugundua siri nyingi na ameweza kwa nguvu ya elimu kupenya kutoka ardhini hadi kwenye ufalme wa mbingu. Lakini elimu ya maada pekee inamsahaulisha binadamu na muumba wake.

Tukio la Israi na Miraji linatupa somo kwamba maada na roho ziko sambamba. Kwa hiyo kwenda kwake kwenye utukufu wa juu kulikuwa ni kwa umbile la kibinadamu kutokana na maada na kuendeshwa kulikotokana na roho ya Muumba Mtukufu, Jibril akawa anachukua nafasi ya muelekezaji njia. Nasi hatuna kizuizi cha kumfanya ni nembo, kwa madaraka ya elimu, ambayo itatuongoza kwenye safari yetu katika maisha haya kuelekea kwa muumba wa ulimwengu".

Ya kushangaza niliyoyasoma kuhusu maudhui haya ni kauli ya anayesema kuwa Israi ya Mtume **(s.a.w.w)** ilikuwa kwa roho sio kwa mwili wake mtukufu kwa kutoa dalili ya hadith iliyopokewa kutoka kwa Aisha, kwamba mwili wa Mtume haukumwacha usiku ule. Na inajulikana kuwa wakati wa Israi, Aisha alikuwa mdogo, wala hakuwa ameolewa na Mtume **(s.a.w.w)**; Kwa hiyo Hadithi hiyo inajipinga yenyewe.

## MASJIDUL-HARAM NA MASJIDUL-AQSWA

Masjidul-Aqswa unafanana na Masjidul-Haram katika mambo haya yafutayo:-

1. Yote iko upande wa mashariki.

2. Historia ya yote ni ya zamani; isipokuwa Masjidul-haram ni wa zamani zaidi na pia ni mtukufu zaidi. Kwa sababu ndiyo nyumba ya kwanza kujengwa kwa ajili ya ibada duniani: "Hakika nyumba ya kwanza waliyowekewa watu ni ile iliyoko Makka yenye kubarikiwa na mwongozo kwa viumbe. Mna humo ishara zilizo wazi: Mahali aliposimama Ibrahim. Na mwenye kuingia humo huwa katika amani; na ni haki ya Mwenyezi Mungu juu ya watu kuhiji nyumba hiyo kwa mwenye kuweza njia ya kuiendea. Juz; 4 (3:96–97).

3. Miji yote miwili, Makka ulio na Masjidul-haram na mji wa Quds ulio na Msjidul–Aqswa ilianzishwa na Waarabu au walishiriki kuianzisha. Makka ilijengwa na Ibrahim na mwanawe Ismail waliojenga Al-ka'aba: "Na tuliagana na Ibrahim na Ismail kuwa: Itakaseni nyumba yangu kwa ajili ya wale wenye kutufu na wenye kujitenga huko kwa ibada na wanaorukuu na kusujudu… Na Ibrahim alipoinua misingi ya ile Nyumba (Al-Kaaba) na

Ismail (wakaomba): Ewe mola wetu! Tutakabalie; hakika wewe ndiye Msikizi, Mjuzi, Juz; 1(2:125,127).

Inajulikana kuwa Ismail ndiye Mtume wa kwanza kuzungumza lugha ya Kiarabu ambayo haikuwa lugha ya baba yake. Maquraysh na waarabu wengineo wanatokana naye. Qur'an ilishuka kwa lugha yake.

Quds nayo waliishi hapo wayabusi, kabila la waarabu wa Kanani. Walifika kwenye mlima maarufu unaojulikana kwa jina la Zayuni, mnamo mwaka wa 2500 (B.C.) kabla ya kuzaliwa Nabii Isa wakiongozwa na mzee wao aliyeitwa Salim Al-yabusi. Watu wa kabila hili ndio wa kwanza kuweka jiwe la kwanza la kujenga mji wa Quds ambao baadae ulikuwa ndio Qibla cha ulimwengu.[1]

Baada ya Waislamu kuuteka mji wa Quds walijenga msikiti ulioitwa Masjid Umar, uliasisiwa na Umar bin A-khattwab na Masjid Qubbatusswakhra (msikiti wa kuba la mwamba) ulioasisiwa na Abdulmalik bin Marwana, Yote hiyo ilikuwa ndani ya haramu ya Quds, Waislamu walikuwa hawaruhusu asiyekuwa Mwislamu kukanyaga hapo.

4. Waislamu wanaitukuza misikiti yote miwili, ambapo mwanzo walikuwa wakiswali kwa kuelekea Masjiul-Aqswa kwa muda wa miaka 13 wakiwa Makka na miezi kadhaa Madina. Kuongezea safari ya Israi, inakuwa si jambo la ajabu kwa Waislamu kupafanya mahali hapo ni pa takatifu na ni pa pili baada ya Makka na Madina kwa utukufu, heshima na ulinzi.

Mpokezi mengi yanaeleza kuwa Mtume alimfunga Buraq hapo Baytul-Muqaddas, Mpaka sasa ukuta wa magharibi ya haram, mahali alipomfunga, unaitwa ukuta wa Buraq, pia mapokezi yanaeleza kuwa Mtume aliswali kwenye sehemu ya mwinuko katika hekalu la Nabii Suleiman, pamoja na Nabii Ibrahim, Musa na Isa akiwa yeye ndiye Imam. Na kwamba yeye alitumia mwamba wa Ya'qub kuwa ndio kituo chake cha kupanda mbinguni.

Ndio maana uharibifu wa Quds mnamo mwaka 1967 uliyotekelezwa na wazayuni na wakoloni wa kimarekani na waingereza, ni maafa ya waislamu na wakiristo.

Mkono mchafu ulichafua na kudharau sehemu takatifu za dini ya kiislamu na ya kikiristo. Usiku huo wa damu walikesha na ufuska; wakafanya sherehe za dansi na ulevi.

Ajabu ya maajabu ni kwa Marekani na Uingereza kudai kuwa wao ni wahami wa dini na ni maadui wa ulahidi, wakati huo huo wakiwasaidia wazayuni amabo hawaamini misimamo yoyote, hawaheshimu maadili, hawaheshimu dini za wengine wala hawatambui haki yoyote katika haki za binadamu.

Amerika na Uingerza zimeisaidia Israili, zikaipa mali na silaha na zikaiunga mkono kweneye Baraza la usalama na Umoja wa mataifa. Zikaipongeza kwa kuingila sehemu takatifu za waislamu na wakiristo. Wameendelea na misimamo hii ulimwenguni pote.

---

1. Maelezo hayo yanatokana na uchambuzi wa mtaalam Michel Khalil, uliotolewa na jarida la Al-yawm no. 25/5/1968.

Sisi hatuna shaka kwamba iko siku itawafikia wakoloni na marafiki zao wazayuni kupitia mikononi mwa wanamapinduzi wapigania uhuru; kama ilivyowafikia hivi sasa wamarekani kutoka kwa wavietnam na kabla yake iliwafikia wazayuni kutoka kwa Nebuchadnezzar, Waroma, Mtume **(s.a.w.w)** na Khalifa wa pili Umar bin Al-khattwab.

Hivi sasa kila siku vyombo vya habari haviachi kutangaza habari za upinzani wa Palestina na kujitoa mhanga ambako kumeifanya Israil yote iishi kwenye jinamizi la hofu na woga[1].

## SOMO KATIKA ISRAI

Qur'an hii ambayo tunaisoma ni masomo aliyompatia Muumbaji Mtume wake ili ayafikishe kwa watu wote, Masomo haya yako aina nyingi. Miongoni mwayo ni hukumu ya maarifa ya halali na haramu, jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, ikhlasi na subira kwa ajili ya haki.

Lililo muhimu zaidi katika yote ni kumwamini Mwenyezi Mungu na utukufu wake kwa imani sahihi inayobainishwa na maarifa ya kujua; sio kwa kuigiza, kasema fulani au kwa kuwazia tu.

Mwenyezi Mungu ameongoza njia za elimu na yakini ambazo ni kufikiri katika maumbile ya ulimwengu pamoja na ardhi na mbingu yake. Pia mipangilio, hekima na mfumo sahihi katika vyote vilivyo baina ya mbingu na ardhi, vikiwa mbalimbali na pamoja:

أَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِم مَّا خَلَقَ اللَّـهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى ﴿٨﴾

Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi ila kwa haki na kwa muda maalum. (30:8).

Baada ya Mwenyezi Mungu kumpa wahyi mja wake kwa somo la ukuu wa ulimwengu na kuumba mbingu na ardhi, alimuhusisha yeye tu kwa safari ya ardhini, kutoka Masjidul-haram hadi Masjidul-aqswa na safari ya mbinguni, kutoka Masjidul-aqswa hadi kwenye wingu wa juu.

Lengo la safari hizi mbili ni kuwa Mtume apate somo la kimatendo baada ya kupata la kinadharia kuhusu ulimwengu, aone mwenyewe, kwa macho yake, maajabu ambayo akili haiwezi kuyawazia. Njia hii, siku hizi, watu wanaifuata, ambapo waalimu wanawaandalia wanafunzi wao safari za kimasomo ili wakajionee wenyewe yale waliyojifunza.

Kwa hiyo basi somo kubwa katika safari mbili za Mtume ni kuhimiza akili kuangalia vizuri katika uumbaji wa mbingu na ardhi:

أَوَلَمْ يَنظُرُوا فِي مَلَكُوتِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا خَلَقَ اللَّـهُ مِن شَيْءٍ ﴿١٨٥﴾

Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na alivyoviumba Mwenyezi Mungu, Juz. 9 (7:185).

Imam Ali [(a.s)] anasema: **"Nashangaa na anyemtilia shaka Mungu na anaona alivyoviumba Mungu!"**

وَآتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ أَلَّا تَتَّخِذُوا مِن دُونِي وَكِيلًا ﴿٢﴾

2. Na tukampa Musa Kitabu na tukakifanya ni uongofu kwa Wana wa Israil, kwamba msi- fanye mtegemewa asiyekuwa Mimi.

1. Kumbuka mazungumzo haya ni ya miaka ya sitini.

ذُرِّيَّةَ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ ۚ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿٣﴾

3. Enyi kizazi tulichokichukua pamoja na Nuh! Hakika yeye alikuwa ni mja mwenye shukrani.

## NA TUKAMPA MUSA KITABU

**Aya 2-3**

## MAANA

Na tukampa Musa Kitabu na tukakifanya ni uongofu kwa Wana wa Israil, kwamba msimfanye mtegemewa asiyekuwa Mimi.

Makusudio ya kitabu hapa ni Tawrat na Israil ni Ya'qub bin Is-haq bin Ibrahim (a.s). Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu ameitermsha Tawrat kwa Musa ili Wana wa Israil waongoke nayo kwenye njia ya haki na ukweli na wamtegemee Mungu peke yake wala wasimfanye mwengine kuwa ni msimamizi au msaidizi wao.

Lakini wao waliyapotosha maneno ya Mwenyezi Mungu, wakaabudu ndama, wakaua mitume, na wakaijaza dunia shari na ufisadi kwa kila nyenzo waliyo nayo.

Enyi kizazi tulichokichukua pamoja na Nuh!

Nuh alichukuwa watoto wake watatu pamoja na wake zao katika Safina. Wao walikuwa ni Ham, Sam, na Yafith. (Hamu Shemu na Yafeti). Kutokana na wao kizazi kiliendelea baada ya tufani; miongoni mwa hicho kizazi ni Wana wa Israil waliokuwa katika zama za Nabii Musa. Hapa ni kuwakumbusha Wana wa Israil neema za Mwenyezi Mungu ambazo wao wanazikufuru na kuzikana.

Hakika yeye alikuwa ni mja mwenye shukrani.

Yeye ni Nuh (a.s); yaani enyi mayahudi! Kuweni na shukrani na kukumbuka neema za Mwenyezi Mungu; kama alivyokuwa Nuh, lakini hashukuru neema ila mkweli aliye mwaminifu. Na haikujulikana kwa waisraili, tangu walipopatikana, isipokuwa uongo udanganyifu na hiyana.

Imepokewa Hadith kutoka kwa Imam Ja'far Asswadiq (a.s) kwamba: Nuh (a.s) anapopambaukiwa alikuwa akisema hivi: **"Ewe mola wangu! Hakika ninashuhudia kwamba neema ya dini au dunia iliyonipambaukia inatokana na wewe; huna mshirika; wakusifiwa na kushukuriwa kwa neema hizo kwangu ni wewe mpaka uridhie."**

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَقَضَيْنَا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ فِي الْكِتَابِ لَتُفْسِدُنَّ فِي الْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾

4. Na tukawaambiwa wana wa Israili katika kitabu, hakika mtafanya ufisadi katika ardhi mara mbili, Na hakika mtajitia uluwa, uluwa mkubwa.

فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ أُولَاهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَا أُولِي بَأْسٍ شَدِيدٍ فَجَاسُوا خِلَالَ الدِّيَارِ وَكَانَ وَعْدًا مَّفْعُولًا ﴿٥﴾

5. Basi itakapofika ahadi ya kwanza yake, tutawapelekea waja wetu wenye nguvu wakali na wakawasaka majumbani. Na ilikuwa ni ahadi iliyotimizwa.

ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ الْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنَاكُم بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَجَعَلْنَاكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٦﴾

6. Kisha tukawarudishia nguvu dhidi yao na tukawasaidia kwa mali na watoto na tukawajaalia mkawa watu wengi zaidi.

إِنْ أَحْسَنتُمْ أَحْسَنتُمْ لِأَنفُسِكُمْ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ لِيَسُوءُوا وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا مَا عَلَوْا تَتْبِيرًا ﴿٧﴾

7. Mkifanya uzuri mnajifanyia wenyewe na mkifanya ubaya mnajifanyia wenyewe. Na ikifika ahadi ya mwisho, ili waziharibu nyuso zenu. Na waingie msikiti kama walivyoingia mara ya kwanza na waharibu kila walichokiteka kwa uharibifu mkubwa.

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يَرْحَمَكُمْ وَإِنْ عُدتُّمْ عُدْنَا وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ حَصِيرًا ﴿٨﴾

8. Huenda Mola wenu akawarehemu, Na mkirudia, na sisi tutarudia. Na tukaifanya jahannam ni gereza kwa ajili ya makafiri.

## WAISRAILI NA UFISADI MARA MBILI

**Aya 4 – 8**

### LUGHA

Neno Qadha lina maana nyingi; miongoni mwazo ni kuhukumu. Maana nyingine ni kuumba; kama alivyolitumia Mwenyezi Mungu aliposema: "Na akaziumba mbingu saba kwa siku mbili" (41:12). Maana nyingine ni kupitisha jambo; kama alivyolitumia Mwenyezi Mungu katika Sura hii tuliyo nayo Aya 23, aliposema: "Na Mola wako amepitisha kuwa msimwabudu yoyote ila Yeye tu na kuwatendea wema wazazi wawili." Pia lina maana ya kutoa habari kama lilivyotumika katika Aya hii tuliyo nayo.

### MAANA

Maana ya kijumla ya Aya hizi ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwapa habari wana wa Israil kwamba wao watafanya ufisadi katika ardhi kisha Mungu atawaletea watakaowadhalilisha kwa kuuliwa kutekwa na kuporwa. Baadae Mungu atawarudishia nguvu zao, lakini watarudia ufisadi mara ya pili na Mungu atawaletea tena watakaowapa pigo mara ya pili.

Ufafanuzi wa hayo ni kama ifuatavyo:

1. Na tukawaambiwa wana wa Israili katika kitabu.

Makusudio ya neno Qadhayna hapa ni kutoa habari na kuweka wazi, sio kupitisha, kwa sababu Mwenyezi Mungu hapitishi ufisadi: “Hakika Mwenyezi Mungu haamrishi machafu.” Juz,8 (7:28).

Makusudio ya Kitabu hapa ni Tawrat iliyoteremshwa kwa Nabii Musa (a.s) kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu katika Aya iliyopita: “Na tukampa Musa Kitabu.” Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwapa habari Waisraili kuwa watakaowafuatia watafanya ufisadi katika nchi mara mbili.

2. Hakika mtafanya ufisadi katika ardhi mara mbili.

Makusudio ya ufisadi hapa sio ufisadi kwa maana yake ya kiujumla ambayo yanachanganya ukafiri, uongo, kula riba, kupanga njama n.k; kwani hayo yote ndio dini yao na mazowea yao wakati wowote na katika kila kizazi chao, ambapo Mwenyezi Mungu alikwisha wasimulia pale aliposema: “Walisema Mayahudi: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba.

Mikono yao ndiyo iliyofumba, na wamelaaniwa kwa waliyoyasema… Kila mara wanapowasha moto wa vita Mwenyezi Mungu huuzima, Na wanajitahidi kuleta ufisadi katika ardhi, Na Mwenyezi Mungu hawapendi wafisadi, Juz; 6 (5: 64).

Makusudio hasa ya ufisadi hapa ni kwa maana maalum ambayo ni kutawala na kwamba utawala wao wenyewe utakuwa ni ufisadi, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwaambia Wana wa Israil:

3. Na hakika mtajitia uluwa, uluwa mkubwa.

Qur’an inalitumia neno uluwa kwa maana ya kupetuka mipaka na ufisadi. Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ ﴿٤﴾

“Hakika Fira’un alijitia uluwa katika ardhi,” (28:4).

Amesema tena:

تِلْكَ الدَّارُ الْآخِرَةُ نَجْعَلُهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ عُلُوًّا فِي الْأَرْضِ وَلَا فَسَادًا وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٨٣﴾

“Hiyo nyumba ya Akhera tumewafanyia wale wasiotaka kujitia uluwa katika ardhi wala ufisadi na mwisho ni wa wenye takua.” (28:83).

Maana ni kuwa nyinyi Wana wa Israil, mtatawala mara mbili na utawala wenu mtaufanya ni nyenzo ya ufisadi mkubwa na wa hatari ambao hauna mfano wake; mtachafua sehemu takatifu, mtavunja miko ya Mwenyezi Mungu na mtadharau misimamo mizuri, maadili na kila haki ya Mungu na ya watu.

Qur’an haikueleza mahali wala wakati wa ufisadi wao huo mara mbili, lakini wanahistoria na jamaa katika wafasiri wamesema kuwa Wana wa Israil waliivamia Palestina baada ya kuhangaika, kwa uongozi wa Yusha bi Nun, (Yoshua) khalifa wa Musa bin Imran, wakaikalia kwa mabavu na wakapora mali yote baada ya kuwafyeka wenyeji wa hapo wengi ambao walikuwa ni Wakan’ani (wakanani) na waliobakia wakawafanya watumwa. Sera yao kwa Yusha ilikuwa kama ilivyokuwa kwa Musa – uasi na inadi. Hiyo ndiyo iliyokuwa mara yao ya kwanza, kama wanavyosema wafasiri na wanahistoria.

Ama mara ya pili, kuna wanaosema kuwa bado haijatokea na kwamba itatokea baadae kwa Waarabu na Waislamu katika Palestina. Wengine wanasema kuwa imekwishatokea na kuisha, Kauli hii ndiyo yenye nguvu. Kwa hali yoyote ni kwamba Qur'an inaeleza waziwazi kuwa Wana wa Israil wakitawala hufanya ufisadi katika ardhi na kupanda kiburi kikubwa.

Kwa hiyo si uzushi kwa dola ya kizayuni kupasua matumbo ya wanawake wa kipalestina wenye mimba, kuwazika wazima vijana, kuwamiminia risasi wafungwa, kuwapiga mabomu ya sumu walio majumbani, kuvunja majumba ya wenyeji na kuwaziba midomo kwa mali na kwa vikwazo. Kisha inajitia kulia kuwa eti inachokozwa na kudhulumiwa.

Tunasema hivi tukijua kuwa Qur'an haikukiashiria kikundi hiki ambacho kimejiuza kwa kila mwenye kuongoza shari, lakini imekuja ishara yake kwa sababu kina jina la Israil na kunasibika kwenye kizazi kilichogeuzwa manyani na nguruwe.

Basi itakapofika ahadi ya kwanza yake.

Yaani ya kwanza katika hizo mara mbili za kufanya ufisadi, Ahadi hapa ni kwa maana ya wakati walioahidiwa Wana wa Israil kufanya ufisadi.

Tutawapelekea waja wetu wenye nguvu wakali.

Wanaambiwa Wana wa Israil. Waja sio lazima wawe wema, kama wanavyodai wengine, wanaweza pia kuwa waovu; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

يَا حَسْرَةً عَلَى الْعِبَادِ مَا يَأْتِيهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٣٠﴾

Ni sikitiko kwa waja, hakuwafikia Mtume yeyote ila walikuwa wakimfanyia stihzai, (36:30).

Wenye nguvu na wakali, ni ukali wa vita. Hao walikuwa ni wababilon wakiongozwa na Nebuchadnezzar au baba yake Nabopolassar ambao waliwaua mayahudi, wakachoma Tawrat na wakawachukua mateka watu wengi, wake kwa waume na watoto, Hayo yalikuwa mnamo mwaka 586 kabla ya kuzaliwa Nabii Isa (586 B.C.). Imesemekana kuwa ni mwaka 596.

Na wakawasaka majumbani.

Neno kuwasaka hapa tumelifasiri kutoka neno la Kiarabu Jasu ambalo maana yake hasa ni kutafuta sana na kurudiarudia. Qur'an haikulitumia neno hili isipokuwa hapa tu.

Maana ni kuwa hao jamaa walikuwa waki- watafuta Mayahudi majumbani mwao na wakirudi tena kuwatafuta ili wawaue.

Na ilikuwa ni ahadi iliyotimizwa bila ya kuhalifu au kuachwa Muhtasari wa Aya hizi ni kuwa Wana wa Israil walipofanya ufisadi mara ya kwanza Mwenyezi Mungu aliwapelekea watu wenye nguvu waliowaua, wakuwafurusha wanaume na kuchukua wanawake, wakapora mali zao na kuharibu majumba yao. Ufisadi huo wa kwanza na pigo lake ulikuwa kabla ya Uislamu.

Kisha tukawarudishia nguvu dhidi yao na tukawasaidia kwa mali na watoto na tukawajaalia mkawa watu wengi zaidi.

Waliorudishiwa nguvu ni Wana wa Israil dhidi ya Wababiloni; yaani Wana wa Israil walijikomboa kwa Wababilon. Inajulikana kuwa Wana wa Israil hawakupigana na Wababiloni katika miji yao wala hawakuwahi kuwashinda.

Lakini mnamo mwaka 538 Bc, mfalme wa Fursi (Iran ya sasa) aliishinda miji ya Wababiloni na akawakomboa mateka wa Kiisrail waliokuwa humo. Kwa hiyo nguvu za Wana wa Israil dhidi ya Wababiloni ni kupitia mfalme wa Fursi.

Abu Hayan Al-andalusi anasema katika Tafsir yake Albahrul-Muhit: "Mfalme alipigana vita na Wababilon. Nebuchadnezzar alikuwa ameua wana wa Israil elfu arubaini, waliobaki wakawa ndani ya Babilon wakidhalilishwa. Basi mfalme alipopigana nao na akawashinda alioa mwanamke wa Kiisrail. Huyo mke akamtaka mumewe awarudishe watu wake Baytul–Muqaddas, naye akafanya hivyo."[1]

Waliporejea wana wa Israil Palestina, Mwenyezi Mungu aliwasaidia kwa mali na watoto na akaifanya idadi yao zaidi ya ilivyokuwa mwanzo. Lakini mara tu iliporudi nguvu yao, walirudia uovu na kupotoka na dini kuliko mwanzo. Wakamuua Zakariya na wakaazimia kumuua Bwana Masih (a.s).

Mkifanya uzuri mnajifanyia wenyewe, na mkifanya ubaya mnajifanyia wenyewe.

Katika maana haya ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ ﴿٢٨٦﴾

"Faida ya yale iliyoyachuma ni yake na hasara iliyochuma ni yake." Juz, 3 (2:286)

مَّنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا ﴿٤٦﴾

"Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe na mwenye kutenda uovu basi ni juu yake" (41:46).

Na ikifika ahadi ya mwisho.

Baada ya kupita ufisadi wa kwanza wa wana wa Israil na ikapita misukuosuko yake, ulikuja ufisadi wa pili na misuko suko ya pili nayo ikachukua nafasi yake, basi Mwenyezi Mungu aliwapelekea watu ili waziharibu nyuso zenu.

Hapo wanaambiwa wana wa Israil. Kuharibika nyuso ni fumbo la misukosuko na kudhalilika kwao. Kwa sababu uso unadhihirisha furaha au huzuni iliyo moyoni. Ni mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu:

سِيئَتْ وُجُوهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ﴿٢٧﴾

"Nyuso za waliokufuru zitaharibika" (67:27).

Na waingie msikiti kama walivyoingia mara ya kwanza na waharibu kila walichokiteka kwa uharibifu mkubwa.

Makusudio ya msikiti hapa ni mji wa Quds, kwa sababu ndani yake mna hekalu la Nabii Suleiman. Limeitwa msikiti (masjid) kwa vile ni mahali pa kusujudu.

Maana ni kuwa wana wa Israil walipofanya ufisadi mara ya pili, Mwenyezi Mungu aliwapelekea watu waliowapa adhabu mbaya na hali yao ikawa kama ya kwanza – kuuliwa, kufukuzwa na kuharibiwa majumba.

Mara zote mbili za ufisadi na kuadhibiwa zilikwishapita kabla ya Uislamu.

1. Ndoa hii inaonyesha wazi jinsi Mayaudi, tangu zamani, walivyokuwa wakiitu- mia ngozi nyeupe kufikia malengo yao.

Katika Majmau-bayan imeelezwa kuwa aliyewashambulia wana wa Israil mara ya kwanza ni Nebuchadnezzar na aliyewashambulia mara ya pil ni mfalme wa Roma, akaharibu Baytul-Muqaddas na akawateka wenyeji wake.

Haya yanaafikiana na aliyoyanukuu Al-Maraghi kutoka Tawarikhl-Yahud, akasema kuwa muda baina ya mashambulizi mawili ulikuwa miaka mia tano.

Huenda Mola wenu akawarehemu.

Kwa sharti la kutubia na kuwa na huruma. Kwa sababu asiyekuwa na huruma hahurumiwi; kama ilivyoelezwa katika Hadith tukufu.

Na mkirudia ufisadi kujitia uluwa na kiburi, na sisi tutarudia kuwaadhibu na kuwadhalilisha.

Walirudia na wakafanya ufisadi; wakataka kumuua Masih (a.s) na wakamkadhibisha Muhammad **(s.a.w.w)**. Mwenyezi Mungu akawapelekea Waislamu, wakawaua Bani Quraydha, wakawatawala Bani Nadhir, wakaichukua Khaybar na wakafukuzwa Mayahudi Bara Arabu.

Na tukaifanya Jahannam ni gereza kwa ajili ya makafiri.

Wengine wamefasiri neno hasir kwa maana ya busati. Yaani tumeifanya Jahannam ni busati.

Vyovyote iwavyo, makusudio yake hapa ni kuwa Jahannam itawazunguka wala hakuna matarajio ya kuepukana nayo; sawa na kauli yake Mwenyezi Mungu:

أُولَـٰئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَلَا يَجِدُونَ عَنْهَا مَحِيصًا ﴿١٢١﴾

"Hao makazi yao ni moto wa Jahannam wala hawatapata pa kuukimbia" Juz. 5 (4:121).

## KUELEZEA MWENYEZI MUNGU NA DOLA YA ISRAIL

Mnamo mwezi Januari mwaka hu 1969, kulitokea mjadala motomoto kwenye magazeti ya Misr kuhusu Aya inayoeleza ufisadi wa wana wa Israil. Walishiriki kwenye mjadala huu wataalamu wengi wenye ghera ya haki, Uliendelea mjadala na malumbano kwa muda kiasi, Gazeti liliuchapisha kwenye matoleo mane ya kila Ijumaa ya mwezi huo tulioutaja.

Washiriki waligawanyika makundi mawili:

Kundi la kwanza linasema kuwa pigo la kwanza la wana wa Israil lilitokea kutoka kwa Umar bin Al-khttab alipoishinda Quds. Yeye na waislamu wakasaka nyumba za wapalestina. Na ufisadi wa pili wakasema kuwa ni Walivyofanya wazayuni mnamo mwaka 1967 na wanavyoendelea kufanya leo.

Kundi hili limefasiri kuwa pigo la pili la Mayahudi litatoka kwa warabu ambao watashinda hivi karibuni na warudishe ardhi zao zilizoporwa na na wakoloni hao.

Na wakasema kuwa hiyo ndio maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na waingie msikiti kama walivyoingia mara ya kwan- za." Yaani waarabu wataukomboa Msikiti wa Aqswa kutoka kwa Waisrail kama walivyoukomboa kwanza.

Hakuna rejea ya tafsir hii isipokuwa matamanio na utabiri ambao ni wajibu kuuepusha na Qur'an. Kwa sababu hiyo ni Kitabu na nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu inayofichua kawaida na desturi ya maumbile ambayo hayageuki wala kubadilika na inaangalia kila kilichomo

ulimwenguni, kuanzia chembechembe hadi vitu vikubwa; wakati huo Qur'an inambebesha kila mtu majukumu ya kufanya mambo kwa juhudi na kuchukuliwa hisabu yake mbele ya Mwenyezi Mungu, ya dhamira na ya watu wote. Kundi la pili linasema mara zote mbili za ufisadi pamoja na mapigo yake yamekwisha pita kabla ya Uislamu.

• Pigo la kwanza lilitangulia Uislamu kwa kiasi cha miaka elfu moja na lilitekelezwa na Nebuchadnezzer au baba yake, ambaye aliiharibu Quds, kuchoma Hekalu, kuua wayahudi wengi na waliobaki wakawateka nyara hadi Babiloni.

• Pigo la pili, linasema kundi hili, kuwa lilitokea mnamo mwaka wa 70.

Baada ya kuzaliwa Nabii Isa (70A.D.) lilitekelezwa na Titus (Tito) wa Roma ambaye aliuzingira mji wao na akauponda ukuta wake, akaingilia kuharibu majumba kubomoa hekalu na kuua kiasi cha watu milioni moja mbali na waliochukuliwa watumwa na kuuzwa sokoni; kama anavyosema Flavius ambaye aliishuhudia tukio lenyewe, Waliobaki wakasambaa ulimwenguni[1].

Vilevile, kundi hili la pili, limesema kuwa Qur'an haishirii kwa mbali wala karibu kuhusu kikundi kilichoko katika ardhi ya Palestina kinachojiita Israil. Kwani hicho si kikundi cha kidini wala chama cha kisiasa au serikali ya kiuhakika; isipokuwa ni adui mpya wa waarabu na Waislam, nacho ni ukoloni wa kizayuni au uzayuni wa kikoloni ambacho kimevaa nguo ya Daud kikiwa kimechukua ramani ya ulafi iliyosajiliwa kwenye Tawrat ya kupangwa iliyopotolewa 'kuanzia Nail hadi Furat' na kunyakua mali ya taifa chini ya nembo ya uyahudi. Lengo la kwanza na lamwisho ni kuleta ukoloni mamboleo kwa waarabu na waislamu kikiongozwa na Marekani.

Kwa ufupi ni kuwa Qur'an haikuashiria kabisa Israil ya sasa na kwamba Aya zinazozungumzia Wana wa Israil zimewakusudia koo kumi na mbili katika kizazi cha Ya'qub bin Is-haq bin Ibrahim ambao walikuwa katika zama za Nabii Musa na Harun. Na hawa ambao wamenyakua ardhi yetu kwa silaha za ukoloni na mali ya kizayuni si katika kizazi cha Israil bin Is-haq wala hawako kwenye dini yake wala dini ya Musa; isipokuwa wao ni viumbe wapya wa kushangaza wasiokuwa na mfano.

Kwa sababu wamepatikana kutokana na vizazi mbali visivyokuwa na mfungamano baina yao wala kujumuika kwa mkusanyiko wa kiinchi au lugha wala hawana msingi wowote isipokuwa msingi wa kibaraka wa nguvu ya shari.

Zaidi ya hayo ni kwamba tukitafsiri kuwa Mwenyezi Mungu amekwishaeleza kuwa tutauingia msikiti, tutabweteteka tu na kuzitupilia mbali sababu za ushindi za kawaida alizozibainisha Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake na kupitia kwa Mtume wake.

Ambapo mara anatuhimiza jihadi na mara nyingine anatuhiza kusaidiana, huku tukiwaandaa wengine, kutokata tamaa kuwa na subira na mara ningine kung'ang'ania jambo, kujitolea mali na kulifanya rahisi kila lililo ghali kwa ajili ya dini na uzal- endo; sawa na alivyofanya Muhammad, swahaba wa

1. Ni katika maneno ya Al-bahi Al-khawliy kwenye gazeti la Al-akhbar la Misr 31-1-1969

Muhammad **(s.a.w.w)** na waliowafuatilia wao kwa wema na kama vile wanavyofanya wanaoji- tolea mhanga hivi sasa.

Baada ya yote hayo ni kuwa Mwenyezi Mungu hapigani wala hatapigana na Israil na ukoloni wa kizayuni kwa niaba yetu; hata kama tukiswali na kumtarajia Yeye tu. Kwa sababu ibada bora zadi kwake ni kujitolea mhanga kwa nyenzo na nguvu zote dhidi ya dhulma, ukandamizaji, ufisadi na uchokozi.

Nasi tunamiliki uwezo wa kutosha wa kumtoa adui kwenye ardhi yetu. Tunamiliki uwezo huo kwa idadi yetu, dini yetu, turathi zetu na mali zetu. Lililobaki ni kuzitumia tu na hapana budi, lazima tuzitumie. Kwa sababu kupenda kubakia kunalazimisha hilo. Ukoloni na uzayuni umetuweka kwenye mambo mawili hakuna la tatu: Ama kufa au kuishi, Hakuna anayependa kufa kuliko kuishi au kuwa mtumwa kuliko kuwa huru au udhalili kuliko heshima.

3

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

إِنَّ هَـٰذَا الْقُرْآنَ يَهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا
كَبِيرًا ﴿٩﴾

9. Hakika hii Qur'an inaongoza kwenye yaliyonyooka kabisa na inawabashiria waumini ambao wanatenda mema kwamba watapata malipo makubwa.

وَأَنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٠﴾

10. Na kwamba wale wasioamini Akhera tumewaandalia adhabu chungu.

وَيَدْعُ الْإِنسَانُ بِالشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ وَكَانَ الْإِنسَانُ عَجُولًا ﴿١١﴾

11. Na mtu huomba shari kama vile aombavyo kheri. Na mtu amekuwa ni mwenye pupa.

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَتَيْنِ فَمَحَوْنَا آيَةَ اللَّيْلِ وَجَعَلْنَا آيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً لِّتَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن
رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ وَكُلَّ شَيْءٍ فَصَّلْنَاهُ تَفْصِيلًا ﴿١٢﴾

12. Na tumeufanya usiku na mchana kuwa ni ishara mbili, Tena tukaifuta ishara ya usiku. Na tukaifanya ishara ya mchana ni ya kuangazia ili mtafute fadhila itokayo kwa Mola wenu na mpate kujua idadi ya miaka na hisabu, Na kila kitu tumekifafanua wazi wazi.

## QUR'ANI INAONGOZA KWENYE YALIYONYOOKA

**Aya 9 -12**

### MAANA

Hakik hii Qur'an inaongoza kwenye yaliyonyooka kabisa na inawabashiria waumini ambao wanatenda mema kwamba watapata malipo makubwa.

Yaliyonyooka kabisa ni mila au njia ambayo imenyooka. Neno hili lina maana ya kuenea masilahi zaidi kwenye kila kitu, wakati wowote, mahali popote na kwa mtu yeyote.

Aya hii ni madai yaliowazi yaliyosajiliwa na Qur'an anayoyaamini kila Mwislamu - kwamba Uislamu ndio dini bora zaidi ya dini zote. Dalili ya usahihi wa madai haya na ukweli wake ni Qur'an kutokana na itikadi yake, sharia yake na mafunzo yake mengine kuongezea sera ya mwenye ujumbe huo, Muhammad Bin Abdillah **(s.a.w.w)** ambaye ameijaza ardhi elimu, imani, wema na uadilifu baada ya kuwa na ujahili, kufuru na ufisadi.

Maulama wamethibitisha hakika hii na wakatunga mamia ya vitabu katika kufasiri maneno ya Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu na sera yake, itikadi sharia na maadili ya kiislamu ambayo yamethibitika katika nyanja mbalimbali, Tumetaja baadhi katika juzuu zilizotangulia za tafsiri hii. Tutaonyesha baadhi ya mifano ya misingi hiyo kama ifuatavyo:

### 1. Uislamu Ni Dini Ya Maumbile

Kila msingi katika misingi ya Uislamu, kila tawi katika sharia yake na kila hukumu katika hukumu zake, imejikita kwenye umbile safi: “Ndilo umbile alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu, Hiyo ndiyo dini iliyonyooka, lakini watu wengi hawajui.”

Aya inaonyesha wazi kwamba Uislamu unaitikia matakwa ya maumbile ya binadamu na kunyoosha mikono yake kwa kila jipya lenye faida; ni sawa liwe limekuja kutoka mashariki au magharibi. Amesema Imam Ali (a.s): “Hekima ni adimu kwa Mumin. Chukua hekima hata kama ni kutoka kwa wanafiki.” Akasema tena: “Angalia kauli usiangalie aliyesema” Kuna hadith nyingi zenye maana haya.

### 2. Imani Ya Uislamu Kwenye Elimu

Uislamu unaamini elimu na kusimamia kwake maisha katika pande zote. Mwenyezi Mungu anasema katika sura hii tuliyo nayo Aya 36: “Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo.” Amesema tena:

﴿قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١١١﴾

Sema: Leteni dalili zenu kama nyinyi ni wasema kweli.” Juz.1 (2:111)

﴿فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾

“Basi waulizeni wenye ukumbusho ikiwa nyinyi hamjui” Juz,14(16:43).

Mtume **(s.a.w.w)** amesema: “Wino wa mulama utapimwa na damu ya mashahidi siku ya kiyama.” Imam Ali naye amesema: “Elimu ni dini, inafuatwa dini kwayo.”

Maana ya kuamini elimu ni kuamini maendeleo na kufanya mambo kwa ajili ya maisha yaliyo bora na ya ukamilifu.

### 3. Kuiachia Huru Akili

Uislamu unatoa mwito wa kufikiri, kutaamali na kuchunguza maumbile haya kwa kutafiti kuweza kujua siri zake, faida zake na manufaa yake. Vilevile kujua mafungamano ya mtu na muumba wake. Pia Uislamu unatoa mwito kwa dini, elimu na falsafa, kutilia umuhimu mambo yanayoonekana na maarifa ya hisia; jambo ambalo wamekuwa nalo waislamu tangu mwanzo, kisha likaenda kwa wazungu. Ikawa msingi wa elimu ya majaribio uko kwao:

﴿أَوَلَمْ يَنظُرُوا فِي مَلَكُوتِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا خَلَقَ اللَّـهُ مِن شَيْءٍ ﴿١٨٥﴾

Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na alivyoviumba Mwenyezi Mungu. Juz. (7:185).

### 4. Uhuru Wa Kufikiri

Uislamu unatoa uhuru wa kusema na kufikiri, kiasi ambacho Mwenyezi Mungu aliwaruhusu watumishi wake, Malaika, wamuhoji huku wakisema:

﴿قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ ﴿٣٠﴾

Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu? Juz; 1 (2:30).

Pia aliruhusu Ibrahim (a.s) amjadili kuhusu watu wa Lut:

﴿فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ إِبْرَاهِيمَ الرَّوْعُ وَجَاءَتْهُ الْبُشْرَىٰ يُجَادِلُنَا فِي قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٤﴾

“Basi hofu ilipomwondokea Ibrahim na ikawa ile bishara imemfikia, alianza kujadiliana nasi juu ya watu wa Lut.” Juz; 12 (11:74).

Bali alimruhusu hata Iblis kutoa hoja mbele yake:

قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِّنْهُ خَلَقْتَنِي مِن نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِن طِينٍ ﴿١٢﴾

“Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kwa moto naye umemuumba kwa udongo” Juz, 8 (7:12).

### 5. Wigo Mpana

Mafunzo yote ya kiislam yanaenea kwa wote; hayahusiki na mtu wala kikundi wala hayabagui:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّـهِ أَتْقَاكُمْ ﴿١٣﴾

“Hakika mtukufu wenu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mwenye takua zaidi” (49:13)

Hadith inasema: “Nyote mmetokana na Adam, na Adama ametokana na mchanga”.

### 6. Jihadi

Uislamu umelazimisha jihadi ya hali na mali dhidi ya dhulma na ufisadi kwa kila mwenye uwezo. Mwenyezi Mungu anasema:

“Nendeni mkiwa wepesi na wazito, na mpiganie jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, Hilo ni kheri kwenu mkiwa mnamjua.” Juz; 10 (9:41).

Imam Ali (a.s) anasema: **“Wallah! Lau si Mwenyezi Mungu kuchukua ahadi kwa Maulama kwamba wasiafiki kuvimbiwa kwa dhalim wala kufa njaa kwa aliyedhulumiwa, ningelitupilia mbali kamba yake na ningelim- nywesha wa mwisho wake kwa glasi ya wa mwanzo wake na dunia yenu hii kwangu ingelikuwa ya upuzi kuliko kamasi za mbuzi.”**

Ustadh Muhammad Sa’d Jalal, katika Jarida la Al-katib la Misr anasema, ninamnukuu: “Makusudio ya Imam (Ali) ni kuwa lau si ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa maulama kutokubali tofauti mbaya baina ya watu katika kula; ambapo wengine wanavimbiwa kwa kula ili wengine wawe na njaa, basi asingeli- fanya juhudi ya kuitaka haki yake ya ukhalifa ambayo ndiyo nyenzo ya kuthibitika uadilifu wa kuzuia tofauti iliyotajwa. Kwa hiyo jihadi yake haikuwa kwa ajili ya kutamani utawala na manufaa ya nafsi yake; isipokuwa ilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza hukumu ya uadilifu wa kijamii katika kugawa utuajiri kwa waislamu wote kwa namna ambayo hatakuweko mwenye kuvimbiwa kwa kula wala mwenye utapia mlo.”

### 7. Mali Ni Ya Mwenyezi Mungu

Vyote vilivyomo ulimwenguni ni mali ya Mwenyezi Mungu na binadamu ni wakala wa vile vilivyomo mikononi mwake. Kwa hiyo ni juu yake kutotumia ila kwa idhini na amri ya yule mwenyewe anayemuwakilisha: “Ni vyake vilivomo mbinguni na vilivyo katika ardhi na viliomo baina yao na viliyomo chini ya ardhi” (20:6) (57:7) Angalia Juz; 4 (180).

### 8. Uislamu Na Maisha

Uislamu unalenga binadamu aishi katika uwiano unaokwenda sambamba na nidhamu ya ulimwengu na mahitaji ya maisha:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّـهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ﴿٢٤﴾

Enyi mlioamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapowaita kwenye lile litakalowapa uhai, juz.9 (8:24).

Angalia maelezo yake huko, Hivi karibuni kimetoka kitabu kipya cha mwandishi Wilfred Smith, Anasema katika kitabu hicho: "Waislamu wana uwezo, kulingana na dini yao, wa kuleta maendeleo pamoja na mahitaji ya sayansi na kuchangia katika kutengeneza jamii itakayoongozwa na maendeleo ya kijamii kwa uadilifu na heshima."

Na kwamba wale wasioamini Akhera tumewaandalia adhabu chungu.

Hakuna tofauti baina ya anayemkufuru Mwenyezi Mungu na anayekufuru siku ya mwisho. Kwa sababu kukataa kurudishwa viumbe baada ya kufa, maana yake ni kuwa Mwenyezi Mungu hawezi hilo; na hivyo hasa ni kufuru.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Namstaajabu yule anayemtilia shaka Mwenyezi Mungu naye anaona umbile lake; na namstaajabu yule anayekanusha ufufuo wa Akhera naye anaona ufufuo wa kwanza."**

Na mtu huomba shari kama vile aombavyo kheri.

Katika maisha haya kuna huzuni na furaha, tamu na chungu, Hakuna kimo- jawapo kinachodumu. Ni kuanzia hapa ndio ikasemwa: 'siku ni mbili: kuna siku yako na siku ya kwako.' Lakini baadhi ya watu wanapopatwa na jambo baya lolote wanalalamika na mishipa kuwasimama, wakidhani kuwa wako kwenye matatizo makubwa yasiyotatulika. Kwa hiyo wanajiombea shari, kama wanavyojiombea heri. Na hii ni aina ya ujinga na upumbavu. Lau wangelingojea siku kidogo tu, matatizo yangeliondoka pamoja na siku zinavyokwenda

Na mtu amekuwa ni mwenye pupa katika kujiombea shari bila ya kuwa na subira na uvumilivu.

Makusudio ya mtu hapa ni baadhi sio watu wote. Kwenye Nahjul-balagha kuna msemo huu: "Msilifanyie haraka lile linalokuwa kwa kungojewa, Wala msione kuchelewa litakalokuja kesho, Ni mangapi yaliyopatikana yakidhaniwa hayatapatikana?"

Na tumeufanya usiku na mchana kuwa ni ishara mbili.

Ni dalili mbili za kuweko Mwenyezi Mungu; Kwa sababu zinafuatana kulingana na kanuni thabiti na nidhamu ya kudumu kwenye maelfu ya miaka; hakuna hata mwaka mmoja uliotufautiana na mwingine. Yote hayo, na mengine mfano wake, ni dalili mkataa ya kuweko mpangiliaji mzuri na mhandisi mwenye ujuzi wa hali ya juu sana.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawapa mwito wataalamu na wenye fikra kumwamini Yeye kupitia kufikiria vizuri na kuzingatia maumbile ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, jinsi vilivyopangiliwa kwa utaalamu wa hali ya juu; kama vile kufuatana usiku na mchana na mengineyo yanayoonekana ulimwenguni.

Ama wale watu wa kawaida anawalingania kwa kukumbuka neema zake:

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَـٰذَا الْبَيْتِ ﴿٣﴾ الَّذِي أَطْعَمَهُم مِّن جُوعٍ وَآمَنَهُم مِّنْ خَوْفٍ ﴿٤﴾

Basi na wamwabudu Mola wa nyumba hii, ambaye amewaliwasha kutokana na njaa na akawasalimisha na hofu (106: 3-4).

Tunasema hivi huku tukijua kuwa miito yote miwili (kufikiria maumbile na neema) inaweza kuwa pamoja.

Tena tukaifuta ishara ya usiku.

Kusema ishara ya usiku ni kubainisha; maana yake ni hiyo hiyo ishara ambayo ni usiku.

**Unaweza kuuliza kuwa**: dhahiri ya neno kufuta ni kuondoka kabisa na inajulikana usiku upo kwa hisia na kuona?

Makusudio ya kufuta hapa ni kuondoka athari ya kiutendaji. Kwa sababu watu wanatulia kinyume na mchana ambapo watu wanafanya kazi na kuhangaika huku na huko. Kwa hiyo linalofutwa hapa ni ule utulivu. Mwenyezi Mungu anasema:

وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا ﴿٩٦﴾

Ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu, Juz. 6 (6:96)

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾

Na tukaufanya usiku kuwa ni sitara na mchana kuwa ni wakati wa maisha (78:10–11).

Na tukaifanya ishara ya mchana ni ya kuangazia kila kitu kionekane ili mtafute fadhila itokayo kwa Mola wenu.

Usiku ni wa utulivu na kupumzika na mchana ni wa kutafuta riziki kwa mkono na kutoka jasho, sio kwa kughushi, hila, hiyana na kuwa kibaraka ili mtafute fadhila kutoka kwa ofisi za mabalozi na za upelelezi. Fadhila ya Mwenyezi Mungu inatolewa kwa kila mwenye kuitaka; nayo ni bora na ni yenye kubaki, tena ni safi na twahara.

“Ewe Mola tujaalie tutosheke na halali yako tusiwe na haja na haramu yako na tutosheke na twa yako tusiwe na haja na maasi yako na fadhila yako tusiwe na haja ya kumuomba asiyekuwa Wewe”

Na mpate kujua idadi ya miaka na hisabu.

Tumelizungumzia hilo kwa ufafanuzi katika Juz; 10 (9:36).

Na kila kitu tumekifafanua waziwazi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametubainishia halali na haramu, akatuwekea hoja, dalili na mawaidha. Mwema ni yule aliyejikomboa na matamanio na akajikwamua na hawa ya nafsi yake.

وَكُلَّ إِنسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَائِرَهُ فِي عُنُقِهِ وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٣﴾

13. Na kila mtu tumemfungia ndege wake shingoni mwake, Na siku ya Kiyama tutamtolea kitabu atakachokikuta kimekunjuliwa.

اقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٤﴾

14. Soma kitabu chako! Nafsi yako leo inakutosha kukuhisabu.

مَّنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ وَمَن ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ وَمَا
كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾

15. Anayeongoka hakika anaongoka kwa faida ya nafsi yake tu, na anayepotea anapotea kwa hasara ya nafsi yake tu. Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine, Wala sisi hatuadhibu mpaka tupeleke Mtume.

## NDEGE SHINGONI

**Aya 13 – 15**

## LUGHA

Makusudio ya ndege hapa ni matendo ya mtu ya kheri na shari. Waarabu walikuwa wakiona ni bahati njema ndege anayekuja upande wa kuume kwa sababu mtu anaweza kumpiga na wakiona ni kisirani ndege akitokea upande wa kushoto, kwa sababu hawezi kumpiga.

Ndio likaazimwa neno ndege kwa matendo ya heri na shari[1].1 Shingoni mwake ni fumbo la kuwa nayo; kama vile amefunga koja au mkufu.

## MAANA

Aya hizi tatu zinatofautiana kimatamshi, lakini zinashabihiana kimaana, Kauli yake Mwenyezi Mungu: Na kila mtu tumemfungia ndege wake shingoni mwake ni fumbo la kuwa mtu peke yake ndiye mwenye jukumu la matendo yake. Na kauli yake:

Na siku ya Kiyama tutamtolea kitabu atakachokikuta kimekunjuliwa.

Maana yake ni kuwa mtu kesho hataweza kuficha kitu chochote katika mambo aliyoyatenda:

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِن سُوءٍ تَوَدُّ لَوْ أَنَّ بَيْنَهَا وَبَيْنَهُ أَمَدًا بَعِيدًا ﴿٣٠﴾

"Siku ambayo kila nafsi itakuta kheri iliyoitenda imehudhurishwa Na iliyoyatenda katika uovu, itapenda lau kungekuwa na masafa marefu baina ya uovu huo na yeye." Juz. 3(3:30)

Kwa maelezo zaidi angalia huko.

Pia kauli yake Mwenyezi Mungu: Soma kitabu chako! Nafsi yako leo inakutosha kukuhisabu.

Hakuna haja ya shahidi wala mhasibu kesho; Kwa sababu mtu mwenyewe atajishuhudia na atajihisabu. Twabrasi anasema: "Atakuwa anajihisabu mwenyewe kwa sababu Siku ya Kiyama atakapoyaona matendo yake yote yameandikwa na kuona malipo yake pia yameandikwa kwa uadilifu, hayakupunguwa wala kuzidishiwa adhabu hata kidogo, atakiri na kukubali yeye mwenyewe, wala hatakuwa na hoja wala upinzani, Itawadhihirikia watakaofufuliwa kuwa hakuna dhulma.

Anasema Hasan: **"Ewe mwanadamu! Amekufanyia insafu yule aliyekufanya ujihisabu mwenyewe."**

Anayeongoka hakika anaongoka kwa faida ya nafsi yake tu, na anayepotea anapotea kwa hasara ya nafsi yake tu.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (6: 104) na Juz. 11 (10: 108).

Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (6:164), Wala sisi hatuadhibu mpaka tupeleke Mtume.

Angalia Juz. 2 (2:159) kifungu cha 'Ubaya wa adhabu bila ya ubainifu'.

---

1. Hata Waswahili pia hulitumia neno ndege kwa maana ya bahati njema au kisir- ani, wanasema: ndege mzuri au ndege mbaya - Mtarjumu.

4

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَإِذَا أَرَدْنَا أَن نُّهْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا فَحَقَّ عَلَيْهَا الْقَوْلُ فَدَمَّرْنَاهَا تَدْمِيرًا ﴿١٦﴾

16. Tunapotaka kuangamiza mji, huwaamrisha wapenda anasa wake, lakini hufanya maovu humo; basi hapo kauli huhakikika katika mji huo na tukauangamiza maangamizo makubwa.

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِن بَعْدِ نُوحٍ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

17. Na karne ngapi tumeziangamiza baada ya Nuh? Na Mola wako anatosha kuwa ni mwenye habari na mwenye kuona dhambi za waja wake.

مَّن كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَن نُّرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصْلَاهَا مَذْمُومًا مَّدْحُورًا ﴿١٨﴾

18. Anayetaka ya upesi upesi (dunia) tutamharakishia humo tunayoyataka kwa tunayemtaka; kisha tunamwekea Jahannam; ataiingia hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa mwenye kufurushwa.

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُم مَّشْكُورًا ﴿١٩﴾

19. Na mwenye kutaka ya mwisho (Akhera) na akayahangaikia kwa mahangaikio yake huku akiwa ni mumin, basi hao mahangaikio yao yatakuwa ni yenye kushukuriwa.

كُلًّا نُّمِدُّ هَٰؤُلَاءِ وَهَٰؤُلَاءِ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿٢٠﴾

20. Wote hao tunawasaidia, hawa na hao, katika atia za Mola wako; na atia za Mola wako hazizuiliki.

انظُرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَلَلْآخِرَةُ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿٢١﴾

21. Angalia jinsi tulivyowafad- hilisha baadhi yao kuliko wengine. Na Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na fadhila kubwa zaidi.

## TUNAWAAMRISHA WAPENDA ANASA WAKE

**Aya 16 -21**

### LUGHA

Neno ‘mutraf,’ambalo tumelifasiri kwa neno wapenda anasa, lina maana ya wale ambao wanastarehe watakavyo.

### MAANA

Nilipofikia kufasiri Aya hii (tunawaamrisha watanasi wake), nilikumbuka swali nililoulizwa na mmoja wa mahatibu wa Iraq akisema: Kwa nini unawatukana wapenda anasa kwenye vitabu vyako? Nami nikamuuliza: Kwanini wewe unawatetea? Je, wewe ni mmoja wao? Au ni kwa vile wao ni mawalii wa neema zako? Basi akarudi nyuma na swali lake na akaomba msamaha. Hili limenifanya niieleze Aya hii kwa mfumo ufuatao:

1. Mbali ya neno ‘utajiri,’ neno ‘wapenda anasa’ pamoja na mnyumbuliko wake limekuja mara nane katika Qur’an; kama ilivyoelezwa

katika Murshid, Katika Nahjulbalagha neno hili limeelezwa mara nyingi. Halikutajwa neno wapenda anasa ila pamoja na shutuma.

2. Watu wa Lugha wamesema: Neno Taraf katika mnyumbuliko wake linatumika hivi: Amejitanaasi mtu, kwa maana ya kujineemesha. Ameitanasi mali, kwa maana ya kuifuja. Pia neno hilo linakuwa kwa maana ya uovu na kiburi, Haya ndio maelezo yake kilugha. Ama sifa yake iliyotajwa katika Qur'an na kwengineko ni: Kughafilika na Mwenyezi Mungu, kuwafanyia uovu waja wa Mwenyezi Mungu, kuifanyia kiburi amri ya Mwenyezi Mungu na kuwapiga vita mawalii wa Mwenyezi Mungu. Vile vile kujifaharisha kwa wingi, kujiona, unyanyapaa na mengine mengi ya shutuma; isipokuwa yule aliyehurumiwa na Mungu na akajihurumia mwenyewe.

3. Tunapotaka kuangamiza mji, huwaamrisha wapenda anasa wake, lakini hufanya maovu humo; basi hapo kauli huakikika katika mji huo na tukauangamiza maangamizo makubwa.

Linaoamriwa ni uadilifu na twaa; yaani tunawamrisha uadilifu na utiifu. Wafasiri wametaja njia nne katika maana ya Aya hii. Yenye nguvu zaidi ni ile inayosema kuwa Mwenyezi Mungu amelitumia neno wapenda anasa kwa watu wote wa mji, katika mtindo wa kutumia sehemu kwa maana ya yote.

Mfano huu katika maneno ya waarabu unatumika sana, ikiwa hiyo sehemu ni muhimu zaidi; kama jicho katika mwili, wamelitumia kwa mstari wa mbele katika jeshi; kwa sababu jicho ni kiungo muhimu katika mwili[1]1

Kwa kuwa wapenda raha ni wepesi zaidi na wajasiri wa kufanya maasi kuliko wengine, ndio ikafaa kulitumia neno hilo kwa watu wote wa mji; kama linavyotumika jicho kwa mtu.

Kwa hiyo basi maana ya Aya yanakuwa kwamba Mwenyezi Mungu hawaangamizi watu wa mji ila wakistahili hilo baada ya kuwekewa hoja kwa kutumwa mtume awaamrishe kheri, kuwakataza uovu, kuwahadharisha na uhalifu na maasi. Wakifanya uovu na kutoka kwenye utiifu, basi linahakika neno la adhabu juu yao na Mwenyezi Mungu huwateremshia maangamizi.

Ni kweli maana haya yanawafikiana na matamshi ya Aya, wala hayakataliwi na akili, lakini sisi tutaifasiri kwa njia njingine; kama ifuatavyo: Jamii yoyote iliyo na wapenda anasa, kwa maana tuliyoyataja, basi ni jamii inayoishi kwenye nidhmu ya ufisadi na dhulma. Kwani kuweko kwao ni sawa kabisa na kuweko saratani katika mwili.

Wa kulaumiwa kwanza kabisa kwa kupatikana wafisadi ni jamii yenyewe; kwa vile haikusimama kidete kuwapinga au angalu kutowaunga mkono; bali wanawabatiza majina ya waheshimiwa, kuwatukuza, kuwapa kura na kuwapa uongozi.

Hapa ndio inakuwa jamii yenyewe ni mshiriki kamili wa wapenda anasa na wafisadi katika makosa na madhambi yao yote na wanastahiki maangamivu; sawa na wapenda anasa.

---

1. Hata Waswahili pia hutumia mfumo huu; kwa mfano wanasema: 'huyu ndiye jicho letu' kwa maana ya mtu muhimu.

Kuna Hadith isemayo: **"Mwenye kuridhia dhulma ni kama mwenye kuifanya"** "Mwenye kuinyamazia haki ni kama shetani bubu" Ikiwa mambo ni hayo itakuwaje kwa yule mwenye kuiridhia batili?

Anasema Seyyid Afghani: "Ewe mkulima unayechimba ardhi kwa jembe lako kwa nini usilitumie jembe hilo kuuchimba moyo wa anayekufanya mtumwa?" Tazama Juz; 13 (13:11).

Kwa hakika maangamizi yako aina nyingi; Yanaweza kuwa tufani tetemeko la ardhi, vimondo n.k. Vile vile yanaweza kuwa kwa udhalili na kusalitiwa shari.

Aina hii ni mbaya na ya kufedhesha zaidi. Wameadhibiwa nayo umma wa Muhammad **(s.a.w.w)** pale walipoacha jihadi, wakawafumbia jicho wafisadi na washari na wakaukubali udhalili na unyonge.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Hakika kwenye utawala wa kiislamu kuna hifadhi ya mambo yenu, basi upeni utiifu wenu…; Wallahi ni lazima mfanye hivyo au Mwenyezi Mungu atauondoa kwenu utawala wa kiislamu kisha usirudi kwenu kabisa mpaka mambo yarudie kwa wengine wasiokuwa nyinyi."**

Yaani tukiutii Uislamu tutaishi kwenye ngome imara tukiwa na hadhi na heshima; vinginevyo utawala utahama kwenda kwa maadui zetu, kisha usirudi kwetu; Kila ninaposoma onyo hili basi hujisikia natetema.

Na karne ngapi tumeziangamiza baada ya Nuh?

Makusudio ya karne hapa ni watu. Hii ni hadhari na ahadi kwa wale wanaomkadhibisha Muhammad **(s.a.w.w**) kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni muweza wa kuwafanya kama alivyowafanya wale waliowakadhibisha Mitume waliokuwa kwenye karne zilizopita; kama vile Ad na Thamud:

أَفَأَمِنُوا مَكْرَ اللَّـهِ ۚ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّـهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٩٩﴾

"Je, wamejiaminisha na hila ya Mwenyezi Mungu? Hawaaminishi hila ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye hasara." Juz; 9 (7:99).

Imam Ali (a.s) amesema: **"Hakika radhi ya Mwenyezi Mungu kwa waliobaki ni moja na uchukivu wa Mwenyezi Mungu kwa waliobaki ni mmoja. Jueni kuwa Yeye hataridhia chochote alichokichukia kwa waliokuwa kabla yenu wala hatachukia chochote alichowaridhia waliokuwa kabla yenu"**

Na Mola wako anatosha kuwa ni mwenye habari na mwenye kuona dhambi za waja wake.

Kwa hiyo atamwadhibu anavyostahiki, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alisema kumwambia Abu dharr: **"Hakika mumin anaziona dhambi ni jiwe kubwa analohofia kumwangukia na kwamba kafiri anaona dhambi zake ni kama nzi tu anayepita puani mwake."**

Anayetaka ya upesi upesi (dunia) tutamharakishia humo tunayoyataka kwa tunayemtaka.

Sio kuwa kila alitakalo mtu anapewa na Mungu, Kwani sisi huwa tunataka mambo mengi na hayawi. Ispokuwa makusudio ya Aya ni kuwa mwenye kufanya kwa ajili ya dunia tu, bila ya kuamini chochote isipokuwa manufaa yake, basi atapata matunda ya kazi yake na juhudi yake kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, kwani mja hawezi kufikia jambo lolote kama Mungu akikataa, hata kama atafanya kazi usiku na mchana. Hakika

Mwenyezi Mungu hatupi tunayoyataka ila kwa kutaka kwake. Hayo ndio makusudio ya 'tunayoyataka kwa tunayemtaka'

Kisha tunamwekea Jahannam; ataiingia hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa mwenye kufurushwa.

Kwa vile yeye anaamini masilahi yake tu na haoni umuhimu wowote isipokuwa nafsi yake, wala hafanyi lolote isipokuwa kwa ajili yake.

Na mwenye kutaka ya mwisho (Akhera) na akayahangaikia kwa mahangaikio yake huku akiwa ni mumin, basi hao mahangaikio yao yatakuwa ni yenye kushukuriwa.

Makusidio ya kuyahangaikia kwa mahangaikio yake ni kutaka kheri na kuifanya na kuiamini si kwa chochote isipokuwa kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu na kheri. Anayefanya hivi ndiye anayestahiki daraja na cheo mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya watu.

Ama anayefanya kwa ajili ya faida na biashara basi yake ni Jahannam. Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anasemama: "Ambaye Hijra yake (kuhama kwake) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi Hijra yake ni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na ambaye hijra yake ni kwa ajili ya kuipata dunia au mwanamke amuoe, basi Hijra yake ni kwa lile alilololi- hajiria.

Muhtasari wa yote haya ni kuwa Uislamu ni njia inayomuelekeza mtu kufanya kheri na kuiacha shari hiyo yenyewe. Kwa hiyo itakuwa ni lazima kusema ukweli kwa kuwa ni lazima kufanya hivyo na ni lazima kujiepusha na uongo kwa kuwa ni lazima kujiepusha. Mtume **(s.a.w.w)** ameutolea ibara mwelekeo huu kwa kusema: **"Hakika nimetumwa kutimiza tabia njema."** Ilivyo hasa ni kuwa tabia njema haiwi ila ikiwa imetakata na kila uchafu.

Wote hao tunawasaidia, hawa na hao,

Hiyo ni ishara ya makundi yote mawili: wale wanaotenda kwa ajili ya dunia na wale wanaotenda kwa ajili ya akhera.

Katika atia za Mola wako; na atia za Mola wako hazizuiliki.

Atia (vipawa) za Mwenyezi Mungu kwa mtu zinaanzia tangu kuumbwa kwake na kuweko kwake ambako hakupatikani ila kwake tu; kisha sababu za kubakia kwake na kukua kwake. Atia hizi zinamhusu mwema na muovu. Ama atia zake katika akhera zitawahusu wema wanaomcha Mungu tu.

Angalia jinsi tulivyowafadhilisha baadhi yao kuliko wengine.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) hawagawanyi watu kwenye tabaka, wala kuto- fautiana katika haki za kibinadamu kwa mtu binafsi au makundi. Vipi iwe hivyo na hali yeye ndiye aliyesema:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّـهِ أَتْقَاكُمْ ﴿١٣﴾

"Hakika mtukufu wenu zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mwenye takua zaidi katika nyinyi" (49:13).

Kwa hiyo basi kuzidiana watu katika dunia, katika isiyokuwa haki ya kibinadamu, inafaa; kama vile afya, umri, riziki kupitia kufanya kazi, kurithi au njia nyingine yoyote aliyoihalalisha Mungu. Lakini utajiri unaokuja kwa ulanguzi, hila na uporaji unatokana na shetani, wala haifai kuunasibisha na Mwenyezi Mungu.

Na akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na fadhila kubwa zaidi.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja kuwa watu wanatofautiana katika dunia, sasa anasema kuwa huko Akhera pia itakuwako tofauti, lakini

huko tofauti ni kubwa sana. Kwani sifa zinazowatofautisha hapa ni utajiri na ufukara, elimu na ujinga, maradhi na siha na umri mrefu na mfupi; kisha wote wanaishia kwenye mauti kwa usawa, hata wema na waovu. Ama sifa watakazotofautiana huko Akhera, ni kuungua katika moto na kuwa kwenye neema na furaha. Wapi na wapi tofauti hii na ile.

لَّا تَجْعَلْ مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُومًا مَّخْذُولًا ﴿٢٢﴾

22. Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukabaki ni mwenye kukalaumiwa uliyetupwa.

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۚ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا

فَلَا تَقُل لَّهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾

23. Na Mola wako amepitisha kuwa msimwabudu yoyote ila Yeye tu na kuwatendea wema wazazi wawili. Mmoja wao akifikia uzee naye yuko kwako au wote wawili, basi usiwaambie Ah! Wala usiwakemee, Na sema nao kwa msemo wa heshima.

وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُل رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

24. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma na useme: Mola wangu! Warehemu kama walivyonilea utotoni.

رَّبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۚ إِن تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غَفُورًا ﴿٢٥﴾

25. Mola wenu ni Mjuzi zaidi wa yaliyo katika nafsi zenu, ikiwa nyinyi mtakuwa wema. Hakika Yeye ni Mwenye kughufiria wanaorejea kwake.

## USIWAMBIE AH!

**Aya 22 – 25**

### MAANA

Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukabaki ni mwenye kulaumiwa uliyetupwa.

Maneno haya anaambiwa kila mtu, sio Mtume **(s.a.w.w)** kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu: 'mmoja wao akifikia uzee naye yuko kwako au wote wawili; Na inajulikana kuwa Mtume alikuwa yatima.

Na Mola wako amepitisha kuwa msimwabudu yoyote ila Yeye tu na kuwatendea wema wazazi wawili. Mmoja wao akifikia uzee naye yuko kwako au wote wawili, basi usiwaambie Ah! Wala usiwakemee, Na sema nao kwa msemo wa heshima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma na useme: Mola wangu! Warehemu kama walivyonilea utotoni.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekutanisha shukrani ya wazazi wawili na shukrani yake na akawajibisha kuwatendea wema. Kuna Hadith isemayo: "Kuna mtu mmoja alikwenda kwa Mtume **(s.a.w.w)** akimtaka idhini ya kupigana jihadi pamoja naye. Akamuuliza: je, Wazazi wako wako hai? Akasema: Ndio. Akasema mtume: basi fanya jihad kwao.

Kauli yake Mwenyezi Mungu: 'kama walivyonilea utotoni,' ni ishara ya kuwa wao walijitolea nafsi zao kwa ajili yake, wakakesha usiku ili yeye alale, wakawa na njaa ili ashibe yeye na wakawa uchi ili yeye avae. Na hili ni deni shingoni mwake, ni wajibu alilipe atakapokuwa na nguvu na wao

kuwa dhaifu, na kuwachukulia kwenye uzee wao sawa na wao walivyomchukulia alipokuwa mdogo, na wao wamemzidi kwa kumtangulia.

Imam Zaynul-abidin (a.s) anasema akiwaombea Mungu wazazi wake: “Ewe Mola wangu! Ni wapi na wapi urefu wa shughuli yao ya kunilea mimi? Ni wapi na wapi shida ya tabu yao ya kunilinda mimi? Ni wapi na wapi kujinyima kwao kwa jili ya kunifurahisha mimi? Ni mbali kwa mbali kabisa na jinsi walivyotekeleza haki yao kwangu; ni mbali kwambali yote hayo na jinsi ninavyowafanyia! Wala mimi sijatekeleza wadhifa wa kuwahudumia.”

Kila mmoja kati ya baba na mama anajitolea kwa nafsi yake na pumzi zake zote kwa ajili ya mtoto, kisha hataki malipo wala shukrani yoyote. Analotamani ni kuwa mtoto wake awe ni mtu mwenye kutajika. Nimepata mtihani wa kuwa baba, lakini wazazi wangu hawakuupata mtihani huo, kwa sababu nilikuwa yatima wa baba na mama.

Ninasema nimepatwa na mtihani huo, kwa sababu mimi sioni raha yoyote katika maisha haya isipokuwa raha ya mwanangu wa kike na kiume. Tabasamu moja tu ya mmoja wao kwangu ni sawa na dunia na vilivyomo ndani yake na hasononeki yoyote kati yao ila huwa ninahisi kuna mkono unatoa roho yangu iliyo mbavuni mwangu.

Mola wenu ni Mjuzi zaidi wa yaliyo katika nafsi zenu, ikiwa nyinyi mtakuwa wema. Hakika Yeye ni Mwenye kughufiria wanaorejea kwake.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) anajua maazimio, kama anavyojua kauli na vitendo na kumlipa kila mmoja kulingana na nia yake. Mwenye kufanya uovu kisha akatubia sawasawa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, mwenye kurehemu.

Hiii ni tahadhari kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa yule mwenye kuwaudhi wazazi wake na akawa anawaona ni mzigo kwake, kama ambavyo pia ni hadhari ya kuacha ikhlasi katika kauli na vitendo.

5

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَآتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾

26. Na mpe jamaa wa karibu haki yake na maskini na mwana njia, wala usifanye ubadhirifu.

إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيَاطِينِ ۖ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٧﴾

27. Hakika wabadhirifu wamekuwa ni ndugu wa mashetani, na shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake.

وَإِمَّا تُعْرِضَنَّ عَنْهُمُ ابْتِغَاءَ رَحْمَةٍ مِّن رَّبِّكَ تَرْجُوهَا فَقُل لَّهُمْ قَوْلًا مَّيْسُورًا ﴿٢٨﴾

28. Na ikiwa unajipurukusha nao kwa kutaraji rehema ya Mola wako, basi sema nao maneno laini.

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٩﴾

29. Wala usiufanye mkono wako umefungwa shingoni mwako, wala usiunyooshe wote kabisa, utabaki mwenye kulaumiwa, mwenye kuishiwa.

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۚ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٣٠﴾

30. Hakika Mola wako humkunjulia riziki amtakaye na humpimia amtakaye. Hakika Yeye kwa waja wake ni mwenye habari, aonaye.

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۚ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾

31. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa kuishiwa, sisi tutawaruzuku nyinyi na wao . Hakika kuwaua ni hatia kubwa.

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنَىٰ ۖ إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

32. Wala msiikurubie zinaa; Hakika hiyo ni uchafu na njia mbaya.

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ وَمَن قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لِوَلِيِّهِ سُلْطَانًا فَلَا يُسْرِف فِّي الْقَتْلِ ۖ إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

33. Wala msiiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuiua), ila kwa haki. Na aliyeuliwa kwa kudhulumiwa, basi tumempa madaraka walii wake, lakini asipetuke mpaka katika kuua, kwani hakika yeye anasaidiwa.

وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۚ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۖ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾

34. Wala msiikurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi, mpaka afikie kukomaa kwake; Na tekelezeni ahadi. Hakika ahadi itasailiwa.

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾

35. Na timizeni kipimo mnapopima, na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni kheri kweni na hatima njema.

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۚ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَٰئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٦﴾

36. Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo. Hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitasailiwa.

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَن تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

37. Wala usitembee katika Ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.

كُلُّ ذَٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهُ عِندَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾

38. Hayo yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako.

ذَٰلِكَ مِمَّا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ۗ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ فَتُلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٩﴾

39. Hayo ni katika hekima alizokupa wahyi Mola wako. Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukalaumiwa, uliyetupwa.

## WASIA 10

**Aya 26 – 39**

### MAANA

1. Na mpe jamaa wa karibu haki yake na maskini na mwana njia wala usifanye ubadhirifu.

Amenukuu Tabrasi katika Majmaul-bayan kutoka kwa Assadiy, ambaye ni miongoni mwa wafasiri wakubwa, kwamba makusudio ya jamaa wa karibu ni jamaa wa Mtume **(s.a.w.w)**.

Abu Hayan Al-andalusi amenukuu kutoka kwa Imam Ali bin Husein (a.s) kwamba yeye amesema: “Hao ni jamaa wa Mtume **(s.a.w.w)**, Mwenyezi Mungu ameamrisha kuwapa haki yao kutoka katika hazina.

Amesema Abu Bakar Al-mua’firi Al-maliki katika Ahkamul-qur’an: “Anaingia katika jamaa wa karibu jamaa wa Mtume kuingia kwa kutangulia na kwa njia ya aula tu. Lakini hakika Aya ni ya ndugu wa mtu walio karibu zaidi. Ama jamaa wa karibu wa Mtume Mwenyezi Mungu amebainisha kuwahusu wao na akaeleza kwamba kuwapenda ndio ujira wa Mtume kwa yale aliyotuongoza.”

Imesemekana kuwa makusudio ya jamaa wa karibu ni yule ambaye ana haki ya kumtunza na kurithi, masikini ni muhitajia na mwananjia ni msafiri aliyekatikiwa njiani asiyekuwa na uwezo wa gharama za kurudi kwao. Hawa wawili wana haki ya zaka; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ

وَفِي سَبِيلِ اللَّـهِ وَابْنِ السَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّـهِ ۗ وَاللَّـهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

“Hakika sadaka ni ya (hawa) tu: Mafukara na masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao na kuwakomboa watumwa na wenye madeni na katika njia ya Mwenyezi Mungu na mwana njia.” Juz.10 (9:60).

Hakika wabadhirifu wamekuwa ni ndugu wa mashetani, na shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameleta ibara ya wabadhirifu kuwa ni ndugu wa shetani, kwa sababu ubadhirifu ni jambo linalochukiwa na Mwenyezi

Mungu na kila linalochukiwa na Mwenyezi Mungu linapendeza kwa shetani.

Hakuna anayetofautiana na wenzake kuwa maana ya ubadhirifu ni kutoa mali kwenye njia isiyokuwa yake na kuiweka mahali pasipokuwa pake, iwe kwa uchache au kwa wingi. Kwa ibara ya watu wa mantiki ni kwamba ubadhirifu ni katika aina si katika idadi.

**Unaweza kuuliza kuwa**: kauli ya isiyokuwa njia yake na pasipokuwa mahali pake inafanana na maneno yenye kutatiza ambayo yanahitaji ufafanuzi na maelezo; basi ni ipi hiyo njia yake na mahali pake?

**Jibu**: kila mwenye kutumia mali yake katika mambo yanayomletea madhara au yasiyokuwa na manufaa yoyote, basi huyo ni mwenye israfu, mbadhirifu na safihi, kikawaida na kisharia; isipokuwa mali anayoitoa kwa ajili ya kuvuta sigara. Tumedokeza kuhusu matumizi mabaya na kuzuiliwa kutumia matumizi ya kimali kwa mwenye kufanya hivyo, katika Juz. 4 (4:5).

## WAKO WAPI WAADILIFU?

**Swali la pili** linaweza kuja hivi: Mtu ametumia mali yake kwa kunywa pombe, kula nyama ya nguruwe na mengineyo katika yaliyoharamishwa ambayo yanamletea manufaa ya sasa na madhara ya muda ujao. Mtu huyu watu wengi hawamuoni kuwa ni mbadhirifu wala safihi; sasa je, sharia ya kiislamu inawajibisha kuzuiliwa matumizi ya kimali, kwa vile yeye ni safihi mwenye kufanya israfu?

**Jibu**: Mtu mwenye akili anayo ruhusa ya kutumia mali yake bila ya kuiingiliwa; awe mumin au kafiri, fasiki au mwadilifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Mkiwaona wana uwekevu, basi wapeni mali zao" Juz. 4 (4:6) na wala hakusema mkiwaona wana uwekevu wa dini au uadilifu. Imepokewa Hadith Mutawatur kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** kwamba yeye amesema: "Watu wamesalitiwa na mali zao," na wala hakusema waumini au waadilifu.

Kwa hiyo sharti pekee la kusihi matumizi haya ni uwekevu katika mali si katika dini. Lau ingelikuwa uadilifu na uongofu ni sharti la kusihi matumizi ya mtu katika mali yake, basi nidhamu ingeliharibika na maisha yangesimama, kwa sababu watu wa duniani wako kama tunavyowajua, tutawatoa wapi watu wa dini na waadilifu?

Hanafi, Malik na Hambali wako katika rai yetu hii. Ama Shafii, wamesema kuwa uongofu ndio unaofaa katika dini na mali, kama ilivyoelezwa katika kitab Al-mughni cha Ibn Abi quddama.

Na ikiwa unajipurukusha nao kwa kutaraji rehema ya Moa wako, basi sema nao maneno laini.

Wakusema nao hapa ni jamaa wa karibu, masikini na msafiri aliyeishiwa njiani. Maana ni kuwa, akikuuliza kitu katika mali na wala usipate cha kumpa na ukamuomba Mwenyezi Mungu amtosheleze yeye na akutosheleze wewe kutokana na fadhila yake na rehema yake, basi sema naye kwa kauli laini kwa kumpa maneno mazuri yatakyompa matumaini na matarajio katika moyo wake. Kuna Hadith isemayo: " Ikiwa hamna wasaa wa kuwapa watu mali zenu basi mnao wasaa wa kuwapa maadili yenu" Mshairi naye anasema: Kutamka kuwe kwema ikiwa hali si njema.

2. Wala usiufanye mkono wako umefungwa shingoni mwako, wala usiunyooshe wote kabisa, utabaki mwenye kulaumiwa, mwenye kuishiwa.

Kipimo na uwiano ndio msingi wa kila kitu katika Uislam kiitikadi, kisharia na kimaadili; sio ki ulahidi na kiidadi ya waungu. Na si kwa kuondoa milki ya mtu wala kuweka milki ya utaghuti na wala sio udikteta wa kikundi cha watu au wa mtu mmoja wala si utawala wa kila anayetaka, sio utawa wala sio kuzama kwenye matamanio. Kila kitu kinakuwa na uhalali na uharamu:

وَكُلُّ شَيْءٍ عِندَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٨﴾

"Na kila kitu kwake, ni kwa kipimo" Juz; 13 (13:8).

Kusema kwake ni kwa kipimo ni kuwa na nidhamu inayoafikiana na hekima na masilahi, hakuna kupetuka mpaka wala kupetusha mipaka; wala hivi hivi au kombokombo. Kila kitu kina mpaka wake mbele ya Mwenyezi Mungu ambayo ni wajibu kwa kila mtu asimame kwenye mipaka hiyo bila ya kuikeuka. Kwa mfano mipaka ya hukumu na utawala ni uadilifu; mipaka ya kumiliki ni kutomdhuru mtu au watu; mipaka ya matumizi ni kutofanya uchoyo wala kufanya ubadhirifu na matendo mengineyo.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameuletea ibara uchoyo kwa kufunga mkono shingoni, kwa sababu mchoyo anazuia mkono wake kutoa. Na kauli yake: 'wala usiunyooshe wote kabisa' anakusudia mkono ambao hauzuii kitu. Mwisho wa wote hawa wawili ni mmoja – kuishiwa na lawama.

Mwenye israfu atauma mkono wa kuishiwa, kujuta na kulaumiwa mbele ya Mwenyezi Mungu, watu na yeye mwenyewe, pale atakapokuwa mikono mitupu; wakati ambapo bakhili analaumiwa na kila mtu, na kuishiwa kwake kesho ni zaidi kuliko mbadhirifu. Jambo bora zaidi ni wastani.

**Unaweza kuuliza**: Je, hii ina maana Uislamu unakubaliana na nadharia ya Socrates inayosema: Kila ubora ni kati ya mabaya mawili. Kwa hiyo ushujaa ni wastani baina ya kujitutumua na woga, ukarimu ni baina ya israfu na uchoyo, unyenyekvu ni baina ya kutahayari na kukosa haya nk?

**Jibu**: Hapana! Kwani Uislam unapanga ubora na kuweka sharia ya hukumu kwa misingi ya masilahi ya mtu mmoja mmoja hadi watu wengi. Kila jambo ambalo linaendeleza maisha basi ni wajibu wa lazima kwa kiongozi na wajibu wa kutosheana (kifaya) kwa raia.

Na kila lenye manufaa kwa upande fulani basi ni bora; bali ni ibada ya wajibu kwa kila mwenye uweza au suna kulingana na kiwango cha manufaa. Mwenyezi Mungu anasema:

وَأَمَّا مَا يَنفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ ﴿١٧﴾

"Ama kinachowafaa watu hukaa kwenye ardhi" Juz; 13 (13:17).

Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Bora ya watu ni yule wanayenufaika naye." Dalili wazi zaidi ya hakika hii ni kauli yake Mwenyezi Mungu: "Ambao wanamfuata Nabii asiyesoma wala kuandika ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Tawrat na Injili ambaye anawaamrisha mema na anawakataza maovu, na anawahalalishia vizuri na kuwaharamishia vibaya, na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao." Juz.9 (7:157).

Msingi huu wa Qur'an – masilahi - unaweza kulingana na nadharia ya wastani kwenye vitu vyenye wastani; kama vile ukarimu kuwa baina ya uchoyo na israfu. Lakini unatofautiana katika vitu visivyo na wastani; kama vile uaminifu ni dhidi ya hiyana, wala hakuna jingine la kuleta wastani kuwa ni baina ya uaminifu na hiyana; Tumezungumzia kuhusu maadili katika Juz. 6 (5:79).

Hakika Mola wako humkunjulia riziki amtakaye na humpimia amtakaye. Hakika Yeye kwa waja wake ni mwenye habari aonaye.

Makusudio ya kumpimia ni kuifanya finyu. Kila kitu kiko mikononi mwake, riziki na zisizokuwa riziki. Kwa sababu Yeye ni mmliki wa milki zote, lakini hekima yake imetaka na kupitisha kutomruzuku yeyote isipokuwa kwa sababu za kiulimwengu ambazo ameziumba na kuziwekea njia za kuchuma mali n.k. Angalia Juz. 6(5: 66) na Juz; 13 (13: 26).

3. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa kuishiwa, sisi tutawaruzuku nyinyi na wao pia. Hakika kuwaua ni hatia kubwa.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (6: 151).

4. Wala msiikurubie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu na njia mbaya.

Imekuwa ni uchafu kwa vile mwishilio wake ni kuvurugika na kuchanganyika nasaba. Inatosha zina kuwa ni uovu kwa vile ni katika sifa mbaya za kushutumiwa.

5. Wala msiiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuiua), ila kwa haki.

Umetangulia mfano wake katika katika Juz. 8 (6: 151).

Na aliyeuliwa kwa kudhulumiwa, basi tumempa madaraka walii wake, lakini asipetuke mpaka katika kuua, kwani hakika yeye anasaidiwa.

Kila aliyeuawa bila ya kufanya kosa linalowajibisha kuuliwa basi ameuawa kwa dhulma. Walii wa aliyeuawa ni ndugu zake kwa upande wa baba. Ikiwa hawako basi ni hakimu wa sharia. Kupetuka mpaka katika kuua ni kuua wawili kwa mmoja; kama walivyokuwa wakifanya wakati wa jahilia.

Maana ni kuwa ndugu wa aliyeuawa kwa dhulma wana haki ya kuua aliyeua au kuchukua fidiya; kama ilivyoelezwa katika Hadith tukufu: "Mwenye kuua basi watu wa aliyeuawa wana hiyari mbili: wakipenda wataua na wakipenda watachukua fidiya."

Kwa vile ndugu wa aliyeuawa wana haki hiyo, basi ni wajibu wa hakimu na kila mwislamu kusaidia kutimizwa haki hii; Yametangulia maelezo kuhusu haya katika Juz. 2 (2:178).

6. Wala msiikurubie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora zaidi, mpaka afikie kukomaa kwake.

Imekwishapita Aya kama hii kwa herufi zake katika Juz. 8 (6: 152).

7. Na tekelezi ahadi; Hakika ahadi itasailiwa.

Kila aliloliamrisha Mwenyezi Mungu na kulikataza ni wajibu kutekelezwa; ikiwa ni pamoja na mapatano ya bei, ajira n.k. Kwa maelezo zaidi angalia Juz. 6 (5:1).

Na timizeni kipimo mnapopima na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni kheri kwenu na hatima njema.

Kukamilisha kipimo ni wajibu wa kisharia na kidesturi; wala hauhusiki na dini kuliko dini nyingine au desturi kuliko desturi nyingine. Mwenyezi

Mungu (s.w.t) amehimiza kukamilisha kipimo kwa mifumo mbalimbali; kama vile: pimeni kwa mizani zilizo sawa, timizeni kipimo na mizani, wala msipunguze na wala msipetuke mipaka. Siri ya hilo ni kwamba ustawi wa jamii hauwezi kuwa bila ya usawa wa vipimo.

## KUSEMA BILA YA UJUZI

9. Wala usifuatilie ambalo huna ujuzi nalo. Hakika masikio na macho na moyo, hivyo vyote vitasailiwa.

Neno kufuatilia limefasiriwa kutokana na neno la kiarabu Qafwa lenye maana ya kufatilia athari ya jambo. Miongoni mwa majina ya Mtume **(s.a.w.w)** ni Almuqfi (mfuatiliaji) kwa vile yeye ni mtume wa mwisho.

Kusema jambo bila ya ujuzi ni vibaya hata kwa yule asiyemwamini Mungu na siku ya mwisho. Mwenyezi Mungu ametaja masikio, macho na moyo akikusudia mwenye vitu hivyo vitatu.

Na kwamba Yeye Mwenyezi Mungu ataviuliza na kuviadhibu ikiwa vitawekewa vitu visivyovijua; kama vile lau mtu atasema nimesikia naye hakusikia, nimeona naye hakuona au ni ninaitakidi na kuazimia naye hana itikadi wala maazimio yoyote.

Hakuna tofauti baina ya anayekusudia uongo na anayekurupuka kusema jambo bila ya kulithibitisha. Kwani kusema kwa dhana na shubha ni kusema bila ya ujuzi. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ﴿٣٦﴾

"Hakika dhana haifai kitu mbele yake haki" Juz; 11 (10:36)

إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ ﴿١١٦﴾

"Hawafuati ila dhana na hawakuwa ila wenye kuzua tu." Juz; 8 (6: 116)

Mwenyezi Mungu amelinganisha dhana na kuzua.

Kutokana na Aya hii yanajitokeza mambo yafuatayo:

(i) Kubatilika na uharamu wa Taqlid (kufuata) kwa yule mwenye uwezo wa kuchambua hukumu kutoka kwenye rejea zake. Kwa sababu ameacha elimu yake na akaumia elimu ya mwingine. Hii ni rai ya Shia Imamia. Zaydiya, Muu'tazila, Ibin Hazm, Sheikh Muhammad Abduh, Sheikh Shaltut na wengineo. Tumezungumza kwa ufafanuzi kuhusu taqlid katika Juz. 8 (2:259).

(ii) Uharamu wa kutoa hukumu kwa kutumia qiyas (kukisia) na istihsan (kuchukulia kuwa ni vizuri).

Qiyas ni kulinganisha jambo ambalo halikutajwa katika hukumu na jigine lililotajwa kutokana na kuwa na sababu moja.

Kwa mfano sharia kusema kuwa nyanya wa upande wa mama anarithi na ikanyamazia nyanya wa upande wa baba. Tukasema kuwa huyu pia atarithi kwa kukisia kuwa yeye pia ni nyanya.

Istihsan ilivyosimuliwa kutokana na Abu Hanifa ni kutoa hukumu kwa atavyoonelea mujtahidi kuwa ni vizuri bila ya kuweko dalili yoyote isipokuwa anavyoonelea yeye tu.

Rejea Kitabu Allami' fi usulilfiqh cha Abu Is-haq, Ibrahim bin Ali bin Yusuf Fayruz Abadiy, uk; 65 chapa ya 1939. Mwenya kitabu hicho ametoa mfano wa mwenye kusema:

'Nikifanya jambo fulani basi mimi ni Myahudi' akifanya jambo hilo itabidi atoe kafara kwa kuchukulia kuwa ni kama aliyeapa kwa kusema: 'Wallahi nikifanya jambo fulani basi mimi ni Myahudi.'

Kila mwenye kujasiri kutoa fatwa na kubainisha halali na haramu na yeye si kufu wa kufanya hivyo, basi atakuwa amesema uongo na kumzulia Mwenyezi Mungu na Mtume wake na atakuwa ni katika wale waliokusudiwa na ile Aya isemayo:

تَاللَّـهِ لَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنتُمْ تَفْتَرُونَ ﴿٥٦﴾

"Wallahi! Hakika mtaulizwa hayo mliyokuwa mkiyazua" Juz; 14 (16:56)

Na kauli ya Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)**: "Mwenye kunisemea uongo kwa makusudi basi na ajichagulie makazi yake motoni" Kumsemea uongo Mwenyezi Mungu na Mtume ni kutoa riwaya kutokana nao au kunasibisha halali na haramu kwao.

Siku hizi mamufti wazushi wamekuwa wengi walioifanya dini kuwa ni njia ya kutafutia riziki na pazia ya kuwa wahaini na vibaraka. Wengine wameanzisha vyama vya kutumikia uzayuni na ukoloni, lakini vina majina ya kiislamu na waislamu ili kuwahadaa na kuwapoteza watu.

Sheikh mmoja aliniuliza kuhusu wake wa Habil na Qabil kuwa je, hao ni katika hurilaini wa peponi au sio? Nikamjibu kuwa masuala haya yanajulikana kwa kunakili sio kwa kiakili, na nukuu yake haitumiwi isipokuwa ikiwa ni ya Qur'an au Hadith mutawatir wala hakuna nukuu yoyote ya hilo. Kwa hiyo inatupasa tunyamaze yale aliyoyanyamazia Mwenyezi Mungu.

Akasema: Itakuwaje? Je, tuseme tumeshindwa tutakapoulizwa? Nikamwambia: Je, tunatakikana tujue kila kitu kwa vile sisi tuna vilemba vya ushekhe?

Wala usitembee katika Ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.

Mjinga anaweza kuwa na kiburi na kujifanya mkubwa anapomiliki ghururi za dunia; kama vile jaha na mali. Lakini likimtokea jambo la ghafla katika mambo yaliyojificha, basi anakuwa mnyonge na kudangana hana la kufanya. Mwenye akili ni yule anayejijua, akafikiri na kuzingatia.

Kauli yake Mwenyezi Mungu 'Wala usitembee katika Ardhi kwa maringo' ni kukataza kiburi na kuamrisha kunyenyekea. Kauli yake: 'Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima' ni fumbo la kushindwa mtu na kwamba yeye ni mdhaifu wa kufikia anayoyataka; kama alivyo mdhaifu wa mwili wake kuweza kufikilia jabali kwa urefu na kuweza kuipasua ardhi kwa wayo wake.

Hayo yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako.

Hayo ni kuishiria yaliyotangulia kutajwa katika yale aliyoyaamrisha Mwenyezi Mungu na kuyakataza. Makusudio ya ubaya wake ni yale aliyoyakataza hasa. Maana ni kuwa vitu vyote hivi ambavyo amevikataza Mwenyezi Mungu anavichukia, na mwenye kuvifanya ni mwenye kughadhibikiwa na Mwenyezi Mungu na mwenye kustahili adhabu.

Hayo ni katika hekima alizokupa wahyi Mola wako.

Hayo ni ishara ya maamrisho na makatazo yaliyotanglia kutajwa. Hekima ni kukiweka kitu mahali pake; Hakuna mwenye shaka kwamba hukumu zake zote Mwenyezi Mungu ziko mahali pake. Na kwamba mwenye kuichukua atakuwa ameichukua kwa haki, heri na uadilifu.

Usimfanye mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, usije ukalaumiwa uliyetupwa.

Imetangulia Aya hii pamoja na tafsiri yake katika Sura hii Aya 22. Mwenyezi Mungu ameanzia na kukataza shirki na akamalizia nako, kwa sababu tawhid ndio kianzio na lengo la Uislamu, dini ya Mwenyezi Mungu iliyo ya haki. Kwa kuwa hukumu zote zinatoka kwake, basi hakuna halali ila aliyoiamrisha wala haramu ila aliyoiharamisha.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

أَفَأَصْفَاكُمْ رَبُّكُم بِالْبَنِينَ وَاتَّخَذَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِنَاثًا ۚ إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

40. Je, mola wenu amewachagulia waototo wa kiume na yeye akajichukulia watoto wa kike katika Malaika? Hakika nyinyi mnasema kauli kubwa.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَٰذَا الْقُرْآنِ لِيَذَّكَّرُوا وَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا نُفُورًا ﴿٤١﴾

41. Hakika tumekwishabainisha katika Qur'an ili wapate kukumbuka, lakini haiwazidishii isipokuwa kuwa mbali.

قُل لَّوْ كَانَ مَعَهُ آلِهَةٌ كَمَا يَقُولُونَ إِذًا لَّابْتَغَوْا إِلَىٰ ذِي الْعَرْشِ سَبِيلًا ﴿٤٢﴾

42. Sema lau kama wangelikuwa pamoja naye miungu mingine, kama wasemavyo, basi wangelitafuta njia ya kumfikia Mwenye Arshi.

سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَقُولُونَ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤٣﴾

43. Ametakasika na ametukuka juu kabisa na hayo wanayoyasema.

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَاوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَن فِيهِنَّ ۚ وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَٰكِن لَّا
تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤٤﴾

44. Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na hapana kila kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake, lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole Mwenye maghufira.

## JE, MOLA WENU AMEWACHAGULIA WAVULANA?

**Aya 40 – 44**

### MAANA

Je, mola wenu amewachagulia waototo wa kiume na yeye akajichukulia watoto wa kike katika Malaika?

Qur'an inazingatiwa kuwa ni hoja isiyokuwa na ubishi, katika yote iliyoyasema na kuyasajili; Aya hii inaelezea vile washirikina walivyokuwa wakiitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ana mabinti katika aina ya malaika. Vile vile walikuwa wakiitakidi kwamba mtoto wa kiume ni bora kuliko wa kike; kama alivyosema Mwenyezi Mungu: "Na mmoja wao akibashiriwa msichana uso wake unasawijika naye amejaa chuki." Juz; 14 (16:58).

Kwa hiyo basi wao walijinasibishia ubora na uduni wakamnasibishia Mungu. Ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) akawatahayariza na ujinga huu, akawaambia:

Hakika nyinyi mnasema kauli kubwa, kwa sababu Yeye Mwenyezi Mungu hana mshirika wala aliyeshabihiana naye. Lau angelikuwa na mtoto angelikuwa huyo mtoto wake atamrithi na kushabihiana naye, lau angelikuwa na mzazi angelikuwa mzazi wake ni mshirika wake kwenye utukufu na enzi, bali huyo mzazi angelikuwa ni mtukufu zaidi yake, kwa sababu yeye ndiyo sababu ya kupatikana kwake.

Pengine mantiki ya wajahili ni kwamba siri iliyowafanya wamnasibishie Mungu mabinti na wao watoto wa kiume, ni kuwa Mwenyezi Mungu

hahofii ufukara kwa sababu ya kuwa na watoto wengi wala aibu ya kuwa na mabinti.

Hakika tumekwishabainisha katika Qur'an ili wapate kukumbuka, lakini haiwazidishii isipokuwa kuwa mbali.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameweka dalili na hoja za kupatikana kwake na umoja wake na akazifafanua kwa kupiga mifano na mifumo mbalimbali ili wafahamu na waelewe, lakini wao wameng'ang'ania njozi na kuiga. Wakazidi inadi na kuwa mbali.

Razi anasema: "Hakika Mwenyezi Mungu amekithirisha kutaja dalili katika Qur'an; kwa sababu Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka washirikina wazifahamu na kuziamini; Hii inafahamisha kwamba Yeye, aliyetukuka, anafanya vitendo vyake kwa hekima na inafahamisha kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka imani kwa kila mmoja ni sawa aamini au asiamini."

Kauli hii ya Razi inapingana na aliyoyaelezea mara kwa mara kwamba vitendo vya Mwenyezi Mungu havina sababu ya malengo, na kwamba Yeye ndiye aliyetaka kafiri awe kafiri; kama ilivyo kwa madhehebu ya Ashaira. Lakini Mwenyezi Mungu anataka kuinusuru haki na kuidhihirisha hata kwenye ulimi wa yule anayeipinga bila ya kujitambua.

Sema lau kama wangelikuwa pamoja naye miungu mingine, kama wasemavyo, basi wangelitafuta njia ya kumfikia Mwenye Arshi.

Watu wa tafsiri wametaja maana mbili za Aya hizi:

Kwanza: Ikisemwa kuwa kuna miungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu basi msiwahesabu hao waungu kuwa ni nyota, binadadamu, mawe au vitu vingine. Kwa sababu hivi vyote vimeumbwa na Mwenyezi Mungu, vinamwabudu na kujikurubisha kwake.

Basi mambo yakiwa hivi ni juu yenu enyi washirikiakina kumwabudu Mwenyezi Mungu; kama ambavyo vile manvyoviabudu vinamwabudu Yeye tu.

Maana au tafsiri ya pili ambayo ina nguvu zaidi ni: Lau kungelikuwa na waungu wengine, basi wangelipingana na Mwenyezi Mungu na wangelitafuta nji ya kufikia kwenye madaraka. Hakuna mwenye shaka kwamba kupingana na kuzozana viongozi kunaleta vurugu na ghasia; kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

لَوْ كَانَ فِيهِمَا آلِهَةٌ إِلَّا اللَّـهُ لَفَسَدَتَا فَسُبْحَانَ اللَّـهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٢٢﴾

"Lau wangelikuwemo humo miungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka hizo mbingu na ardhi zingelifisidika," (21:22).

Tumefafanua hayo katika kufasiri, Juz; 5 (5:48).

Ametakasika na ametukuka juu kabisa na hayo wanayoyasema.

Amejivua Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kauli ya madhalimu na washirikina kwamba Yeye ana washirika na watoto.

### KILA KITU KINAMTAKASA (KINAMSABBIH)

Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na hapana kila kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake.

Ndio! Kila kitu kinamtaksa na kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu, hilo halina shaka. Tasbih au utakasho wa kitu unatofautiana na kitu kingine kulingana na kilivyo hicho kitu.

Mwenye akili anamtakasa na kumsifu Mwenyezi Mungu kwa ulimi wake, vitu vingine vinamtakasa kwa lugha ya hali. Kwa maneno mengine vinamtakasa na kumsifu kwa jinsi vilivyopatikana umbile lake na mpangilio wake, kuwa yuko mpangiliaji mzuri aliyevifanya viwe hivyo vilivyo; sawa na unavyojulisha mchoro mzuri kuwa mchoraji ni hodari aliye bingwa.

Lugha ya hali ina nguvu na ni fasaha zaidi kuliko lugha ya maneno. Kwa sababu ya maneno inahitajia dalili, lakini ya hali hiyo yenyewe ni dalili inayopeleka kwenye elimu na yakini; Yamekwisha tangulia maelezo ya hayo katika kufasiri Juz; 13 (13:15).

Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake; Hakika Yeye ni Mpole Mwenye maghufira.

Hawawezi kufahamu walahidi na washirikina tasbihi zao, kwa sababu ya kujiweka mbali kwao na utukufu wa Mwenyezi Mungu katika kuumba kwake au kwa sababu ya kuzembea kuchunguza na kutambua siri na maajabu ya ulimwengu.

Anasema Ibn Arabi katika kitabu Alfutuhatil-makkiyya Juz; 4: “Mwenyezi Mungu ana ishara aina kwa aina: Kuna zile zinazotambulika kwa kutumia akili, zinazotambulika kwa usikizi na zile zinazotambulika kwa kuona. Kwa hiyo ni juu ya kila mtu kutumia vyombo hivi kuweza kujua ishara za Mwenyezi Mungu ambazo amezitaja katika kitabu chake. Akishajua na kuamini kwazo na akatenda kwa mujibu wake basi atakuwa ni miongoni mwa watu wa Qur’an na watu mahususi wa Mwenyezi Mungu.”

Kisha akaendelea kusema Ibn Arabi: “Chukua kupatikana kote kuwa ni Kitabu kinachotamka haki” Hii ni kama kauli ya mmoja wa wataalamu wa elimu ya Mwenyezi Mungu: “Hakika Mwenyezi Mungu ana vitabu viwili: kimoja kinatamka kwa lugha ya makala, hicho ni Qur’an na kingine kinatamka kwa lugha ya hali nacho ni ulimwengu.”

وَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ حِجَابًا مَّسْتُورًا ﴿٤٥﴾

45. Na unaposoma Qur’an tunaweka baina yako na ya wale wasioamini Akhera pazia linalowafunika.

وَجَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا وَإِذَا ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِي الْقُرْآنِ وَحْدَهُ وَلَّوْا عَلَىٰ أَدْبَارِهِمْ نُفُورًا ﴿٤٦﴾

46. Na tunaweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu na tunaweka kwenye masikio yao uziwi, Na unapomtaja Mola wako peke yake katika Qur’an, basi wao hugeuka nyuma wakaenda zao.

نَّحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَسْتَمِعُونَ بِهِ إِذْ يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ وَإِذْ هُمْ نَجْوَىٰ إِذْ يَقُولُ الظَّالِمُونَ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٤٧﴾

47. Sisi tunajua vyema kabisa sababu wanayosikilizia wanapokusikiliza, na wanaponon’gona, wanaposema hao madhalimu: nyinyi hamfuati isipokuwa mtu aliyerogwa.

انظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٤٨﴾

48. Tazama vipi wanavyokupigia mfano, Basi wamepotea, kwa hiyo hawawezi kuipata njia.

## UNAPOSOMA QUR'AN

**Aya 45 – 48**

### MAANA

Na unaposoma Qur'an tunaweka baina yako na ya wale wasioamini Akhera pazia linalowafunika.

Kuna kauli nyingi katika kufasir Aya hii; Yenye nguvu zaidi ni ile isemayo kuwa jamaa katika washirikina walikuwa – Muhammad anaposoma Qur'an – wanajaribu kumzuia kwa kumuudhi, ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamwambia endelea kusoma Qur'an na kutoa mwito wa Mwenyezi Mungu wala usichoke.

Na tunaweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu na tunaweka kwenye masikio yao uziwi.

Hili ni fumbo la inadi ya washirikina. Ama kunasibisha vifuniko na uziwi kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t), tumekuzungumzia kwa ufafanuzi katika kufasiri Juz; 7 (6:25). Hiyo ni mfano wa Aya hii kinukuu na kimaana.

Na unapomtaja Mola wako peke yake katika Qur'an, basi wao hugeuka nyuma wakaenda zao.

Walikuwa washirikina, inaposomwa Qur'an, wanapomsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Lailaha illallah (hapana Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu) basi wanaachana naye na kwenda zao huku wakisema:

أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَـٰهًا وَاحِدًا إِنَّ هَـٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ ﴿٥﴾ وَانطَلَقَ الْمَلَأُ مِنْهُمْ أَنِ امْشُوا وَاصْبِرُوا عَلَىٰ آلِهَتِكُمْ ﴿٦﴾

"Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu. Na wakaondoka wakubwa wao wakiwaambia: Nenedeni zenu na dumuni na miungu yenu." (38: 5-6).

Sio siri kuwa upinzani huu ni kwa vile tu tamko la tawhid linakusanya msingi wa kusema: "Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu ni yule mwenye takua zaidi" (49: 13). Sio utabaka na ubaguzi.

Sisi tunajua vyema kabisa sababu wanayosikilizia wanapokusikiliza, na wanaponon'gona, wanaposema hao madhalimu: Nyinyi hamfuati isipokuwa mtu aliyerogwa.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kusema: 'na tunaweka kwenye masikio yao uziwi' sasa anasema: Sisi tunajua vizuri kwamba wewe wakati unaposoma Qur'an washirikina hawakusikilizi kwa moyo safi, bali wanakusikiliza kwa kwa roho ya chuki, inadi na kiburi, kisha wanaambiana na pia kuwaambia wengine, kuwa Muhammad ni mchawi ameingiwa na jini linalozungumza hekima na ufasaha huu kwenye ulimi wake; itakuwaje azungumze hivi naye hajui kusoma wala kuandika, tena hana hazina ya dhahabu au fedha wala hana shamba la mitende na mizabibu.

Hii ndio fikra yao ya kitabaka, kwamba mwenye mali tu ndio anayeweza kuwa na cheo kitukufu kiwe cha dini au cha kawaida: "Na walisema: kwa nini hii Qur'an haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii" (43:31) Ama akili, ukweli na uaminfu kwao hauna maana.

Tazama vipi wanavyokupigia mfano.

Walizidi mno kwa Muhammad **(s.a.w.w)** kwa vile kuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kutamka maneno ya Mwenyezi Mungu; mara

wakamwita mwendawazimu, mara mchawi, mara kuhani na mara nyingine wakamwita mshairi.

Muhammad ambaye ametumwa kukamilisha tabia njema, amekuwa mchawi na mwendawazimu? Kwa nini amekuwa hivyo? Kwa vile yeye anatamka haki na kuitolea mwito na wala hakukubaliana na matamanio ya wabatilifu na wafisadi. Zaidi ya hayo hana farasi wala mali.

Kwa ufupi ni kwamba watu wa matamanio na matakwa, hisia zao ziko upande mmoja tu, matamanio na masilahi yao binafsi. Hawasikii wala hawaoni isipokuwa kwayo tu; kiasi cha kuhalalisha yote kwenye hawa zao na matamanio. Kwa hali hii ndio tunapata tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu: "Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho yao pana kifuniko" Juz, 1 (2:7) na tafsiri ya kila Aya iliyo na maana haya katika maneno ya Mtukufu Aliyetukuka.

Basi wamepotea, kwa hiyo hawawezi kuipata njia, ya kuwakadhibisha wenye haki, isipokuwa uzushi, upotevu, ulaghaii, uadui, njama na rushwa.

وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا عِظَامًا وَرُفَاتًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٤٩﴾

49. Na wakasema: je, tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagika, je tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

قُلْ كُونُوا حِجَارَةً أَوْ حَدِيدًا ﴿٥٠﴾

50. Sema: kuweni hata mawe au chuma.

أَوْ خَلْقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ فَسَيَقُولُونَ مَن يُعِيدُنَا قُلِ الَّذِي فَطَرَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ قُلْ عَسَىٰ أَن يَكُونَ قَرِيبًا ﴿٥١﴾

51. Au umbo lolote mnaloliona kubwa katika vifua vyenu, Watasema: Ni nani atakayeturudisha tena? Sema: Ni huyo aliyewaumba mara ya kwanza. Watakutikisia vichwa vyao Na watasema: lini hayo? Sema: asaa yakawa karibu.

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِثْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾

52. Siku atakayowaita nanyi mkamwitikia kwa kumsifu. Na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mchache tu.

## TUTAKAPOKUWA MIFUPA NA MAPANDE YALIYOSAGIKA

**Aya 49 – 52**

### MAANA

Na wakasema: je, tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagika, je tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

Hii ndio hoja ya mwenye kutilia shaka ufufuo, tangu zamani hadi sasa, kuwa itakuwaje mtu arudi kuwa hai baada ya kuwa vumbi linalotifuka?

**Jibu**: Yule aliyeweza kuumba kitu na kukifanya kiwepo baada ya kuwa hakipo, basi ni wazi kuwa anaweza kukikusanya baada ya kutawanyika. Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameitaja shaka hii na jawabu lake kwenye Aya kadhaa; miongoni mwazo ni ile iliyo katika sura Yasin:

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَن يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا

أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

“Akasema: ni nani huyo atakayeihuisha mifupa nayo imekwisha mung’unyika? Sema: atahiuisha huyohuyo aliyeiumba mara ya kwanza na Yeye ni mjuzi wa kila kuumba” (36: 78 – 79).

Tumelifafanua suala hili katika Juz; 13 (13:5).

Sema: kuweni hata mawe na chuma au umbo lolote mnaloliona kubwa katika vifua vyenu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawaambia wale wanaokanusha ufufuo kuwa hata kama mtakuwa mawe au chuma au kitu kikubwa zaidi ya hivyo tutawaumba tu kuwa watu hai.

Anayeweza kuumba kutokana na chuma au jiwe au kitu kigumu zaidi ya hivyo, basi ni muweza zaidi wa kumrudishia uhai yule aliyempa uhai mwanzo. Kwa sababu kuvikusanya vitu baada ya kutawanyika ni rahisi zaidi kuliko kuvianzisha upya.

Kwa ufupi ni kuwa kumfufua mtu baada ya kufa ni wepesi zaidi kuliko kukifanya chuma kuwa mtu, Anayeweza hivi basi hashindwi kufanya vile.

Watasema: Ni nani atakayeturudisha tena kwenye uhaai baada ya kuwa mavumbi yanayopeperuka. Jibu la swali hili ni:

Sema: Ni huyo aliyewaumba mara ya kwanza.

Mwenye kurudisha ndiye yule aliyeanza; Kuanza na kurudisha ni kumoja tu; bali kurudisha ni wepesi zaidi, kwa sababu ni kurudisha ilivyokuwa. Tunasema hivi, kama mfano tu, tukijua kuwa Mwenyezi Mungu anaumba vichache na vingi na pia vidogo na vikubwa kwa neno.

كُن فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

“Kuwa! Na kikawa” (36:82).

Watakutikisia vichwa vyao kwa stihzai na kukadhibisha Na watasema: lini hayo? Makusudio ya swali hili ni kuona kuwa haiwezekani.

Sema: asaa yakawa karibu. Makusudio ya karibu hapa ni kuhakikika na kutokea, kwani ‘Kila lijalo liko karibu.’

Siku atakyowaita nanyi mkamwitikia kwa kumsifu.

Makusudio ya Siku ni siku ya Ufufuo, kuitwa ni kupuziwa parapanda, kuitikia ni fumbo la kutoka kwao makaburini na kumsifu ni kutii na kufuata:

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَإِذَا هُم مِّنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنسِلُونَ ﴿٥١﴾

“Na itapulizwa parapanda mara watatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola wao” (36:51).

Na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mchache tu.

Watu watakapotoka makaburini watadhani kuwa wao hawakukaa duniani isipokuwa siku moja au sehemu ya siku:

قَالَ كَمْ لَبِثْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿١١٢﴾ قَالُوا لَبِثْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَاسْأَلِ الْعَادِّينَ ﴿١١٣﴾

“Atasema: mlikaa muda gani katika ardhi kwa hisabu ya miaka? Watasema tulikaa siku moja au sehemu ya siku,” (23:112- 113).

7

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَقُل لِّعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ الشَّيْطَانَ يَنزَغُ بَيْنَهُمْ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلْإِنسَانِ عَدُوًّا
مُّبِينًا ﴿٥٣﴾

53. Waambie waja wangu waseme maneno mazuri. Kwani shetani huchochea baina yao. Hakika shetani ni adui aliye dhahiri kwa mtu.

رَّبُّكُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ إِن يَشَأْ يَرْحَمْكُمْ أَوْ إِن يَشَأْ يُعَذِّبْكُمْ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿٥٤﴾

54. Mola wenu anawajua vilivyo, akipenda atawarehemu na akipenda atawaadhibu. Na hatukukutuma ili uwe mlinzi juu yao.

وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِمَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَىٰ بَعْضٍ وَآتَيْنَا دَاوُودَ
زَبُورًا ﴿٥٥﴾

55. Na Mola wako anawajua vilivyo waliomo mbinguni na waliomo ardhini. Na hakika tumewafadhilisha baadhi ya manabii kuliko wengine; na Daud tulimpa Zaburi.

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُم مِّن دُونِهِ فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنكُمْ وَلَا تَحْوِيلًا ﴿٥٦﴾

56. Sema: Waombeni hao mnaodai badala Yake; hawawezi kuwaondolea madhara wala kuyabadilisha.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ
إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ﴿٥٧﴾

57. Hao wanawaomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kujikurubisha kwa Mola wao, hata walio karibu miongoni mwao, na wanataraji rehema zake na wanaihofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuhofiwa.

## WAAMBIE WAJA WANGU WASEME MANENO MAZURI

**Aya 53 – 57**

### MAANA

Waambie waja wangu waseme maneno mazuri.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Mtume wake mtukufu awaamrishe waumini au watu wote waseme maneno mazuri, watamke haki na uadilifu kwa thamani yoyote itakayokuwa, Angali Juz; 13 (14: 24–26).

Kwani shetani huchochea baina yao.

Shetani hutafuta makosa ya ulimi ili ayafanye ni kuni za moto wa uadui na chuki baina ya watu. Makosa ya ulimi hayawi tu kwa kutukana bali pia kwa kusifu pasipokuwa mahali pake na kwenye matamshi ya ufuska na uovu.

Hakika shetani ni adui aliye dhahiri kwa mtu.

Uadui huu aliubainisha wazi pale aliposema:

قَالَ فَبِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٦﴾ ثُمَّ لَآتِيَنَّهُم مِّن بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِ نْ
خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَن شَمَائِلِهِمْ ﴿١٧﴾

"Kwa kuwa umenipoteza, basi hakika nitawakalia katika njia yako iliyonyooka; kisha hakika nitawaendea kwa mbele yao na nyuma yao na kuumeni kwao na kushotoni kwao" Juz; 8 (7:16-17).

Mola wenu anawajua vilivyo, akipenda atawarehemu na akipenda atawaadhibu.

Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwadilifu na Mwenye hekima. Anajua hali za waja wake, yale yaliyo na masilahi nao na yale yenye ufisadi na anawachukulia kwa uadilifu wake na hekima yake.

Atamrehemu anayestahiki rehema naye ni yule anayefuata amri na mtiifu; Na atamwadhibu anayestahiki adhabu; naye ni yule muasi jeuri. Hiyo ni baada ya kuwawekea hoja kwa kuwafikishia yaliyo halali na yaliyo haramu kupitia kwa Mtume mtukufu.

Na hatukukutuma ili uwe mlinzi juu yao, bali ni mfikishaji:

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٤٠﴾

"Basi ni juu yako kufikisha na juu yetu hisabu," Juz.13: (13:40).

Na Mola wako anawajua vilivyo waliomo mbinguni na waliomo ardhini. Na hakika tumewafadhilisha baadhi ya manabii kuliko wengine; na Daud tulimpa Zaburi.

Mwenyezi Mungu anawajua watu wa mbinguni na wa ardhini na anajua uwezo wa kila mmoja wao. Kwa misingi hiyo ndio huwachagua wajumbe kwenda kwa mitume wake; kama vile Jibril (a.s). Na hupeleka mitume wabashiri na waonyaji kwa watu.

Kama alivyowafadhilisha baadhi ya Malaika kuliko wengine; vilevile Mitume, baadhi amaewafadhilisha kuliko wengine.

**Unaweza kuuliza kuwa**: Uislamu unasimama kwenye misingi ya usawa ;sasa kuna maana gani ya ubora huu kwa baadhi kuliko wengine? Kisha ubora huu utapatikana vipi kwa Malika na Mitume na hali tunajua kuwa wote ni waja wa Mwenyezi Mungu wenye kutukuzwa, hawamtangulii kwa jambo lolote na wanafanya kulingana na amri yake?

**Jibu**: Ndio ni kweli kuwa hakuna tofauti kwa msingi wa utiifu, isma, na utawala kama ulivyo; isipokuwa kwa upande wa sifa; kama vile dhahabu tunajua kuwa yote ina thamani, lakini kuna baadhi inathamani zaidi kuliko nyingine. Vile vile vitu vingine vizuri vinatofautiana kulingana na uzuri wake na daraja yake, sio katika kuwa kwake na hakika yake. Ndio maana ikasemwa: 'Nuru juu ya nuru' au 'kheri juu ya kheri'

**Swali la pili**: imekuwaje Mwenyezi Mungu kumtaja Daud peke yake kuwa amempa Zaburi na tunajua kuwa Musa alimpa Tawrat, Isa Injil na Muhammad akampa Qur'an?

Amemtaja peke yake kuwarudi washirikina waliosema: vipi Muhammad atakuwa ni mtume na yeye ni yatima fukara. Njia ya kuwarudi ni kuwa Yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaujalia ujumbe wake kwa yule anayestahiki - awe yatima aliyefukara, kama Muhammad au tajiri, kama Daud. Katika vitabu vingi vya sera na tarikh, hutajwa Mfalme Daud.

Sema: Waombeni hao mnaodai badala Yake, hawawezi kuwaondolea madhara wala kuyabadilisha.

Wafasiri wengi wamesema kuwa Aya hii na inayofuatia zilishuka kwa ajili ya wale wanaoabudu malaika, Isa na Uzayr. Na kwamba wanokusudiwa hapa sio waabudu masanamu, kwa sababu Mwenyezi Mungu amewataja hao waabudiwa kwa kusema: 'wao wenyewe wanatafuta njia ya kujikuru- bisha kwa Mola wao,' na kutafuta nji hakuelekeani na masanamu.

Kwa hiyo maana ni kuwa ewe Muhammad! Waambie wale wanaoabudu Malaika, Isa na Uzayr: yakiwapata madhara, kama ufukara na maradhi, basi waaombeni wale manowaabudu wawaondolee, kisha muangalie, je wanaweza kuwakinga au kuwabadilishia? Hakuna mwenye shaka ya kushindwa kwao, kwa vile wao wenyewe hawawezi kujikinga itakuwaje kwa mwengine?

Hao wanawaomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kujikurubisha kwa Mola wao.

Yaani hao ambao mnawaabudu enyi washirikina wanatafuta kujikurukubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa twaa, hawajitii kiburi kwa waja wengine, wanamtakasa na kumsujudia Mungu, sasa vipi nyinyi mnawaabudu.

Hata walio karibu miongoni mwao, na wanataraji rehema zake na wanaihofu adhabu yake.

Yaani kila mmoja kati ya Malaika, Isa na Uzayr anajitahidi, kumwabudu Mwenyezi Mungu na kumfanyia ikhlasi ili awe karibu na msamaha wake na rehema zake na awe mbali na machukivu yake.

Hiyo ni kwa vile Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuhofiwa.

Wanaihofia manabii na mawalii, je, wengine? Kila mwenye akili ni lazima ahofie mwisho na kuuandalia maandalizi, kwa hali yoyote atakavyokuwa na cheo na daraja; hasa ikiwa mwenye kuchukua hisabau anajua siri na yaliyofichikana.

وَإِن مِّن قَرْيَةٍ إِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ أَوْ مُعَذِّبُوهَا عَذَابًا شَدِيدًا كَانَ ذَٰلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ﴿٥٨﴾

58. Hapana mji wowote ila Sisi tutauangamiza kabla ya Siku ya Kiyama au kuupa adhabu kali, Haya yamekwishaandikwa kwenye Kitabu.

وَمَا مَنَعَنَا أَن نُّرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَن كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ وَآتَيْنَا ثَمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا وَمَا نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا ﴿٥٩﴾

59. Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na wathamudi tuliwapa ngamia jike kuwa ni dalili inayoonekana, lakini wakamdhulumu. Nasi hatupeleki ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha.

وَإِذْ قُلْنَا لَكَ إِنَّ رَبَّكَ أَحَاطَ بِالنَّاسِ وَمَا جَعَلْنَا الرُّؤْيَا الَّتِي أَرَيْنَاكَ إِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ وَنُخَوِّفُهُمْ فَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٦٠﴾

60. Na tulipokwambia: hakika Mola wako amekwishawazunguka hao watu. Na hatukuifanya ndoto tuliyokuonyesha ila ni fitna (majaribu) kwa watu na mti uliolaaniwa katika Qur'an. Na tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa.

## MJI WOWOTE

**Aya 58 – 60**

### MAANA

### Mahdiy Anayengojewa

Hapana mji wowote ila Sisi tutauangamiza kabla ya siku ya Kiyama au kuupa adhabu kali, Haya yamekwishaandikwa kwenye Kitabu.

Dhahir ya Aya inafahamisha kuwa watu wote watatoweka kabla ya siku ya kiyama, ambapo itafika siku kwenye ardhi kutakuwa hakuna yoyote kabisa; na kwamba jambo hili limekwishaandikwa katika kadha na kadari ambayo haiepukiki. Kuna jamii itatoweka kwa mauti ya kawaida na nyingine kwa adhabu kali, lakini Mwenyezi Mungu hakubainisha wasifa wa hawa wala wale.

Hiyo ndiyo dhahir ya Aya, lakini wafasiri wamesema kuwa jamii njema itatoweka kwa mauti ya kawaida na jamii ya ufisadi itatoweka kwa adhabu kali. Lakini haya hayaafikianai na kauli yao katika kufasiri Aya za mwanzo za sura Hajj:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ  إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ﴿١﴾ يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَارَىٰ وَمَا هُم بِسُكَارَىٰ وَلَـٰكِنَّ عَذَابَ اللَّـهِ شَدِيدٌ ﴿٢﴾

"Enyi watu! Mcheni Mola wenu, Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu. Siku mtakapoiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshae na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake na utawaona watu wamelewa kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali," (22:1-2).

Tuonavyo sisi mji alioukusudia katika kauli yake hii ni mji ambao watu wake ni madhalimu; yaani jamii yenye ufisadi tu; na kwamba Yeye ataiangamiza jamii hii au ataiadhibu kabla ya Siku ya Kiyama, wala hawatabakia ispokua watu wema tu, wote wakiwa wanaishi kwenye twaa ya Mwenyezi Mungu wakiwa na amani ya nafsi zao na vitu vyao vyote.

Kuna Hadith nyingi zinazozungumzia suala hilo; miongoni mwazo ni hizi:-

Hadith iliyoko kwenye Sunan Abi Daud As-sasjsataniy, kikiwa ni mojawapo ya Sahih sita kwa masunni, Juzuu ya pili chapa ya mwaka 1952, uk. 422:

"Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: Lau haitabaki isipokuwa siku moja ya dunia, basi Mwenyezi Mungu atairefusha siku hiyo mpaka amlete mtu kutokana na watu wa nyumba yangu (Ahli bayti), Jina lake linafanana na jina langu na jina la baba yake ndio jina la baba yangu, ataijaza ardhi usawa na uadilifu; kama ilivyojazwa dhulma baada kujazwa usawa na uadilifu."

Hadith iliyoko katika Sunan Ibn Maja, Pia nayo ni miongoni mwa sahih sita, juzuu ya pili chapa ya mwaka 1952, Hadith namba: 4083: Amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu: "Atakuwa katika umma wangu Mahdi, utaneemeka uma wangu neema ambayo haujaneemeka mfano wake."

Mapinduzi na kujitoa mhanga kwa kujilipua (intifada), kila mahali kwa ajili ya kujikomboa na dhulma, ufisadi, ujinga na umasikini, yana fahamisha waziwazi kuwa hilo litakuwa tu karibuni au baadaye.

Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na wathamudi tuliwapa ngamia jike kuwa ni dalili inayoonekana, lakini wakamdhulumu.

Washirikina walipendekeza kwa Mtume awaletee muujiza wanaoutaka wao. Miongoni mwa waliyoyasema ni: Tuchimbulie chemchem kutoka ardhini, tuletee Mungu na Malaika, tuletee kitabu kutoka mbinguni tukisome na mengineyo.

Ndio Mwenyezi Mungu akawajibu katika Aya hii, kwamba yeye amekwishapitisha katika kadha na kadari yake, kuwang'owa kwa adhabu kila kaumu iliyokadhibisha miujiza iliyokuja kwa maombi yao.

Wathamudi walimwomba Mtume wao awapatie ngamia wa muujiza. Alipowajia na sifa zile walizozitaka, walimkanusha na wakamchinja. Ukawanyakua ukelele wakawa ni wenye kuangamia; Yametangulia maelezo ya ngamia katika Juz; 8 (7:73 –79).

Imekwishapitisha kadari yake kutowang'oa Makuraishi, kutokana na mapendekezo waliyoyapendekeza kwa Mtume. Kwa sababu watapatikana watu watakaotubia na kuamini, watazaliwa wengine wapigania jihadi kwa Mwenyezi Mungu. zaidi ya hayo kadari ya Mwenyezi Mungu imepitisha kuwa uma wa Muhammad na sharia yake ubakie mpaka siku ya ufufuo. Kwa sababu hii na nyinginezo, Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuitikia maombi ya makuraishi.

Nasi hatupeleki ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha.

Hakuna ishara yoyote inayodhihiri mikononi mwa Mtume ila ina malengo; yakiwemo: mawaidha, makaripio na kuhadharisha adhabu isiyokuwa na kinga wala kafara; sasa vipi wao wanaharakia kutoa maombi ya adhabu?

Na tulipokwambia: hakika Mola wako amekwishawazunguka hao watu.

Imeelezwa hapo juu kuwa makuraishi walimtaka Mtume awalete muujiza na kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimpa wahyi Mtume wake kuwa lau atawaitikia maombi yao na wakaasi, wataangamia.

Lakini jawabu hili halikuwakinaisha washirikina na wakamwambia kuwa lau ungelikuwa ni Mtume ungelituletea yale tunayotaka, ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia mtume wake kuwa wewe endelea tu, wala usiwajali wale wanaofanya inadi na kiburi. Sisi tunawajua zaidi watu na wanayoyafanya na tumewadhibiti.

Katika maana ya Aya hii ni ile isemayo:

وَاللَّـهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ﴿٦٧﴾

"Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu," Juz. 6 (5:67).

Na hatukuifanya ndoto tuliyokuonyesha ila ni fitna (majaribu) kwa watu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema kuwa alimuonyesha Mtume wake ndoto usingizini na kwamba ndoto yenyewe ni fitna, lakini hakubainisha ilikuwa ya aina gani wala makusudio ya hiyo fitna au majaribu.

Ndio maana wafasiri wakatofautiana katika maana yake, Akataja Razi kati- ka Tafsiri al-kabir, Abu Hayan Al-andalusi katika Al-bahrul-muhit,

Muhammad bin Ahmad Al-kalabiy, katika Attas-hil na wengineo, wametaja kauli kadhaa katika tafsiri ya ndoto na fitna.

Miongoni mwazo ni mtume **(s.a.w.w)** aliota kuwa yeye ataingia Makka pamoja na swahaba, lakini alipotaka kuingia makuraishi walimzuia katika mwaka wa Hudaybiya.

Akaingiwa na shaka mwenye shaka miongoni mwa waislamu kuhusu ndoto ya Mtume, akamwambia: "Si umesema kuwa tutaingia Makka kwa amani?" Akasema: "Ndio, kwani nimesema tutaingia mwaka huu?" Akasema: "Hapana" Mtume **(s.a.w.w)** akasema: "Inshallah tutaingia" wakaingia mwaka uliofuatia.

Miongoni mwa kauli nyingine zinazotokana na tafsiri ni kuwa Mtume **(s.a.w.w)** aliona kwenye ndoto bani Umayya wakiiparamia mimbari yake kama anavyoparamia nyani, akahuzunika na akawa hana raha, na hakuonekana akicheka.

Kikundi miongoni mwa swahaba wako kwenye tafsiri hii; miongoni mwao ni Said bin Al-musabbib na Ibn Abbas; kama ilivyo katika Tafsiru-rrazi. Pia Sahal bin Sa'd; kama ilivyo katika Tafsir Al-bahr al-muhit.

Katika Sahih Al-bukhari Juzuu ya tisa Kitabu Al-fitan, imeelezwa kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alisema: "Kuangamia kwa umma wangu kutakua mikononi mwa wafidhuli wa kikuraishi," Riwaya hii inatia nguvu tafsiri ya ndoto kuhusu Bani Umayya.

Kwa hiyo makusudio ya Na mti uliolaaniwa katika Qur'an ni Bani Umayya. Katika Tafsiru-rrazi imeelezwa kuwa kuna kundi la wafasiri wanasema: "Mti uliolaaniwa katika Qur'an ni mayahudi." Matukio ya Historia ya kale na ya sasa yamethibitisha kuwa mayahudi ndio mzizi wa fitina.

Na tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa.

Mwenyezi Mungu amewahadharisha wanafiki kwa mifumo mbalimbali, lakini haikufaa kitu; bali hizo hadhari ziliwazidishia upotevu, kwa sababu wao hawataharaki isipokuwa kwa wahyi wa masilahi na manufaa. Ama hoja, maadili na misimamo, kwao ni maneno na njozi tu.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ قَالَ أَأَسْجُدُ لِمَنْ خَلَقْتَ طِينًا ﴿٦١﴾

61. Na tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia wote isipokuwa Iblis, alisema: Je, nimsujudie uliyemuumba kwa udongo?

قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَٰذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ لَئِنْ أَخَّرْتَنِ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَأَحْتَنِكَنَّ ذُرِّيَّتَهُ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٢﴾

62. Akasema: Unaona! Huyu ndiye uliyemtukuza zaidi kuliko mimi? Kama utaniahirisha mpaka Siku ya Kiyama, bila shaka nitakiburuza kizazi chake isipokuwa wachache tu.

قَالَ اذْهَبْ فَمَن تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاؤُكُمْ جَزَاءً مَّوْفُورًا ﴿٦٣﴾

63. Akasema: Ondoka! Atakayekufuata katika wao, basi Jahannam itakuwa ndio malipo yenu, malipo yenye kutimia.

وَاسْتَفْزِزْ مَنِ اسْتَطَعْتَ مِنْهُم بِصَوْتِكَ وَأَجْلِبْ عَلَيْهِم بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ وَشَارِكْهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ وَعِدْهُمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦٤﴾

64. Na uwachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na wendao kwa miguu na shirikiana nao katika mali na watoto na uwaahidi. Na shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu.

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٦٥﴾

65. Hakika waja wangu hutakuwa na mamlaka nao, na Mola wako anatosha kuwa ni wa kutegemewa.

## WAKASUJUDU

**Aya 61-65**

### MAANA

Na tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam, wakamsujudia wote isipokuwa Iblis, alisema: Je, nimsujudie uliyemuumba kwa udongo?

Umepita mfano wake katika Juz. 1 (2:35) na Juz, 8 (7:11).

### KUMTANGULIZA ALIYEZIDI JUU YA ALIYEZIDIWA

Akasema: Unaona! Huyu ndiye uliyemtukuza zaidi kuliko mimi?

Iblisi anahoji kwa majisifu na ufedhuli akimwambia, aliyemtukufu na kutukuka, kuwa ni nani huyo ambaye umemfadhilisha kuliko mimi? Na ni kitu gani kimemfanya awe na heshima hiyo na ukamilifu? Naona ni kinyume na hivyo:

قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِّنْهُ خَلَقْتَنِي مِن نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِن طِينٍ ﴿١٢﴾

"Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, umeniumba kwa moto naye umemuumba kwa udongo." Juz; 8 (7:12).

Habithi huyu alijitia ubora kwa kutetea mantiki yake, kuwa yeye ni bora na mkamilifu; Kwa hiyo yeye hafai kumsujudia aliyemzidi.

Ibilisi amekosea katika mantiki yake haya; Kwa sabau yeye si bora kabisa kuliko Adam, bali ni kinyume. Kwahiyo Mwenyezi Mungu

hakumtanguliza aliyezidiwa juu ya aliyezidi; kama alivyodai Ibilisi. Ni akili gani inayoruhusu kuwa Mwenyezi Mungu amkurubishe aliye baidi na ambaidishe aliye karibu? Lakini hakika hii imefichika kwa Ashaira[1] na Mu'tazila, waliposema kuwa inafaa kutangulizwa aliyezidiwa juu ya aliyemzidi. Tazama kitabu Al-mawqif Juzuu ya nane Uk. 373.

Wanasema Ashaira; Akili inakubali kuwa Mwenyezi Mungu atamwadhibu mtiifu na kumpa thawabu muasi, kwa sababu, kwa Mwenyezi Mungu hakuna uovu wala hana wajibu wowote. Tazama kitabu hicho hicho Uk. 195. Shia Imamiya wanasema akili haikubali kuwa Mwenyezi Mungu amwadhibu aliyefanya wema, lakini inakubali kuwa anaweza kuwasamehe waovu; sawa na mwenye haki yake, anaweza akasamehe yote au baadhi.

Wakaendelea kusema kuwa haikubaliki kiakili kutangulizwa aliyezidiwa juu ya aliyemzidi kwa sababu ni daraja ya juu na ya chini kulingana na utaratibu wa kimaumbile. Kumfanya aliyejuu kuwa yuko chini na aliye chini kuwa yuko juu ni kinyume na mantiki ya kiakili na kimaumbile.

Kama utaniahirisha mpaka siku ya kiyama, bila shaka nitakiburuza kizazi chake isipokuwa wachache tu.

Ibilisi anatishia kuchukua kisasi kwa kizazi cha Adamu; si kwa jambo lolote ila ni kwa sababu Mwenyezi Mungu amemtukuza Adamu. Anachukua kisasi kwa kuwaburuza kwenye maasi, kama vile anavyokokotwa mnyama; isipokuwa wachache tu ambao ni wale wenye ikhlasi.

Kisha Ibilisi anataka apewe muda katika maisha yake ili apoteze watu na afanye ufisadi; Mwenyezi Mungu akamkubalia maombi yake, akasema: ondoka! Atakayekufuata katika wao, basi Jahannam itakuwa ndio malipo yenu, malipo yenye kutimia.

Ibilisi alipotishia kuwapoteza wanadamu, Mwenyezi Mungu naye akamkemea yeye na wale atakaowapoteza na kumwambia: fanya utakavyo, atakufuata kwenye upotevu yule atakayetaka, kwani mimi si mlazimishi yeyote kwenye twaa na maasi. Wote ninawapa uwezo, akili na utashi na ninawabainishia njia ya kheri na njia ya shari. Ninakataza hili na kuamuru lile. Mwenye kufuata na akatii, basi pepo ni makazi yake na mwenye kuwa jeuri na akaasi basi jahannam ndio makazi ya waasi; watal- ipwa humo malipo wanayostahiki kwa ukamilifu bila ya upungufu.

Na uwachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na wendao kwa miguu.

Hakuna jeshi la hakika hasa la iblisi lililo na farasi au bila ya farasi; isipokuwa ni fumbo la wafisadi, yaani watu wanaofuata hawaa, wahaini na vibaraka.

Amesema Imam Ali katika Nahjul-balagha: "Tahadharini asije aka-chochea -shetani- kwa mwito wake na kuwakusanya kwenye jeshi lake la wapanda farasi na wanaokwenda kwa miguu." Sheikh Muhammad Abduh naye akaongezea kwa kusema: "Anawachochea mfanye lile alitakalo, mkichelewa atawakusanyia jeshi lake la wapanda farasi na waendao kwa miguu, yaani wasaidizi wake."

1. Madhehebu ya kiitikadi yanayofuatwa na masunni wengi. Muasisi wake ni Abul Hassan Al-ash'ariy aliyekufa mwaka 324 AH (936 AD) -Mtarjumu.

Umepita mfano wake katika Juz; 8 (7:18). Huko tumejibu maswali matatu: kuwa je, alizungumza moja kwa moja na Mwenyezi Mungu au kwa kupitia kitu kingine? Je, upotevu unatokana na Mwenyezi Mungu au na Ibilisi? Kwanini Mwenyezi Mungu akampa muda Ibilisi ili apoteze watu? Rudia huko.

Na shirikiana nao katika mali na watoto.

Kushirkiana katika mali ni fumbo la kila mali iliyopatikana kwa njia isiyokuwa ya haki; kama vile uporaji, riba, utapeli, hiyana na kuwa kibaraka. Au kuitumia isivyostahiki; kama vile kufanya israfu, kuitumia kwenye pombe, kamari na kwenye mambo ya kujionyesha. Ama kushirikiana katika watoto ni fumbo la zina, kuua watoto kwa kuhofia ufukara na aibu na kuwalea malezi ya ufisadi.

Na uwaahidi na shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu.

Ahadi ya udanganyifu ni kuivisha batili nguo ya haki na makosa kuyavika nguo ya usawa; kwa mfano shetani kumtia wasiwasi anayeamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, kuwa usihofie kumuasi Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu ni karimu Mwingi wa maghufira, na wewe bado una umri, utatubia kesho na kuomba maghufira.

Kuna baadhi ya mapokezi yanayosema kuwa Ibilisi alimtia wasiwasi mfanya ibada mmoja katika waisrail, afanye dhambi kisha atubie ili ibada yake iwe na nguvu.

Hakika waja wangu hutakuwa na mamlaka nao, na Mola wako anatosha kuwa ni wa kutegemewa.

Umepita mfano wake katika Juz. 14 (15: 42).

رَّبُّكُمُ الَّذِي يُزْجِي لَكُمُ الْفُلْكَ فِي الْبَحْرِ لِتَبْتَغُوا مِن فَضْلِهِ إِنَّهُ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾

66. Mola wenu ndiye anayewaendeshea majahazi, ili mtafute katika fadhila zake. Hakika Yeye ni Mwenye kuwarehemu.

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَن تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ فَلَمَّا نَجَّاكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ الْإِنسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾

67. Na inapowagusa dhara katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu, Anapowaokoa mkafika nchi kavu mnageuka. Na Mtu amekuwa mwingi wa kukanusha.

أَفَأَمِنتُمْ أَن يَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وَكِيلًا ﴿٦٨﴾

68. Je, mmeaminisha kuwa hataweza kuwadidimiza upande wa nchi kavu au kuwaletea tufani la kokoto, kisha msipate wa kutegemea?

أَمْ أَمِنتُمْ أَن يُعِيدَكُمْ فِيهِ تَارَةً أُخْرَىٰ فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِّنَ الرِّيحِ فَيُغْرِقَكُم بِمَا كَفَرْتُمْ ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٩﴾

69. Au mmeaminisha kuwa hatawarudisha humo mara nyingine awapelekee kimbunga cha upepo awazamishe kwa mlivyokufuru, kisha msipate wa kutufuatilia.

## ANAWAENDESHEA MAJAHAZI

**Aya 66-69**

**MAANA**

Mola wenu ndiye anayewaendeshea majahazi, ili mtafute katika fad- hila zake. Hakika Yeye ni Mwenye kuwarehemu.

Jahazi inatembea kwenye uso wa bahari kwa sababu za kimaumbile, hilo halina shaka, lakini sababu hizi zote zinaishia kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu yeye ni muumba wa ulimwengu na vilivyomo ndani yake.

Ni kwa sababu hii ndio ikafaa kutegemeza kuendesha kwake Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hekima ya hilo ni kuwa mtu daima awe katika fikra ya kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mtendaji mkuu wa vilivyomo ulimwenguni na wala sio maumbile. Ama lengo la jahazi ni kurahisisha mawasiliano.

Na inapowagusa dhara katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu, Anapowaokoa mkafika nchi kavu mnageuka, Na mtu amekuwa mwingi wa kukanusha.

Umepita mfano wake katika Juz. 11 (10:22).

Je, mmeaminisha kuwa hataweza kuwadididimiza upande wa nchi kavu au kuwaletea tufani la kokoto, kisha msipate wa kutegemea?

Watu wote wako mikononi mwa Mungu, popote pale walipo, hata wakiwa kwenye ngome zilizo na nguvu. Wakiwa baharini anaweza kuwangamiza kwa kufa maji, wakiwa nchi kavu anaweza kuwadididimiza ardhini au kunyweshewa na mvua ya mawe na wakiwa kwenye ngome imara anivunjilia mbali. Hawezi kujiaminisha ila mjinga.

Au mmeaminisha kuwa hatawarudisha humo mara nyingine awapelekee kimbunga cha upepo awazamishe kwa mlivyokufuru, kisha msipate wa kutufuatilia.

Humo ni baharini. Maana ni kuwa hakuna njia nyingine ya kuangamia isipokuwa baharini, basi Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kuwarudisha humo, awazamishe kwa kimbunga na asipatikane wa kumfuatilia Mungu kwa aliyowafanyia.

Ufupi wa Aya hizo ni kuwa mjinga humhofia Mwenyezi Mungu anapokuwa na shida, lakini shida ikimuondokea anamgeuka; pamoja na kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni muweza wa kunufaisha na kudhuru. Ama mumin mwenye akili anapata mawaidha kwa shida na raha, anahofia haya na kutaraji msaada kwa yale.

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ
مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

70. Hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba.

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامِهِمْ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَـٰئِكَ يَقْرَءُونَ كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ
فَتِيلًا ﴿٧١﴾

71. Siku tutakapowaita watu kwa Imam wao. Basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kuume, basi hao watasoma kitabu chao wala hawatadhulumiwa hata chembe.

وَمَن كَانَ فِي هَـٰذِهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾

72. Na aliyekuwa kipofu katika hii, basi Akhera atakuwa kipofu na aliyepotea zaidi njia.

## WANAADAMU TUMEWATUKUZA

**Aya 70-72**

### MAANA

Kwanini Mwenyezi Mungu amewatukuza wanaadamu? Kabla ya kujibu swali hili, kwanza tubainishe maana ya matamshi ya Aya.

Hakika tumewatukuza wanaadamu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtukuza binadamu kwa kumpa uwezo na ujuzi uliomfanya awe ni muheshimiwa mwenye kutukuzwa. Tutataja baadhi ya ujuzi huu na uweza baada ya kumaliza kufasiri matamshi ya Aya.

Na tumewabeba nchi kavu na baharini.

Kubebwa huku ni baadhi ya mambo aliyomtukuzwa nayo binadamu. Ni wazi kwamba kurahisishiwa mawasiliano ni katika mambo ya kuendeleza maisha watu.

Na tumewaruzuku vitu vizuri.

Kila linalomletea mtu manufaa kwa namna moja au nyingine, basi hilo ni zuri, lenye kheri na jema; liwe la kimaada au la kimaana.

Na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba.

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya wengi katika Aya ni wote. Kwa hiyo wakawaingiza Malaika, Suala hili limechukua kurasa ndefu za tafsiri; pamoja na kujua kuwa halina athari yoyote ya kiutendaji, isipokuwa kurefusha maneno.

Ilivyo hasa ni kuwa Aya iko mbali tena mbali sana na kufadhilisha baina ya binadamu na malaika. Na kwamba neno wengi linabaki kwenye dhahiri yake; kwani hakuna dharura ya kuleta taawili; bali elimu inawajibisha kubakia na dhahiri yake.

Kwani ugunduzi wa elimu umebatilisha nad- hariya isemayo kuwa ardhi ndio kituo kikuu cha ulimwengu na binaadamu ndiye bwana mkubwa wa ulimwengu wote.

Ugunduzi huu umehakikisha upotevu wa binadamu kulingana na ukubwa wa ulimwengu. Ugunduzi unathibitishwa na kukubaliwa na Qur'an, pale iliposema:

لَخَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

"Umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la watu, lakini watu wengi hawajui (40:57)

Yaani hii sayari ya ardhi ambayo anaishi binadamu ni mojwapo tu ya mamilioni ya sayari ambazo sayansi hazijui idadi yake, pamoja na kuwa imegundua mambo ambayo hayana ukomo. Zaidi ya hayo ni kwamba wataalamu wengi wanasema kuwa kuna sayari zinazokaliwa na viumbe vyenye akili pengine zaidi kuliko binadamu.

Ni kweli kuwa binadamu ni bwana mkubwa aliyetukuzwa, hilo halina shaka, lakini yeye si bwana wa viumbe vyote, bali ni mmoja tu kati ya mabwana. Hakuna jambo linalofahamisha hilo zaidi kuliko ujinga wa

binadamu kwenye vitu vingi na kushindwa kwake kuvitumia, Bali hajui vitu vingi vilivyomo ardhini; sikwambii vilivyo katika sayari nyingine. Kimsingi ni kwamba sharti la kwanza la ubwana ni uwezo wa kutumia vitu.

Baada ya kufafanua matamshi ya Aya, sasa tunadokeza mambo ambayo Mwenyezi Mungu amemtukuza nayo binadamu:

1. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemuumba mtu akalifanya zuri umbo lake na sura yake. Mwenyezi Mungu anasema:

وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ ﴿٦٤﴾

"Na akawatia sura na akazifanya nzuri sura zenu." (40:64).

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾

"Hakika tumemuumba mtu katika hali nzuri sana," (95:4).

2. Akili. Lau si hiyo, binadamu asingekuwa chochote, bali lau si akili muumba asingejulikana. Kwayo tunajua utukufu wa Mwenyezi Mungu na ukubwa wa ulimwengu na ukubwa wa akili yenyewe vilevile.

Mmoja wa wenye akili anasema: "Ikiwa ulimwenguni kuna nyota zinazomeremeta, basi ndani ya akili kuna nyota inayomeremeta na kuangaza. Ikiwa vitu vinavyotuzunguka vimepangiliwa kwa ufundi, basi akili ni kuu zaidi. Ikiwa wataalamu wa falaki wanaona kuwa mpangilio wa ndani wa ulimwengu na ukuu wake ni dalili ya ukuu wa Muumbaji, basi kuweko mtu ni dalili kubwa zaidi ya ukuu wa Mwenyezi Mungu. Ikiwa kuangalia mbin- guni kunamfanya mtu ahisi upotevu wake, basi kujifikiria mtu kunamfanya ahisi ubingwa na ukuu wa aliyemuumba na kuumba ulimwengu wote."

Ulimwengu ni mkuu na akili ni kuu. Kitu pekee cha kujua ukuu wa Mwenyezi Mungu, ulimwengu na mtu ni akili, Lakini usisahau kuwa sio mtu tu, peke yake ndiye aliyepewa akili.

3. Mtu ana sifa na siri nyingi: elimu na ujinga, dini na kufuru, mapenzi na chuki, upole na hasira, ujasiri na hofu, ukarimu na ubakhili, unyenyekevu na kiburi, uaminfu na hiyana, uthabiti na kuwa kigeugeu na mengineyo mengi yasiyokuwa na idadi. Sijui kama ametia chumvi aliyesema: "Binadamu sio kitu kimoja isipokuwa ni mamilioni ya vitu vilivyo na akili na vilivyo na wazimu, vilivyoendelea na visivyo na maendeleo."

4. Binadamu huwa anatafuta kuishi kwenye maisha, hata kama tayari yuko katika maisha bora, atatafuta bora zaidi. Kuna Hadith isemayo: "Lau mtu angelikuwa na mlima wa dhahabu na mwingine wa fedha, basi atatamani wa tatu." Ikiwa binadamu yuko hivyo, basi inafaa kwake pia kuwa na hamu kubwa ya kufikia kwenye utukufu zaidi.

5. Mtu ana sharia na misimamo, ambayo ni lazima aifuate na kuitumia. Ataulizwa na kuhisabiwa; na atakuwa mtukufu au mpuuzi.

6. Mtu anaathirika kwa waliopita na yeye anawathiri wajao, wakati huo huo akiathiriana na alio nao; wanamuathiri naye anawaathiri. Ndio maana akawa ana historia, turathi na athari, ambapo viumbe vingi havina.

7. Mtu ana maisha mengine, amabyo ni uwanja wa hukumu na malipo, kutokana aliyoyafanya katika maisha yake ya kwanza, na mengineyo katika neema alizoziashiria Mwenyezi Mungu kwa kauli yake:

وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّـهِ لَا تُحْصُوهَا ﴿٣٤﴾

“Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzidhibiti,” Juz;13 (14:34).

Siku tutakapowaita watu kwa Imam wao. Basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia , basi hao watasoma kitabu chao.

Imam ni yule anayefuatwa na kufutwa amri zake, Anaweza kuwa mtu, wahyi, akili au hawaa. Kuna Hadith isemayo: “Watu wataitwa Siku ya Kiyama kwa Imam wa zama zao, kitabu cha Mola wao na sunna ya nabiiwao.”

Makusudio ya kitabu katika Aya ni kitabu cha matendo ya mtu, watu wa kuume ni watu watiifu walio wema na watu wa kushoto ni waasi walio waovu.

Maana ni kuwa mnadi atanadi siku ya Kiyama: Wako wapi wafuasi wa Mitume na wa viongozi wema? Wako wapi waliotumia akili na dini? Watakuja na watachukua kitabu cha mambo wema na thawabu zake kwa mikono yao ya kuume, wakiwa na furaha.

Vilevile atanadi mnadi: wako wapi wafuasi wa madhalimu na wasaidizi wao? Wako wapi wahaini na wafisadi? Watakuja na watachukua kitabu cha maovu na adhabu yake kwa mikono yao ya kushoto wakiwa madhalili waliohizika.

Wala hawatadhulumiwa hata chembe.

Yaani Mwenyezi Mungu atamlipa kila mtu kulingana na matendo yake, hapunguzi thawabu za mwenye kufanya wema wala hazidishi adhabu ya mwenye kufanya uovu.

Na aliyekuwa kipofu katika hii, basi Akhera atakuwa kipofu na aliyepotea zaidi njia.

Katika hii, ni dunia na kipofu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliyezama kwenye ujinga. Wasifu wa fasaha zaidi katika hilo ni aliyoyasema Imam Ali (a.s):

**“Amepotelewa na makusudio, mwenye uchu wa maneno ya bid’a, mwenye kulingania upotevu. Yeye ni fitna ya mwenye kufitinika na ni mpotevu wa uongofu uliokuwa kabla yake, mpotezaji wa aliyemfuata katika uhai wake na baada ya kufa kwake”.**

Kwa ufupi wa maana ya Aya hii ni kwamba ambaye amali yake imekuwa mbaya katika maisha haya, basi mwisho wake huko Akhera utakuwa mbaya. Vile vile Aya hii inafahamisha wazi kuwa thawabu au adhabu katika Akhera inafungamana moja kwa moja na matendo katika maisha ya dunia.

Ndio maana ikasemwa: ‘Dunia ni shamba la Akhera.” Inatosha kuwa ni dalili kauli yake Mtume: “Watu watafufuliwa na niya zao.” Angalia Juz. 4 (3: 142).

9

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَإِن كَادُوا لَيَفْتِنُونَكَ عَنِ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ لِتَفْتَرِيَ عَلَيْنَا غَيْرَهُ ۖ وَإِذًا لَّاتَّخَذُوكَ خَلِيلًا ﴿٧٣﴾

73. Na hakika walikaribia kukufitini uache tuliyokupa wahyi ili utuzulie mengine, Na hapo wangelikufanya rafiki.

وَلَوْلَا أَن ثَبَّتْنَاكَ لَقَدْ كِدتَّ تَرْكَنُ إِلَيْهِمْ شَيْئًا قَلِيلًا ﴿٧٤﴾

74. Lau sikukuweka imara ungelikurubia kuwaelekea kidogo.

إِذًا لَّأَذَقْنَاكَ ضِعْفَ الْحَيَاةِ وَضِعْفَ الْمَمَاتِ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيْنَا نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

75. Hapo basi, tungelikuonjesha maradufu ya uhai na maradufu ya mauti; kisha usingelipata wa kukunusuru nasi.

وَإِن كَادُوا لَيَسْتَفِزُّونَكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا ۖ وَإِذًا لَّا يَلْبَثُونَ خِلَافَكَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٧٦﴾

76. Na kwa hakika walikaribia kukukera katika nchi ili wakutoe humo; na hapo wasingelibakia nyuma yako ila muda mchache.

سُنَّةَ مَن قَدْ أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِن رُّسُلِنَا ۖ وَلَا تَجِدُ لِسُنَّتِنَا تَحْوِيلًا ﴿٧٧﴾

77. Ndio desturi ya wale tuliowatuma kabla yako wala hutapata mabadiliko katika desturi yetu.

## JE MTUME ANAHADAIKA NA DINI YAKE

**Aya 73 -77**

### MAANA

Na hakika walikaribia kukufitini uache tuliyokupa wahyi ili utuzulie mengine, Na hapo wangelikufanya rafiki.

Waliokaribia ni washirikina. Walijaribu washirikiane na Mtume **(s.a.w.w)** kwa kumtaka awakubalie matakwa yao na wamfanye kuwa ni kiongozi na rafiki. Miongoni mwa hayo ni kuigusa miungu yao au angalau aache kuikashifu, lakini Mtume hakuwakubalia matakwa yao washirikina, kwa sababu yeye ni maasum na maasum hawezi kuchangia dini yake na risala yake na mambo mengine.

**Unaweza kuuliza**: Kauli yake Mwenyezi Mungu: 'walikaribia kukufitini' inafahamisha kuwa yeye Mtume alikaribia kuwakubalia matakwa yao?

**Jibu**: Aya hii inafungamana moja kwa moja na Aya inayofuatia.

Lau sikukuweka imara ungelikurubia kuwaelekea kidogo.

Kwa hiyo maana ni kuwa, hakika wewe Muhammad lau si ulinzi wetu kwako kwa kukupa isma (kuhifadhika) ya dhambi, basi ungelikaribia kuwaelekea washirikina na kuwatikia maombi yao, Isma ndiyo iliyokuzuia kuwakubalia. Ni sawa na kusema: 'Lau si fulani ungeliangamia' Umetangulia mfano wake katika Juz; 12 (12: 24).

Zaidi ya hayo, kufikiria kufanya kitu ni jambo jingine na kukifanya ni jambo jingine. Kuna Hadith mutawatir kutoka kwa Mtume kwamba yeye amesema: "Umeondolewa umma wangu yale yanayozungumzwa na nafsi zao madamu hawakufanya au kuzungumza," yaani kujizungumzia mtu mwenyewe nafsini mwake, hakuna athari, Kuna mapokezi yanayosema, kuwa washirikina walipomwambia Mtume alinyamaza, hakuwajibu.

Hapo basi, tungelikuonjesha maradufu ya uhai na maradufu ya mauti.

Maana ni kuwa, ewe Muhammad! Lau ungeliwaelekea washirikina tungelikuadhibu mara mbili zaidi ya mwengine, duniani na Akhera. Kwa sababu adhabu ya wakuuu inakua kulingana na ukuu wao na cheo chao. Hii ni kiasi cha kukadiria tu, na ‘kukadiria muhali sio muhali.’

Kisha usingelipata wa kukunusuru nasi, kukukinga na adhabu.

Katika Nahju-lbalagha imeelezwa: “Siku ya Kiyama ataletwa kiongozi mkandamizaji, akiwa hana wa kumsaidi wala wa kumtolea udhuru, atatupwa katika Jahannam, azunguke humo kama pia, kisha afungwe kwenye shimo lake.”

Na kwa hakika walikaribia kukukera katika nchi ili wakutoe humo; na hapo wasingelibakia nyuma yako ila muda mchache.

Waliposhindwa washirikina na Mtume walijaribu kumkera kwa kila njia ili atoke Makka, Lau wangelimtoa, basi Mwenyezi Mungu angeliwangamiza muda kidogo baada ya kutoka kwake.

**Unaweza kuuliza kuwa**: si walifanya hivyo washirikina pale walipoafikiana kumuua Mtume, mpaka akalazimika kutoka kwenda Makka kwa kuhofia, kama ilivyoelezwa katika Juz. 9 (8:30).

**Jibu**: makusudio ni kuwa lau washirikina wangelimtoa wao kwa nguvu na kua ni mkimbizi aliyefukuzwa asiyejua pa kwenda, basi Mwenyezi Mungu angeliwangamiza haraka sana. Lakini Mtume alitoka Makka kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwenda kwa watu ambao walijitolea kwake kwa hali na mali na familia.

Ndio desturi ya wale tuliowatuma kabla yako wala hutapata mabadiliko katika desturi yetu.

Yametangulia maelezo kuhusu hukumu ya Mwenyezi Mungu na kadha yake, kwamba kaumu yoyote itakayomtoa Mtume wao kwa nguvu, Mwenyezi Mungu anaiangamiza haraka. Na hii ndio desturi katika viumbe vyake, haibadiliki wala haigeuki, inaendela wakati wote na mahali kote.

أَقِمِ الصَّلَاةَ لِدُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَىٰ غَسَقِ اللَّيْلِ وَقُرْآنَ الْفَجْرِ ۖ إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿٧٨﴾

78. Simamisha Swala linapopinduka jua mpaka giza la usiku, na Qur'an ya alfajiri; hakika Qur'an ya alfajiri imekuwa ni yenye kushuhudiwa.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾

79. Na katika usiku amka kwayo ni ziada kwa ajili yako; huenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika.

وَقُل رَّبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ وَأَخْرِجْنِي مُخْرَجَ صِدْقٍ وَاجْعَل لِّي مِن لَّدُنكَ سُلْطَانًا نَّصِيرًا

﴿٨٠﴾

80. Na sema: Mola wangu! Niingize muuingizo mwema na nitoe kutoka kwema, na unipe madaraka kutoka kwako ya ushindi.

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ ۚ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾

81. Na sema, haki imefika na batili imetoweka. Hakika batili ni yenye kutoweka.

## SIMAMISHA SWALA LINAPOPINDUKA JUA

**Aya 78-81**

## MAANA

Aya ya kwanza na ya pili ni miongoni mwa Aya za hukumu, zilizoshuka kwa ajili ya kubainisha nyakati za Swala. Wana-Fiqh wana kauli kadhaa, kama zifuatavyo:

1. Simamisha Swala linpopinduka jua mpaka giza la usiku.

Wametofautiana katika makusudio ya kupinduka jua, Imesemekana ni wakati wa kutua jua na ikasemkena ni kupinduka nusu ya mzingo wa mbingu (meridian), na hiyo ndiyo kauli ya wengi.

Imepokewa kutoka kwa Imam Ja'far As-swadiq (a.s) kwamba giza la usiku ni nusu ya usiku.

Katika tafsiri za kisunni na kishia imeelezwa kuwa Aya hii imekusanya nyakati zote za Swala tano: Adhuhuri na Alasiri zinaingia katika kupinduka jua. Magharibi na Isha zinaingia katika giza la usiku na Asubuhi katika Qur'an ya alfajiri.

Katika Shia amesema Tabrasi kwenye Majmau-bayan: "Aya hii imekusanya Swala tano: Swala ya adhuhuri na alasiri zinaingia katika kupinduka jua, swala ya magharibi na isha zinaingia katika giza la usiku na makusudio ya Qur'an ya alfajiri ni swala ya alfajiri; Hizi ndizo Swala tano."

Katika sunni amesema Razi: "Simamisha Swala, yaani idumishe kuanzia wakati wa kupinduka jua mpaka giza la usiku, inaingia swala ya adhuhuri, alasiri magharibi na isha" Kisha akaendela kusema: "wamekongamana kuwa makusudio ya Qur'an ya alfajiri ni Swala ya asubuhi."

Ilivyo ni kwamba mafaqihi, katika vitabu vyao, wanaanza maneno kwa Swala ya adhuhuri kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'linapopinduka jua' ambapo ameanzia Mwenyezi Mungu (s.a.w.) kwa kutaja wakati wake.

Kuongezea mapokezi ya Hadith zinazoelezea kuwa adhuhuri ndiyo ya kwanza kufaradhishwa, kisha zikafuatia nyingine kwa utaratibu ulivyo. Hilo lilikuwa Makka usiku wa Israi, mwaka mmoja kabla ya Hijra (kuhamia Madina).

Madhehebu za kiislamu zimeafikiana kuwa haifai Swala kabla ya kuingia wakati wake na kwamba jua likipinduka ndio umeingia wakati wa Adhuhri, lakini wametofautiana kwenye kiwango cha muda huu, unaisha wakati gani?

Shia Imamiya wamesema kuwa mara tu bada ya kupinduka jua unahusika wakati wa Swala ya adhuhuri kwa kiasi cha kuswaliwa kwake na kiasi cha kuweza kuswaliwa swala ya alsiri mwisho wa mchana kinahusika na Swala ya alasiri. Baina ya wakati wa kwanza na wa mwisho ni wa ushirikano wa Swala mbili; yaani inaweza kuswalia adhuhuri na alasiri.

Dhahiri ya Aya iko pamoja nao: 'linpopinduka jua mpaka giza la usiku' wala Mwenyezi Mungu hakutenganisha; kama ilivyo kwenye madhehebu nyingine.

Wengineo wamesema kuwa wakati wa adhuhuri unaanza linapopinduka jua mpaka kuwa kivuli cha kila kitu mfano wake, ikizidi hapo wakati wa adhuhuri utakuwa umekwisha na utakuwa wakati wa alasiri umeingia. Ufafanuzi uko katika kitabu chetu: Al-fiqh ala madhahib al-khamsa (Fiqh kwenye madhehebu matano).

2. Na Qur'an ya alfajiri. Hakika Qur'an ya alfajiri imekuwa ni yenye kushuhudiwa.
Wameafikiana kwamba makusudio ya Qur'an ya alfajiri ni ile inayosomwa katika Swala ya alfajiri, yaani ya asubuhi. Vil vile wameafikiana kwamba wakati wake unaanzia kutokeza alfajiri ya kweli mpaka kutoka jua (mawiyo); isipokuwa Maliki anasema kuwa asubuhi ina nyakati mbili: Ya hiyari, inaanzia alfajiri hadi kujuana nyuso. Na wakati wa dharura unaoanzia kujuana nyuso hadi kutoka jua. Kauli ya kushangaza ni ile ya masufi wanaosema kuwa makusudio ya alfajiri ni kupasuka moyo.
Wamekongamana mafaqihi, kwa ushahidi wa Tabrasi na Razi, kwamba makusudio ya yenye kushuhudiwa, ni kwamba Malaika wa usiku na mchana wanakusanyika ili washuhudie Swala. Wametegemea riwaya aliyoipokea Bukhari kutoka kwa Abu Hurayra, katika Sahih Bukhari Juzuu ya 6 mlango wa sura Bani Israil, Sisi tunaishuku riwaya hii. Na tunafasiri yenye kushuhudiwa, kuwa ni kuhudhuria hisiya. Kwa sababu mtu wakati wa asubuhi hisia zake zinakuwa zipo baada ya kupumzika na usingizi. Ndio maana ikasemwa 'usingizi unabeba maazimio ya siku'
3. Na katika usiku amka kwayo ni ziada kwa ajili yako.
Kwayo ni hiyo Qur'an. Kwa ajili yako ni kumuhusisha yeye tu. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu amekufaradhishia wewe Muhammad swala nyingine, zaidi ya zile tano ambazo ni zako na wengine, uiswali usiku. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

يَا أَيُّهَا الْمُزَّمِّلُ ﴿١﴾ قُمِ اللَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾

"Ewe mwenye kujifunika nguo! Simama usiku isipokuwa kidogo" (73:1-2)

وَمِنَ اللَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهُ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا طَوِيلًا ﴿٢٦﴾

" Na usiku umsujudie Yeye na umtakase usiku mrefu." (76:26).
Swala hii inaitwa Swala ya usiku (swalatu-llayl); wakati wake ni kuanzia nusu ya usiku hadi alfajiri. Ni wajibu kwa Mtume **(s.a.w.w)**, kama tulivyoeleza mwanzo na ni sunna kwa mwenginewe.

Huenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika.

Huenda ni neno la kutarajia ikiwa linatoka kwa kiumbe na ni la mkato ikiwa linatoka kwa muumbaji, Hapa anaambiwa Muhammad **(s.a.w.w)**.
Hakuna kitu zaidi ya Muhammad wala cheo zaidi ya Muhammad na kizazi zaidi ya kizazi cha Muhammad; isipokuwa yule ambaye hakuna mfano wake kitu chochote. Kuna Hadithi isemayo kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alifasiri cheo chenye kusifika katika Aya hii kuwa ni cheo atakachowaombea umma wake kesho.

Na sema: Mola wangu! Niingize muuingizo mwema na nitoe kutoka kwema.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake mtukufu kuomba dua hii. Kuingia kwema na kutoka kwema ni fumbo la haki na ikhlsi katika itikadi, makusudio, vitendo, harakati zote na kupumzika. Hakuna shaka kuwa mwenye kuwa na silaha ya haki na akamfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu peke yake, basi atamuimarisha kwa kauli thabiti, atampa hoja imara na umakini wa moyo ulio mwema na safi.

Na unipe madaraka kutoka kwako ya ushindi.

Kuna ushindi na madaraka yanayozidi kutajwa Mtume mtukufu pamoja na jina la Mwenyezi Mungu mara tano kwa siku, katika adhana na katika swala za wajibu na sunna? Kuna nguvu gani na heshima adhimu kuliko ile aliyompa Muhammad, aliposema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ﴿٧﴾

"Anachowapa Mtume kichukueni na anachowakataza kiacheni," (59:7).

Na sema haki imefika na batili imetoweka. Hakika batili ni yenye kutoweka.

Haki ni risala ya Muhammad, itikadi na sharia. Vinginevyo ni batili, kiuhalisi na mbele ya Mwenyezi Mungu; hata kama vitaaminiwa na watu wa ardhini wote. Wafasiri wamesema kuwa makusudio ya batili hapa ni ushirikina na kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alipoikomboa Makka aliingia Al-ka'ba na mlikuwa na masanamu 360, akawa anazisukuma huku akisema: "Haki imefika na batili imetoweka, Hakika batili ni yenye kutoweka."

## NGUVU YA HAKI NA NGUVU YA BATILI

**Unaweza kuuliza**: Mara nyingi tunaona na kushuhudia watu wa batili wakishinda na watu wa haki wakishindwa. Hii si inapingana na kauli ya Mwenyezi Mungu 'Hakika batili ni yenye kutoweka'?

**Jibu**: Hakika haki ina nguvu za dhati zisizoepukana nazo kwa hali yoyote; nazo zinatenda kazi na kuathiri kwenye nyoyo safi zilizo takatifu. Mara nyingi athari hii inafikia kiwango ambacho hakuna nguvu yote yote inayoweza kuisimamisha; si mapanga ya wachinjaji wala unyongaji wa mataghuti.

Historia inatusimilia jinsi mashahidi wa itikadi walivyojitolea kuwa mashahidi kwa nyuso za kutabasamu na nafsi zilizo radhi; bali hayo yametokea wakati wetu huu huko Vietnam, Korea, Palestina na kwengineko.

Ndio! Ni kweli hawa ni wachache; kama ilivyo kawaida ya kila jambo tukufu lenye thamani. Lakini wangelikuwa wengi kwa idadi au wengi kwa viwango vya asilimia, basi dunia ingelijaa uadilifu, na dhulma na jeuri isengelikuwa na athari yoyote. Sisi hatuna shaka ubinadamu utakwenda na njia hii; hata kama muda utakuwa mrefu.

Ama batili, haina nguvu wala urefu, isipokuwa kuweko kwake kunategema rushwa, dhulma, ukandamizaji, kuwafukuza watu njama n.k.

Haya yote yataondoka kadiri siku zinavyokwenda na hali kubadilika. Ama nguvu ya haki huwa inakwenda na wakati, inabakia hivyo hivyo tu wakati wote. Kwa sababu inategema hiyo haki yenyewe, kama ilivyo. Kwa ajili hii ndio tunasema tena: Sisi tuna imani isiyokuwa na shaka kwamba mwisho ni wa haki na neno la juu litakuwa la haki peke yake.

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۙ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

82. Na tunateremsha katika Qur'an ambayo ni ponyo na rehema; Wala haiwazidishii madhalimu isipokuwa hasara.

وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَى الْإِنسَانِ أَعْرَضَ وَنَأَىٰ بِجَانِبِهِ ۖ وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ كَانَ يَئُوسًا ﴿٨٣﴾

83. Na tunapomneemesha mtu hugeuka na kujitenga kando na inapomgusa shari hukata tamaa.

﴿قُلْ كُلٌّ يَعْمَلُ عَلَىٰ شَاكِلَتِهِ فَرَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَنْ هُوَ أَهْدَىٰ سَبِيلًا ﴿٨٤﴾

84. Sema: kila mmoja anafanya kwa namna yake, Na Mola wenu anajua aliyeongoka katika njia.

﴿وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ ۖ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

85. Wanakuuliza kuhusu roho, Sema: roho inatokana na amri ya Mola wangu. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu.

## QUR'ANI NI PONYO

**Aya 82-85**

### MAANA

Na tunateremsha katika Qur'an ambayo ni ponyo na rehema.

Qur'an ni rehema kwa yule anayeitakia nafsi yake rehema na ni ponyo la ukafiri, ulahidi, ujinga, ufisadi na kila uchafu, kwa yule mwenye kumfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu na haki.

Imam Ali (a.s) katika kuisifu Qur'an ansema: **"Hakika hiyo ni kamba imara, nuru inayobainisha, ni dawa yenye kuleta nafuu, ni kichujio cha takataka, ni hifadhi kwa mwenye kushikamana nayo na ni uokovu kwa mwenye kufungamana nayo."** Mwenye kuhalifu hukumu miongoni mwa hukumu za Qur'an atakuwa miongoni mwa madhalimu na waliohasirika.

Wala haiwazidishii madhalimu isipokuwa hasara.

Qur'an ni rehema kwa waumini na nakama kwa madhalimu na wafisadi, kwa sababu kila wanapoasi hukumu miongoni mwa hukumu zake, wanazidi dhambi na adhabu.

Na tunapomneemesha mtu hugeuka na kujitenga kando na inapomgusa shari hukata tamaa.

Maana ya Aya hii yanafupilizwa na kauli ya Imam Ali (a.s) katika wasifu wa mtu: "Akijitosheleza huchangamka na kushawishika na anapofukarika hukata tamaa na kubweteka. Umepita mfano wake katika Juz; 11 (10:12) na Juz. 12 (11: 9).

Sema: kila mmoja anafanya kwa namna yake, Na Mola wenu anajua aliyeongoka katika njia.

Wafasiri wamesema: "Namna, ni njia. Na maana ya Aya ni kuwa kila mmoja kati ya mumin na kafiri anafanya kwa njia yake na maumbile yake" lakini sisi tutaifafanua, kama tulivyoifahamu, katika hali zifuatazo:

1. Neno kila mmoja linafahamisha kuenea kwa mtu mmoja mmoja; kwa mfano ukisema: kila mtu analifahamu hili, ni kama umesema: Zayd analifahamu na Bakari, Hindu n.k. (yaani kila mmoja ana namna yake ya kulifahamu) Lakini ukisema: watu wote wanalifahamu, itakuwa kadhia ni moja na hukumu itakuwa imewaenea kwa ujumla sio kwa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo maana ya Aya ni kuwa kila mmoja katika watu ana namna yake inayomuhusu yeye peke yake; kama vile alama za vidole, kila mmoja ana zake.

2. Imepokewa Hadith kutoka kwa Ja'far As-swadiq (a.s) kwamba yeye amefasiri namna kwa maana ya nia. Usahihi wa tafsiri hii unafahamika kutoka na kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na Mola wenu anajua aliyeongoka katika njia' iliyokuja moja kwa moja bila ya kuweko kiunganishi kingine." Yaani Mwenyezi Mungu anamjua anayetaka

kuongoka na kufu- ata njia yake bila ya makusudio mengine yoyote isipokuwa dhati yake Aliye Mtukufu.
Kwa hiyo maana ya Aya yatakuwa: Kila mtu anafanya kulingana na nia yake na kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) atapambana naye kulingana na nia yake; ikiwa kheri basi ni kheri na ikiwa ni shari basi itakuwa ni shari.
Mwenye kudhihirisha kheri mbele ya watu ili awahadae watu na kumbe ana malengo ya shari, basi huyo mbele ya Mwenyezi Mungu ni mshari. Na mwenye kuiba mkate ili ajisitiri njaa baada ya kukosa budi, akiwa hana njia nyingine, basi huyo mbele ya Mwenyezi Mungu hastahiki adhabu.

## ROHO INATOKANA NA AMRI YA MOLA WANGU

Wanakuuliza kuhusu roho, Sema: roho inatokana na amri ya Mola wangu. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu.

Roho ina maana nyingi. Makusudio yake hapa ni uhai. Mtume **(s.a.w.w)** aliulizwa kuhusu roho, Mwenyezi Mungu akamwamrisha amwambie muulizaji kuwa roho ni katika vitu vinavyopatikana kwa amri ya Mungu ambayo ni kusema ‘Kuwa na ikawa.’
Kwa ufafanuzi zaidi ni kuwa vitu viko aina mbili: Aina ya kwanza, Mwenyezi Mungu anavileta kupitia sababu za kimaumbile kutokana na maada; kama mwili wa binadamu.
Aina ya pili ni ile inayopatikana kwa kiasi cha amri tu; ambayo ni neno ‘kuwa’ Na roho ni katika aina hiyo. Aya imeliweka wazi hilo, Kwa sababu neno: ‘roho inatokana na amri ya Mola wangu,’ ni ishara ya neno ‘amri’ lilioko katika kauli yake nyingine Mwenyezi Mungu:

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَن يَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

“Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia kuwa! Na kikawa,” (36:82).
Majaribio yamethibitisha hakika hii na wakaiamini wale waliobobea na kumaliza miaka mingi kwenye utafiti wa asili ya uhai. Waliamni hakika hii baada ya kubainika kwamba sababu ya moja kwa moja ya uhai haina muungano wowote wa kuishia kwenye maada. Lau ingelikuwa inaishia kwenye maada, wangeliweza kumtengeneza binadamu kwenye viwanda vyao na maabara yao.
Wamejaribu wakashindwa: “Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu.” Yaani kadiri viwanda vyenu vinavyotengeneza vitu vya ajabu, lakini si chochote kulingana na chembe hai za nzi, sikwambii nzi mwenyewe: “Enyi watu! Umepigwa mfano, basi usikilizeni, Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, hawataumba hata nzi, wajapojumuika kwa hilo, Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kutoka kwake.

ضَعُفَ الطَّالِبُ وَالْمَطْلُوبُ ﴿٧٣﴾

Amedhoofika huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa,”(22:73)
Umepita mfano wake katika Juz; 9 ( 6:95).

## MWENYEZI MUNGU NA ELIMU YA CHEMBE HAI

Imetokea sadfa, wakati nikifasiri Aya hii, nikasoma makala katika gazeti Ruzil Yusuf la Misri[1] toleo la April 1969 likiwa na maelzo haya:

"Mwili wa mtu una mamilioni ya chembe hai ambazo haziwezi kuonekana isipokuwa kwa darubini. Katika miaka ya karibuni ilikuwa ni vigumu kuweka elimu ya chembe kwa sababu wataalamu walikuwa hawawezi kuzifungua hizo chembe au kuzidunga sindano. Kwa vile kazi ilikuwa inahitaji chombo kidogo kuliko milimita elfu moja, basi sindano nayo ingelihitajika iwe na ncha ndogo kuliko milimita milioni moja.

Hatimae walifanikiwa wataalamu kuzifungua chembe hizo kupitia mwanga, sawa na tunavyowasha sigara kutokana na mwanga wa jua kupitia kioo. Ni njia pekee iliyowawezesha wataalamu kuzifungua chembe hai na kugundua kuwa ni mkusanyiko uliosheheni makumi ya viumbe mbalimbali, kila kimoja kikiwa na sifa yake maalum na kazi yake na mfungamano ulionacho pamoja na wakazi wengine wa chembe hizo.

Kuweza kufahamu kazi hizo na mifungamano hiyo, kutahitajia miaka ya utafiti kama sio vizazi. Ndio ikaanza elimu ya chembe hai na tukawa sasa tunajua kwamba chembe hai zina mwili na viungo, utando, nyuzi na mengineyo ya kushangaza akili.

Imedhihirika kwamba chembe hai za damu ni mkusanyiko wa chembe zinazoelea. Idadi yake ni mara kumi zaidi ya watu wote. Mkusanyiko huo unatengeneza chembe nyingine kila baada ya miezi mine na kuhifadhi idadi ya chembe nyingine, kiasi ambacho zile zinazokuja hazipungui wala kuzidi zile zilizoondoka. Wala hazina matatizo ya makazi kwa sababu ya wingi, kama ilivyo kwa watu.

Hapa ndio kuna maajabu! Ubongo wa mifupa uzalishe mikondo ya damu ya aina na iliyo na kazi tofauti tofauti yenye chembe nyekundu na nyeupe zinazoua na zinazokinga, Vipi basi jinsi moja ilete jinsi nyingi tofauti tofauti? Kwani ngamia anaweza kuzaa ndovu, tena azae mamba, kisha azae kicheche? Lakini kwenye damu linapatikana hilo. Haya ni maajabu kweli! Kwa ufupi kabisa ni kwamba chembe hai hivi sasa zimekuwa ndio gumzo kubwa la utafiti wa kisayansi na njia yake mpya; pengine ni njia pekee ya kufahamu siri za uhai."

Umeona maajabu haya! Kiumbe kidogo ambacho hakiwezi kuonekana isipokuwa kwa kukuzwa mara elfu, tena hakiwezi kupasuliwa ila kwa mwangaza, unywele kwake ni kama ndovu aliye kwenye chungu chungu.

Pamoja na yote haya, kiumbe hiki kina viungo, mishipa, utando na mengineyo; kama mwanadamu. Kisha viumbe hivi, vya ajabu, vinafanya maskani yake ndani ya mwili wa mtu, vikiwa ni mamilioni, kwa kiasi cha miezi mine kisha vinakuja vingine kwa idadi ile ile ya vile vilivyoondoka bila ya kuzidi wala kupungua; kisha vingine na vingine na kuendelea.

Je, hii yote ni sadfa? Je, sadfa inaweza kukaririka mara bilioni. Je, viungo vyote hivyo, utando na nyuzi zilizofumwa kwa nidhamu na mpangilio ni sadfa?

---

1. Nimeupanga wakati wangu kwa namna hii ifuatayo: Saa nzima na nusu, kabla ya adhuhuri ni ya kununua mahitaji ya nyumbani na kusoma magazeti. Saa nzima na nusu usiku ni ya kusoma utafiti mpya wa kielimu na kijamii, mbali ya kazi nyingine za utungaji.

Je sadfa inaweza kuzalisha vitu vya aina mbali mbali kutoka katika aina moja? Maswali yote haya na mengineyo yanataka jawabu.
Hapana! Tena hapana kabisa! Hakuna tafsiri ila kuweko Mjuzi mwenye uweza wa kuumba ulimwengu na uhai kwa neno 'Kuwa' na ikawa.
Baada ya hayo, kila sayansi inavyozidi kupiga hatua, ndio dalili na ushahidi wa kuweko Muumba mwenye amri, unazidi. Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu, aliyesema: "Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu".

وَلَئِن شِئْنَا لَنَذْهَبَنَّ بِالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ بِهِ عَلَيْنَا وَكِيلًا ﴿٨٦﴾

86. Na tungelipenda, tungeliyaondoa tuliyokupa wahyi; kisha usingelipata wakili wa haya juu yetu.

إِلَّا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ إِنَّ فَضْلَهُ كَانَ عَلَيْكَ كَبِيرًا ﴿٨٧﴾

87. Isipokuwa rehema itokayo kwa Mola wako. Hakika fadhila yake kwako ni kubwa.

قُل لَّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَن يَأْتُوا بِمِثْلِ هَـٰذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ

بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾

88. Sema: Lau wangelikusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'an, basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِي هَـٰذَا الْقُرْآنِ مِن كُلِّ مَثَلٍ فَأَبَىٰ أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٨٩﴾

89. Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'an kwa kila mfano, lakini watu wengi wamekataa isipokuwa kukanusha tu.

## TUNGELIPENDA TUNGELIONDOA

**Aya 86- 89**

### MAANA

Na tungelipenda, tungeliyaondoa tuliyokupa wahyi.

Razi anasema, katika kufasiri Aya hii, kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) baada ya kubainisha, katika Aya iliyotangulia, kuwa yeye amewapa elimu kidogo tu, hapa anabainisha kwamba yeye lau angelitaka kuwaondolea hiki kidogo, angeliweza, Na hilo ni kwa kufuta kuhifadhika kwake moyoni na maandishi yake ya vitabuni.

Kisha usingelipata wakili wa haya juu yetu, utakayemtegemea akutetee kukurudishia tulichokichukua kwako. Isipokuwa rehema itokayo kwa Mola wako; Hiyo pekee ndiyo inayoweza kukurudishia ambacho tungekichukua kwako.

Hakika fadhila yake kwako ni kubwa kutokana na elimu aliyokupa na ubwana juu ya watu wote.

Sema: lau wangelikusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'an, basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.

Umepita mfano wake katika Juz 1 (2: 23).

Hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'an kwa kila mfano, katika yanayohusiana na itikadi, sharia na maadili. Na tukaweka hoja mkataa na dalili wazi, lakini watu wengi wamekataa isipokuwa kukanusha tu, na kuwa mbali na haki. Kwa sababu iko chungu na ni nzito, hawawezi kuivumilia isipokuwa wenye takua.

وَقَالُوا لَن نُّؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنبُوعًا ﴿٩٠﴾

90. Na walisema: hatutakuamini mpaka utuchimbulie katika ardhi hii chemchemi.

أَوْ تَكُونَ لَكَ جَنَّةٌ مِّن نَّخِيلٍ وَعِنَبٍ فَتُفَجِّرَ الْأَنْهَارَ خِلَالَهَا تَفْجِيرًا ﴿٩١﴾

91. Au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu na utupitishie mito kati yake ikimiminika.

أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمْتَ عَلَيْنَا كِسَفًا أَوْ تَأْتِيَ بِاللَّـهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿٩٢﴾

92. Au utuangushie mbingu vipande vipande, kama ulivyodai, au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika ana kwa ana.

أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِّن زُخْرُفٍ أَوْ تَرْقَىٰ فِي السَّمَاءِ وَلَن نُّؤْمِنَ لِرُقِيِّكَ حَتَّىٰ تُنَزِّلَ عَلَيْنَا كِتَابًا
نَّقْرَؤُهُ ۗ قُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنتُ إِلَّا بَشَرًا رَّسُولًا ﴿٩٣﴾

93. Au uwe na nyumba ya dhahabu au upae mbinguni, Na hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie Kitabu tukisome. Sema: ametakasika Mola wangu! Kwani mimi ni nani, isipokuwa ni mwanadamu Mtume?

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَن يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَن قَالُوا أَبَعَثَ اللَّـهُ بَشَرًا رَّسُولًا ﴿٩٤﴾

94. Na nini kilichowazuia watu kuamini ulipowajia utume, isipokuwa walisema: je, Mwenyezi Mungu hupeleka mwanadamu kuwa Mtume?

قُل لَّوْ كَانَ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَمْشُونَ مُطْمَئِنِّينَ لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ مَلَكًا رَّسُولًا ﴿٩٥﴾

95. Sema: Lau ingelikuwa duniani kuna Malaika wanaotembea kwa utulivu, basi bila ya shaka tungeliwateremshia Malaika kuwa Mtume wao.

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّـهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۚ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٩٦﴾

96. Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi. Hakika Yeye anawajua vyema waja wake na anawaona.

## KUFIKIRIA MALI

**Aya 90-96**

### KUJIPENDA

Kila mmoja wetu anajipenda; awe mwana mume au mwanamke, mzee au mtoto, mwenye takua au muovu n.k. Ni binadamu gani asiyekuwa na shauku na maisha yake na kutetea heshima yake na uhalisi wake? Lau si hivyo uhai usingeendelea kuwako wala tusingeendelea, Hakuna tofauti katika kujipenda huko baina ya watu; isipokuwa tofauti iko katika aina zifutazo:-

Kuna yule anayekuwa kwenye msingi wa maumbile na akili. Hili linafahamika kutokana na jinsi mtu anavyoheshimu haki za wengine, kutosheka na alichoandikiwa kilichotokana na jasho lake na kusaidiana na kila mwenye kutumai kheri na manufaa ya watu kwa namna moja au nyingine; bali hata kujitolea juu ya hilo.

Kwani mwenye kutoa na kujitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, atakuwa amejipenda, atake asitake, kwa sababu Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa mwenye kufanya wema, vile vile jamii inamsifu na kumtukuza yule mwenye kujitolea kwa ajili ya hiyo jamii.

Na kuna yule anayejipenda kwa kutumia yale yanayopituka akili, dini na uhalisi. Hili linafahamika kutokana na tamaa ya mtu ambaye haioni umuhimu wala manufaa ya mwingine isipokuwa wake.

Hili halikubaliki na mantiki yoyote; hata ya yahisia na ya kuonekana; sawa na alivyosema Mwenyezi Mungu: "Wana nyonyo, lakini hawafahamu

kwazo, na wana macho, lakini hawaoni kwayo, na wanayo masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama bali wao ni wapotevu zaidi, Hao ndio walioghafilika." Juz; 9 (7: 179). Hawa wako kila mahali na kila wakati; miongoni mwao ni wale aliowaashira Mwenyezi Mungu kwa kuli zake zifuatazo:-

1. Na walisema: hatutakuamini mpaka utuchimbulie katika ardhi hii chemchem.

wapenda raha katika washirikina walitoa pendekezo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa awachimbulie chemchem au mto, wao sio watu wengine, kwa ajili ya chumo na faida. Kuna mapokezi yanayosema kuwa vijoho na wapenda anasa walisema: Ewe Muhammad! Hii ardhi ya Makka ni finyu, basi yaondoe majabali yake na utuchimbulie chemchem ili tunufaike na ardhi.

2. Au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu na utupitishie mito kati yake ikimiminika.

Yaani kama hutatuchimbulia chemchem, basi angalu jichimbulie wewe, ili uwe unafanana na hadhi ya juu, Lakini ukiwa huna kitu basi wewe unatakikana uwasikilize walio nacho. Kwamba mali peke yake ndiyo itakayomfanya aliye nayo awe anafaa kuwa kiongozi na bwana mkubwa. Hawakujua kuwa risala ya Muhammad **(s.a.w.w)** ni utajiri mkubwa wa mtu, uhai wake, na kwamba Muhammad ni rehema kwa watu wa ardhini itakayowaokoa na ufukara, ujinga, dhulma na utaghuti. Wapi na wapi wanaoabudu mali na kupigana vikumbo na tamaa waweze kujua rehema na kheri?

3. Au utuangushie mbingu vipande vipande, kama ulivyodai, au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika ana kwa ana.

Walitaka wachimbuliwe chemchem yao au yake; kam sio hivyo au vile, basi awalete adhabu kutoka mbinguni au Mwenyezi Mungu mwenyewe aje na malaika kushuhudia kuwa Yeye ni Mtume.

Hii vile vile inatokana na fikra yao kwamba anayestahiki uongozi ni tajiri, sio fukara. Dalili ya hilo ni kule kuweka sharti la kumwamini Muhammad na jambo wanaloliona kuwa haliwezekani. Ni wazi kuwa kulazimisha jambo lisilowezekana maana yake ni kung'ang'ania matakwa yao ya kuchimbuliwa chemchem ardhini; sawa na kusema: Sifanyi hivi mpaka ngamia apite kwenye tundu ya sindano.

4. Au uwe na nyumba ya dhahabu.

Yaani iliyojengwa kwa dhahabu au iliyopambwa nayo. Hii vile vile inatokana na fikra ya mali.

Au upae mbinguni.

Nalo hili linafungamana na jambo lisilowezekana. Maana yake ni kung'ang'ania kuwa mali ndio kitu pekee cha kumweka mtu kwenye cheo.

Na hatutaamini kupaa kwako mpakaututeremshie Kitabu tukisome.

Baadhi ya wafasiri wapya wanasema: "Unadhihiri utoto wa kuhafamu na kufikria; kama unavyodhihiri ukaidi wa kipumbavu." Lakini hapana huo si utoto wala si upumbavu; isipokuwa hilo linatokana na ufisadi, kujibagua, uporaji, unyang'anyi na kuabudu mali. Kitu kinachofahamisha hilo zaidi ni kule kupendekeza na kuweka sharti la kumfuata Mtume awe na nyumba ya dhahabu kuwa ndio muabudiwa wao wa kwanza na ndio mfano wao mkuu.

Sema: Ametakasika Mola wangu! Kwani mimi ni nani, isipokuwa ni mwanadamu Mtume?

Anayefuata amri ya yule aliyemtuma na kukatazika kwa makatazo yake:

وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَن يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّـهِ ﴿٣٨﴾

"Haiwi kwa Mtume kuleta muujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Juz; 13 (13:38).

Na nini kilichowazuia watu kuamini ulipowajia utume, isipokuwa walisema: je, Mwenyezi Mungu hupeleka mwanadamu kuwa Mtume?

Wafasiri, akiwemo Tabrasi na Razi, wameiangalia Aya hii kuwa haiungani na Aya zilizotangulia na wakasema katika kuifasiri: Hakika washirikina wa Makka hawakumwamini Muhammad **(s.a.w.w)** kwa sababu wao walikuwa wakiitakidi kuwa mjumbe ni lazima awe ni katika jinsia ya malaika, si katika jinsia ya watu. Lakini tafsiri hiyo iko mbali sana kutokana na njia zifuatazo:-

Washirikina wa kikuraishi walikuwa wakiamini utume wa Ibrahim na kwamba wao wanatokana na kizazi chake.

Kauli ya washirikina: 'Hatutakuamini mpaka utuchimbulie,' inafahamisha kuwa wanaamini risala ya binadamu; isipokuwa walitoa sharti la kuwa Mtume awe tajiri: "Na walisema: kwanini hii Qur'an haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii" (43:31) Makusudio ya mtu mkubwa ni Walidi bin Mughira, katika viongozi wa Makka au Urwa bin Masud katika viongozi wa Taif.

Lau ingelikuwa tafsiri kama wanavyosema, basi washirikina wangelikuwa na udhuru katika kupinga kwao utume wa Muhammad (s.a.w.), kwa sababu watakuwa wanafanya lile wanaloliitakidi, na Mwenyezi Mungu amewasifu kwenye Aya nyingi kuwa wanadhihirisha yale waliyoyaficha:

بَلْ بَدَا لَهُم مَّا كَانُوا يُخْفُونَ مِن قَبْلُ ﴿٢٨﴾

"Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani," Juz, 7 (6:28)

"Na wakazikataa kwa dhulma na kujitia uluwa na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo." (27:19).

Kwa ufupi ni kuwa maana sahihi ya Aya ni kwamba washirikina waliposhindwa na hoja ya utume wa Muhammad, walikimbilia ubabaishaji na kujaribu kuwapoteza wajinga wasiokuwa na akili.

Ndio wakasema kama mbinu tu za kuhadaa, kuwa Mwenyezi Mungu hamtumi Mtume binadamu, isipokuwa Malaika tu. Walisema haya wakiwa wanajua kwamba wao ni waongo. Ndio maana Mwenyezi Mungu akasema 'Ispokuwa walisema' na wala hakusema walidhani n.k. Hii inafahamisha kuwa kupinga kwao ni kiasi cha inadi tu ya kauli si ya itikadi.

Sema: Lau ingelikuwa duniani kuna Malaika wanaotembea kwa utulivu, Yaani wanaotembea kama wanadamu basi bila ya shaka tungeliwateremshia Malaika kuwa Mtume wao.

Hekima ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) inataka apeleke Mtume kwa viumbe wake kutokana na jinsi yao. Wakiwa ni watu basi mtume wao atatokana na wao na wakiwa ni Malaika basi watakuwa hivyo hivyo. Kwa sababu jinsia inapendelea zaidi kwenye jinsia yake:

لَقَدْ مَنَّ اللَّـهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ ﴿١٦٤﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu amewaneemesha waumini kwa kuwaletea Mtume miongoni mwao” Juz. 4 (3:164).
Washirikina wanajua hilo, lakini wanafanya vitimbi na hadaa. Umetangulia mfano wake katika Juz.7 (6:9).
Unaweza kuuliza: Jibril ni Malaika naye alikuwa mjumbe wa Mungu kwa Muhammad ambaye ni mtu, imekuwaje? Jibu: baina ya hawa wawili kuna aina fulani ya kukurubiana katika jinsi; kwamba kila mmoja wao ni mjumbe kutoka kwa Mungu.

Sema: Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi. Hakika Yeye anawajua vyema waja wake na anawaona.

Mwenyezi Mungu ni shahidi wa Muhammad kwa miujiza aliyoidhihirisha mikononi mwake, historia inashuhudia heri ya utu iliyopatikana kutokana naye na risala yake inashuhudia kwamba yeye ni rehema kwa viumbe na lolote katika sera ya Muhammad ni hoja tosha ya ukweli wake na utukufu wake.

وَمَن يَهْدِ اللَّـهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ وَمَن يُضْلِلْ فَلَن تَجِدَ لَهُمْ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِهِ وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمْيًا وَبُكْمًا وَصُمًّا مَّأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ كُلَّمَا خَبَتْ زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا ﴿٩٧﴾

97. Na anayeongozwa na Mwenyezi Mungu ndiye aliyeongoka na anayempotoa, basi, hutawapatia walinzi wasiokuwa Yeye. Na tutawakusanya Siku ya Kiyama hali ya kukokotwa juu ya nyuso zao wakiwa ni vipofu na mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahannam. Kila moto ukifanya kuzimika tutazidi kuuchochea uwake kwa nguvu.

ذَٰلِكَ جَزَاؤُهُم بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا عِظَامًا وَرُفَاتًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٩٨﴾

98. Hayo ni malipo yao kwamba wao walizikataa ishara zetu na wakasema: je, tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagika, je tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّـهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَن يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ وَجَعَلَ لَهُمْ أَجَلًا لَّا رَيْبَ فِيهِ فَأَبَى الظَّالِمُونَ إِلَّا كُفُورًا ﴿٩٩﴾

99. Kwani hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi ni Mwenye kuweza kuumba mbingu mfano wao? Na yeye amewawekea muda usio na shaka yoyote, lakini madhalimu hawataki isipokuwa ukafiri.

قُل لَّوْ أَنتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَّأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنفَاقِ وَكَانَ الْإِنسَانُ قَتُورًا ﴿١٠٠﴾

100. Sema, lau mngelikuwa mnamiliki hazina ya rehema ya Mola wangu, basi mngeliizuia kwa kuchelea kuisha. Na mtu ni mchoyo sana.

## ALIYEONGOZWA NA MUNGU

**Aya 97-100**

### MAANA

Na anayeongozwa na Mwenyezi Mungu ndiye aliyeongoka na anayem-potoa, basi, hutawapatia walinzi wasiokuwa Yeye.

Hii ni kumwelezea aliye mwema; yaani anayekuwa hivyo mbele ya Mwenyezi Mungu; na wala sio yule watu wanayesema kuwa ni mwema. Kuna Hadith isemayo: "Dhahiri ni ya watu na batini ni ya Mungu." Katika Nahjulbalagha imeelezwa: "Utajiri na ufukara ni baada ya kuonekana kwa Mungu."

Wafisadi na wapotevu hawana wa kuwanusuru wala kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu. Umetangulia mfano wake katika Juz. 9 (7: 178). Ama adhabu ya wapotevu wanaopoteza, ameiashiria Mwenyezi Mungu kwa kusema:

Na tutawakusanya Siku ya Kiyama hali ya kukokotwa juu ya nyuso zao wakiwa ni vipofu na mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahannam. Kila moto ukifanya kuzimika tutazidi kuuchochea uwake kwa nguvu.

Hili ni fumbo la uchungu wa adhabu na ukali wake kwa yule Mwenye kupinga hisabu na adhabu yake mpaka ajue aliyoyapinga:

كُلَّمَا أَرَادُوا أَن يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّذِي كُنتُم بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢٠﴾

"Na wataambiwa: onjeni adhabu ya moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha" (32:20).

Na hayo ni malipo yao kwamba wao walizikataa ishara zetu pamoja na ufafanuzi wa kutokea ufufuo. Walikanusha na wakapinga si kwa chochote ila ni kwa kuona ni mbali hilo.

Na wakasema: je, tutakapokuwa mifupa na mapande yaliyosagika, je tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

Imekwishatangulia Aya hii neno kwa neno katika Aya ya 49 ya Sura hii.

Kwani hawaoni kwamba Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi ni Mwenye kuweza kuumba mbingu mfano wao? Na yeye amewawekea muda usio na shaka yoyote, lakini makafiri hawataki isipokuwa ukafiri.

Makusudio ya muda hapa ni muda wa ufufuo na kwamba huo utakuwa tu. Wameukana na hali wanaona kuumbwa kwa mbingu na ardhi huku wakikubali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziumba na akazipangilia vizuri kwa uweza wake, lakini wakasema kuwa Mwenyezi Mungu hawezi kuwarudisha tena baada ya kutoweka, kwa vile hilo ni jambo zito.

Ndio Mwenyezi Mungu akawaambia kuwa mwenye kuweza kukifanya kitu bila ya kitu basi ana uweza zaidi kukikusanya kitu hicho baada ya kutawanyika.

Maana ya Aya hii yamekwisha tangulia kwenye Aya nyingi, Angalia Juz.13 (13:5).

Hebu tusome kwa pamoja hoja hizi za kufunga mdomo wa mpinzani wa ufufuo, kwa mfumo usiokuwa na ushabiki; kisha useme: Ole wao wenye kukadhibisha:

"Walisema: Je, tutakapokufa na tukawa mchanga na mifupa ndio tutafufuliwa? Tuliahidiwa haya sisi na baba zetu zamani. Hayakuwa haya ila ni ngano za watu wa kale."

"Sema: Ni ya nani ardhi na mbingu na vilivyomo ndani yake, kama nyinyi mnajua?"

"Watasema ni ya Mwenyezi Mungu."

"Sema: Basi je, hamkumbuki?"

“Sema ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa Arshi kuu?”
“Watasema ni Mwenyezi Mungu.”
“Sema: Basi Je, hamuogopi?”
“Sema: ni nani ambaye ufalme wa kila kitu umo mikononi mwake, naye ndiye alindaye na halindwi, ikiwa mnajua?”
“Watasema ni vya Mwenyezi Mungu”
“Sema: basi vipi mnadanganywa?” 23: (82 – 89).
Huu ni ushahidi wazi kwamba itikadi ya kiislamu iko kwenye misingi ya elimu na uhuru wa akili na rai, Tazama: Juz; 7 (6:4) “Kifungu hakuna udikteta katika ardhi wala mbingu.”

Sema lau mngelikuwa mnamiliki hazina ya rehema ya Mola wangu, basi mngeliizuia kwa kuchelea kuisha.

Rehema ya Mwenyezi Mungu inaenea kwenye kila jambo, kama vile afya, ufahamu, mali na neema nyinginezo, lakini makusudio yake hapa ni kuhusu mali, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t): “Kuhofia kuisha” na ile Aya ya 90 ya Sura hii.

Ubainifu wake ni kuwa Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake awaambie wapenda anasa kuwa nyinyi mlitaka Mwenyezi Mungu awazidishie mali zenu na utajiri wenu kwa kuchimbua mito ardhini, huku akiwa anajua kwamba nyinyi lau mtamiliki hazina ya mbingu na ardhi ambayo haishi, basi mngeendelea na ubahili wenu na uchoyo kwa kuhofia kuisha. Hili linatilia mkazo tuliyosema kwamba wapenda anasa hawafikirii isipokuwa mali.

Na mtu ni mchoyo sana

Katika Juz. 12 (11: 9) tumesema kuwa Qur’an, haikusudii, kwa wasifu huu, kumueleza binadamu alivyo; isipokuwa ni kutafsiri tabia ya binadamu katika badhi ya hali zake. kwa maelezo zaidi rudia huko.

11

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ تِسْعَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ فَاسْأَلْ بَنِي إِسْرَائِيلَ إِذْ جَاءَهُمْ فَقَالَ لَهُ فِرْعَوْنُ إِنِّي لَأَظُنُّكَ
يَا مُوسَىٰ مَسْحُورًا ﴿١٠١﴾

101. Hakika tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. Waulize wana wa Israil; alipowajia na firauni akamwambia: Hakika mimi nakuona wewe umerogwa.

قَالَ لَقَدْ عَلِمْتَ مَا أَنزَلَ هَـٰؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ بَصَائِرَ وَإِنِّي لَأَظُنُّكَ يَا فِرْعَ وْنُ
مَثْبُورًا ﴿١٠٢﴾

102. Akasema: Hakika umekwishajua kuwa hakuziteremsha hizi isipokuwa Mola wa mbingu na Ardhi, kuwa ni dalili. Hakika mimi nakuona, ewe firauni, umeangamia.

فَأَرَادَ أَن يَسْتَفِزَّهُم مِّنَ الْأَرْضِ فَأَغْرَقْنَاهُ وَمَن مَّعَهُ جَمِيعًا ﴿١٠٣﴾

103. Na akataka kuwahamisha katika ardhi, Tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote.

وَقُلْنَا مِن بَعْدِهِ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ اسْكُنُوا الْأَرْضَ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ جِئْنَا بِكُمْ لَفِيفًا ﴿١٠٤﴾

104. Na tukawaambia, baada yake, wana wa Israil: kaeni katika ardhi, Na itakapokuja ahadi ya Akhera tutawaleta nyote pamoja.

## TULIMPA MUSA ISHARA TISA

**Aya 101 – 104**

### MAANA

Hakika tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi.

Yamewishatangulia maelezo, katika Aya kadhaa, kuhusu Musa (a.s) na watu wake na miujiza yake na pia kuhusu Firauni na wakuu wake na utaghuti wake.

Inawezekana kuwa mnasaba wa kutajwa miujiza ya Musa hapa, ni kuwa Mwenyezi Mungu alipotaja mapendekezo ya washirikina kwa Muhammad **(s.a.w.w)**, alifuatishia kuonyesha mapendekzo ya Firauni kwa Musa na matokeo yake yakawa ni balaa kwake; kwamba itatokea hivyo hivyo, lau Mwenyezi Mungu atajibu mapendekezo ya washirikina kwa Muhammad **(s.a.w.w)**.

Kwa sababu wao watayakataa yatakapowajia; sawa na walivyofanya watu wa Firauni na wangeliangamia kama alivyoangamia Firauni. Kwa hiyo kukosa kujibiwa ni heri kwao na Mwenyezi Mungu anajua yanayowafaa waja na yale ya kuwaharibia.

Musa ana ishara na miujiza mingi, ikiwemo ile ya kuifanya risala yake iwe nyepesi; kama vile kuondoka mifundo ya ulimi wake, kuneemeshwa na kufadhilishwa wana wa Israil kwa kutolewa maji katika jiwe, kuteremshiwa manna na salwa au kuhofishwa kwa kufunikwa na mlima. Mingine ni ya kumpa fundishoFirauni na watu wake ili waweze kuamini au malipo ya inadi yao.

Hiyo ndiyo miujiza tisa iliyoashiriwa na Aya. Iliyo dhahiri zaidi ni kugeuka fimbo kuwa nyoka, mkono kuwa mweupe na kuangamizwa makafiri baharini. Ama sita iliyobakia, mitano yake imeashiriwa na Aya hii:

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالدَّمَ آيَاتٍ مُّفَصَّلَاتٍ فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿١٣٣﴾

"Basi tukawapelekea tufani na nzige na chawa na vyura na damu kuwa ishara mbalimbali, lakini wakatakabari na wakawa watu wakosefu" Juz; 9 (7:133)

Na wa sita ni kuangamizwa mali zao: "Na Musa akasema: Mola wetu! Hakika wewe umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali nyingi katika maisha ya dunia. Mola wetu! Hivyo wanawapoteza watu na njia yako.

Mola wetu! Ziangamize mali zao na zitie shida nyoyo zao, Na hawataamini mpaka waione adhabu yenye kuumiza. Akasema Mwenyezi Mungu, maombi yenu yamekubaliwa. Basi muwe na msimamo wala msifuate njia ya wale wasiojua." Juz; 11 (10:88-89).

Waulize wana wa Israil

Maneno yanaelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Makusudio ya wana wa israili ni wale walioamini; kama vile Abdullah bin Salam na maswahiba zake. Lengo la swali hili na jawabu ni kuwadhihirishia mayahudi na wasiokuwa mayahudi ukweli wa Mtume mtukufu kwa kila alilowaletea kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Alipowajia na Firauni akamwambia: Hakika mimi nakuona wewe umerogwa.

Yaani umchawi, kwa maana ya kuwa umepewa elimu ya uchawi, kwa dalili ya Aya nyingine isemayo: "Wakasema wakuu wa watu wa Firauni: Hakika huyu ni mchawi mjuzi." Juz; 9 (7:109). Walisema hivyo baada ya kushuhudia fimbo inageuka kuwa nyoka mkubwa na mkono rangi ya maji ya kunde kuwa mweupe bila ya ubaya.

Akasema; hakika umekwishajua kuwa hakuziteremsha hizi isipokuwa Mola wa mbingu na Ardhi, kuwa ni dalili. Hakika mimi nakuona, ewe firauni, umeangamia.

Makusudio ya 'hizi' ni ishara tisa.

Firauni alipomwambia Musa, mimi nakuona u mchawi, Musa alimjibu kuwa unajua kwa hakika ukweli wa ishara na niliyokuletea na kwamba hizo ni dalili wazi kutoka kwa Mwenyezi Mungu zinazokuonyesha wewe na watu wote kuwa mimi ni mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini wewe unafanya inadi na kiburi kwa ajili ya kupupia cheo chako.

Ikiwa wewe unaniona kuwa mimi ni mchawi basi mimi ninakuona wewe umeangamia; na hayo ni malipo ya kukadhibisha kwako haki na atakayekuwako ataona. Kila mwenye kuipinga haki na akaona uzito kuambiwa basi huyo ni mwanachama wa Firauni na mila yake.

Na akataka kuwahamisha katika ardhi.

Aliyetaka kuwatoa ni Firauni, na waliotakiwa kutolewa ni Musa na watu wake. Maana ni kuwa Firauni alitaka ardhi ya Misri isikaliwe na Wana wa israil kwa kuwaua, kuwachukua mateka na kuwafukuza. Lakini janga likamgeukia yeye, kama inavyokuwa kwa kila taghuti.

Tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote.

Mwenyezi Mungu aliwangamiza baada ya kuwapatia hoja na dalili wazi, lakini wakakataa isipokuwa ukafiri na kupetuka mipaka.

Na tukawaambia, baada yake, wana wa Israil: kaeni katika ardhi.

Ardhi iliwakunjukia wana wa Israil, baada ya kupata amani kwa kuangamia Firauni, Mwenyezi Mungu akawapa hiyari ya kukaaa popote katika nchi. Ilitakikana washukuru Mungu kwa neema hii, lakini wao wakapetuka mipaka na wakafanya uovu:

Wakaabudu ndama badala ya Mwenyezi Mungu, wakasema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumbwa na kwamba Yeye Mwenyezi Mungu ni fukara na wao ni matajiri, wakawaua mitume, wakala haramu na riba, wakaipotoa Tawrat, wakajaribu kumuua Bwana Masih, na kumzulia mama yake uovu na mengineyo aliyoyasajili Mwenyezi Mungu katika Tawrat, Injili na Qur'an na watu wakayasajili katika vitabu vya historia na vya Hadith vya zamani na vya sasa. Uzayuni unatosha kuwa ni ushahidi wa hakika ya kikundi hiki kiovu na kwamba hicho ni shari na balaa kwa ubinadamu.

Na itakapokuja ahadi ya Akhera tutawaleta nyote pamoja.

Maneno hapa wanaambiwa wana wa Israil na akhera ni Siku ya Kiyama, kuletwa pamoja ni mkusanyiko wa wanaotofautiana. Makusudio ni kutoa hadhari na kiaga kwa wale watakokuja katika wana wa Israil kuleteta fitina na ufisadi katika nchi.

Hii ndio dhahiri ya tamko la Aya, Lau ingelikuwa inafaa kufasiri Qur'an kwa maoni yetu, basi tungelisema kuwa neno 'kuletwa pamoja' linaashiria kujumuika mayahudi na uzayuni, kutoka huko na huko, katika ardhi ya Palestina na kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) atawasalitia uovu mkali na itakuwa ni ahadi itakayotimizwa. Usawa ni tuliyoyaelezea katika Aya ya 4 ya sura hii, rudia huko.

وَبِالْحَقِّ أَنزَلْنَاهُ وَبِالْحَقِّ نَزَلَ ۗ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿١٠٥﴾

105. Na kwa haki tumeiteremsha na kwa haki imeteremka. Na hatukukutuma ila uwe mbashiri na muonyaji.

وَقُرْآنًا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ عَلَىٰ مُكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنزِيلًا ﴿١٠٦﴾

106. Na Qur'an tumeigawanya ili uwasomee watu kwa kituo; na tumeiteremsha kidogo kidogo.

قُلْ آمِنُوا بِهِ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا ۚ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا

﴿١٠٧﴾

107. Sema, iaminini au msiiamini. Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa, huanguka kifudifudi wanasujudu.

وَيَقُولُونَ سُبْحَانَ رَبِّنَا إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٠٨﴾

108. Na wanasema: Ametakasika Mola wetu, Hakika ahadi ya Mola wetu lazima itimizwe.

وَيَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿١٠٩﴾

109. Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidishia unyenyekevu.

قُلِ ادْعُوا اللَّـهَ أَوِ ادْعُوا الرَّحْمَـٰنَ ۖ أَيًّا مَّا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلًا ﴿١١٠﴾

110. Sema, mwiteni Mwenyezi Mungu (Allah) au mwiteni Mwingi wa rehema (Rahman), kwa jina lolote mtakalomwita, Yeye ana majina mazuri. Wala usiisome jahara Swala yako wala usiifiche, bali tafuta njia baina ya hizo.

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّـهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ الذُّلِّ ۖ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيرًا ﴿١١١﴾

111. Na sema, sifa njema zote ni za ambaye hakujifanyia mtoto wala hana mshirika katika ufalme, wala hana msaidizi kwa sababu ya udhaifu na mtukuze kwa matukuzo makubwa.

## KWA HAKI TUMEITEREMSHA

**Aya 105 – 111**

### MAANA

Na kwa haki tumeiteremsha na kwa haki imeteremka.

Wafasiri wana kauli nyingi katika jumla mbili hizi; Yenye nguvu zaidi ni ile aliyoisema Tabrasi na Razi. Kwa ufupi wa kauli yao ni kuwa makusudio ya kauli yake Mwenyezi Mungu: Na kwa haki tumeitremsha', ni kwamba Qur'an imedhamini haki na makusudio ya 'Na kwa haki imeteremka' ni kwamba Mwenyezi Mungu kwa kuiteremsha Qur'an alitaka watu waiamini na waitumie. Hilo lilipatikana kwa hakika; ambapo waislamu waliiamini na wakaitumia wale wenye ikhlasi.

Sisi tuko pamoja na Razi na Tabrasi katika kufasiri jumla ya kwanza. Ama jumla ya pili, tuonavyo sisi ni kuwa kila walilokuwa nalo watu kabla ya kuteremshwa Qur'an na watakalokuwa nalo baada ya kuetremshwa, basi Qur'an inalikubali ikiwa ni la haki, kheri na masilahi.

Kwa maneno mengine ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t.) baada ya kusema katika jumla ya kwanza kuwa ameiteremsha Qur'an kwa haki kheri na masilahi, katika jumla ya pili anasema pia Qur'an inakubaliana na kila lililo haki lenye kheri na masilahi wakati wowote litakapokuwa, kabla au baad aya Qur'an.

Kuna Aya zilizo na maana ya tafsiri hii; kama vile:

وَأَمَّا مَا يَنفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ ۚ كَذَٰلِكَ يَضْرِبُ اللَّـهُ الْأَمْثَالَ ﴿١٧﴾

"Ama kinachowafaa watu hukaa kwenye ardhi" Juz.13 (13:17)

يُرِيدُ اللَّـهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ ﴿١٨٥﴾

"Mwenyezi Mungu anawatakia yaliyo mepesi wala hawatakii yaliyo mazito" Juz;2 (2:185).

Imam Ja'far As-swadiq (a.s) naye amesema: **"Kila lenye masilahi kwa watu kwa namna moja au nyingine, basi linajuzu."**

Na hatukukutuma ila uwe mbashiri na muonyaji.

Umbashirie Pepo mtiifu na umonye na moto muasi. Baada ya hapo anayetaka aamini na anayetaka na akufuru.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ مَن يَضِلُّ عَن سَبِيلِهِ ۖ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١١٧﴾

“Hakika Mola wako anawajua vyema wanaopotea njia yake na anawajua sana wanaoongoka,” Juz;8 (6:117).

## JE, QUR’ANI ILISHUKA KIDOGO KIDOGO?

Na Qur’an tumeigawanya ili uwasomee watu kwa kituo.

Qur’an haikuteremka kwa Muhammad kwa mpigo; bali iliteremka kidogo kidogo, ikifiuatana na mara nyingine ikichelewa kulingana na masilahi na matukio ambayo huzuka mara kwa mara. Ama kauli yake Mwenyezi Mungu:

إِنَّا أَنزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ﴿١﴾

“Hakika tumeitermsha Qur’an katika laylatul-qadr (usiku wa heshima),” (97:1).

Maana yake ni kuwa ilianza kuteremshwa usiku huo, kisha ikaendelea hadi kufa Mtume **(s.a.w.w)** na kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kushuka kwake ilikuwa ni miaka ishirini na tatu.

Mwenyezi Mungu amebainisha lengo la kufanya hivyo kwa kusema: ‘ili uwasomee watu kwa kituo;’ yaani kutoa muda ili iwe rahisi kuifahamu na kuihifadhi.

Aya hii ni dalili wazi ya kumkosoa anayesema kuwa Qur’an imeshuka kwa mara moja yote na mtume akaifikisha kidogo kidogo. Mwenyezi Mungu amemrudi mwenye kusema hivi kwa kauli yake: “Na wakasema wale waliokufuru: kwa nini hakuteremshiwa Qur’an kwa jumla moja?” (25: 32) Yaani moyo wako uweze kuwa na nguvu kuweza kufahamu maana ya Qur’an na siri zake.

Zaidi ya hayo kuna Aya kadhaa zinazosimulia visa na matukio yaliyojitokeza upya au kubainisha hukumu yake; kama vile kisa cha Badr, Uhud, Ahzab na Hunayn. Pia kisa cha Wakiristo wa Najrani na mayahudi wa Madina. Vile vile tukio la wake wa Mtume, mwanamke aliyemjadili Mtume kuhusu mumewe na mengineyo.

Amesema Sheikh Mufid: “Qur’an imeshuka kwa sababu na matukio kwa hali baada ya hali. Hilo linafahmika kutokana na dhahiri ya Qur’an, Hadith mutawatr na kongamano la maulama.”

Na tumeitermsha kidogo kidogo.

Jumla hii ni tafsiri na ubainifu wa yaliyo kabla yake.

Sema: iaminini au msiamini. Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa, huanguka kifudifudi wanasujudu. Na wanasema: Ametakasika Mola wetu, Hakika ahadi ya Mola wetu lazima itimizwe. Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidishia unyenyekevu.

Kabla yake, ni kabla ya Qur’an. Wanaoambiwa ni washirikina ambao walimwekea masharti Muhammad **(s.a.w.w)** ya kumwamini; kama ilivyoelezwa katika Aya ya 9 ya Sura hii. Kuanguka kifudifudi ni kusujudu kwa uso. Kumetajwa kusujudu mara mbili, kwa sababu kwa kwanza ni kwa ajili ya kumwadhimisha Mwenyezi Mungu na kwa pili ni kwa kuathrika na Qur’an katika nafsi zao.

Wale ambao wamepewa elimu kabla ya Qur’an ni wale waloiangalia haki katika watu wa Kitabu ambao walimwamini Muhammad **(s.a.w.w)** na wenye maumbile safi, kama wale tutakaowadokeza katika kifungu kinachofuatia.

## WANYOOFU

Mnyoofu ni yule aliyeacha batili na kufuata haki na njia yenye kunyooka. Wakati wa Jahiliya kulikuwa na watu waliopetuka mazingira yao, na kwa mamubile yao safi waliweza kutambua kwamba kuna muumba mmoja mwenye uwezo wa ulimwengu huu na kwamba baada ya mauti kuna ufufuo, hisabu, adhabu na thawabu.

Vile vile kwamba kuabudu masanamu ni ujinga na upotevu. Kuna baadhi ya shairi zao katika kitabu Al-aghani Juzuu ya 3 na Sirat ibn Hisham, Juzuu ya 1. Chapa ya mwak 1936:

- Je, ni Mungu mmoja au elfu miungu?
- Ni dini iliyokioja iliyogawanyika mafungu
- Lakini namuabudi Mola wangu Rahamani
- Anisamehe zangu dhambi Mola ghafuri manani
- Tawaona watu wema makazi yao Peponi
- Na makafiri madhalima kwenye sairi Motoni

Ibn Hisham anasema katika Juzuu ya 1 ya As-siratun-nabawiyya: "Walikusanyika makuraishi katika Idd yao ya masanamu waliyokuwa wakiyaadhimisha, wakajitoa watu wane ambao ni: Waraqa bin Nawfal, Abdallah bin Jahsh, Uthman bin Alhuwayrith na Zayd bin Amr. Wakaambiana: Wallah hawa watu wenu hawana chochote, wameikosea dini ya baba yao Ibrahim! Nini haya mawe tunayozungukia, hayasikii, hayaoni, hayadhuru wala hayanufaishi!

Zayd hakuingia kwenye uyahudi wala unaswara (ukiristo), Aliacha dini ya watu wake kwa kujiepusha na masanamu, mfu, damu na dhabihu zilizokuwa zikitolewa kwa masanamu. Akakataza kuwaua watoto wa kike na akawa anamwambia baba yake: "Usimuue mimi nitamgharimia malezi yake."

Alikuwa akijasiri kuwaambia watu wake na kuwakosoa huku akiwaambia: "Mimi ninamwabudu Mola wa Ibrahim. Ewe Mola wangu! Lau ningejua namna inayopendeza zaidi ya kukuabudu ningeliifanya; lakini siiju, Kisha anasujudi kwenye kiganja chake.

Zayd aliendela kuwasafihi maquraishi na ibada yao. Walipoona ni hatari walimtaka ami yake Khattwab, baba wa Umar bin, Alkhattab amzuie na amkataze, naye akamkataza. Lakini Zayd bado aliendelea na mwito wake. Al-Khattab akawa anawatuma vijana wahuni wa Kikuraishi, akiwemo mtoto wake Umar, kumzuia asiingie Makka, Zaidi akawa anapenye Kisiri.

Walipofahamu walimwambia al-Khattab na wakawa wanamfukuza na kumwudhi kwa sababu ya kuogopa kwao asije akawavutia watu kwenye dini yake, Baadaye Zaid akatoka kutafuta dini ya Ibrahim (a.s). Akawa anahangaika huku na huko katika nchi mbalimbali. Hata hivyo alipokanyaga nchi ya Lakhm, alishambuliwa na kuuawa. Rafiki yake Waraqa alimlilia na kumtungia mashairi haya:

- Hakika bin Amri meongozwa kwa wema
- Mejiepusha na tanuri ya moto unaochoma
- Me mwabudu adhimu Mola aso mithili
- Ukaiacha mizimu ya matwaghuti jahili
- Rehema za Mola wake kiumbe humfikia
- Hata chini ajizike bonde sabini kungia

Zaidi aliuawa kabla ya kutumwa Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**, lakini mtoto wake alimwamini Mtume **(s.a.w.w)** Yeye pamoja Umar bin al-Khattab, ambaye alikuwa ni binamu yake, walimwendea Mtume na kumwuliza: Tunaweza kumuomba Mwenyezi Mungu amsamehe Zaid bin Amr?" Mtume alijibu: "Ndiyo. Yeye atafufuliwa kama mwakilishi pekee wa jamaa zake."

Abdallah bin Jahsh, alibakia mpaka ukaja Uislamu, akasilimu na akahama yeye na mkewe, Ummu Habiba bint Abi Sufyan, kwenda Habasha (Ethiopia), akafia huko baada ya kurtadi kwa kuingia kwenye dini ya unaswara (ukiristo) ... Baadae Mtume akamuo Ummu Habiba.

Uthman bin Huwayrith, alikwenda kwa Kaizari mfalme wa Roma na akawa Mnaswara, huko alipewa cheo kikubwa na akafa Sham. Waraqa aliingia dini ya unaswara (ukristo) na akasoma vitabu vitakatifu vya dini hiyo mpaka akavifahamu barabara. Aliishi Makka, kama mtawa, akiwakataza watu wake kuabudu masanamu.

Warqa alikuwa ni binamu wa Khadija, mke wa Mtume **(s.a.w.w)**. Uliposhuka wahyi kwa mtume alikwenda naye kwa binamu yake huyo. Akamuuliza, ewe mwana wa ndugu yangu, unaona nini? Mtume alipomwambia akasema: "Huyo ndiye Malaika Mkuu amabye aliwashukia Musa, Natamani ningekuwa kijana, natamani niwe hai wakati watu wako watakapokutoa. Mtume akasema: Hivi watanitoa? Akasema ndio! Hakuna mtu yeyote kabisa aliyekuja na mfano wa jambo lako ila hufanyiwa uadui. Kama nikiwahi siku hiyo nitakusaidia sana!

Waraqa alitamka kwa wahyi wa umbile lake safi, "Ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu" Kila mtu atakayerejea kwenye umbile lake hili atamwamini Muhammd **(s.a.w.w)** na atamsaidia kwa sababu "Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu, Hiyo ndiyo dini iliyo sawasawa, Lakini watu wengi hawajui." (30:30).

Sema, mwiteni Mwenyezi Mungu (Allah) au mwiteni Mwingi wa rehema (Rahman), kwa jina lolote mtakalomwita, Yeye ana majina mazuri.

Washirikina walikuwa na masanamu mbalimbali, wakiyaita kwa majina ambayo Mwenyezi Mungu hakuyateremshia dalii yoyote.

Katika majina hayo hakukuwa na jina la Rahman. Kwa hiyo Mtume alipowalingania kumwabudu Rahman ndio wakasema, ni nani huyo Rahman? "Na wanapoambiwa msujudieni mwingi wa rehema (Rahman) wao husema: Ni nani huyo mwingi wa rehma? Je,tumsujudie unayetuamrisha wewe?" (25:60) Yaani ni wasifu gani huu ambao hauna athari yoyote kwa waungu wetu?

Kauli yake Mwenyezi Mungu: Sema, mwiteni Mwenyezi Mungu (Allah) au mwiteni Mwingi wa rehema (Rahman) ni jawabu tosha la upinzani wao.

Kwa sababu maana yake ni kwamba majina na matamshi ni nyenzo tu ya ibara. La kuzingatia ni yule anayeitwa. Mwiteni mtakavyo katika majina yake, yote ni mazuri; Kwa sababu yanaleta ibara ya maana nzuri nayo yako sawasawa katika uzuri.

وَلِلَّـهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ﴿١٨٠﴾

"Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri," Juz; 9 (7:180).

Kwenye Juzuu hiyo ya 9, tumefafanua zaidi katika kifungu cha 'Je, majina ya Mwenyezi Mungu ni hayo hayo au yana kiasi.'

Wala usiisome jahara Swala yako wala usiifiche, bali tafuta njia baina ya hizo.

Makusudio ya jahara kwenye Swala ni kusoma kwa sauti kubwa na kuficha ni kusoma kwa sauti ndogo. Imam Jafar Asswadiq (a.s) anasema katika kufasiri Aya hii: "Jahara ni kuinua sauti na kuficha ni kiasi ambacho masikio yako hayasikii. Na soma kisomo kilicho baina yake"

Na sema: sifa njema zote ni za ambaye hakujifanyia mtoto wala hana mshirika katika ufalme, wala hana msaidizi kwa sababu ya udhaifu, na mtukuze kwa matukuzo makubwa.

Tunamuhimidi Mwenyezi Mungu kwa utukufu wa hisani yake na ukuu wa buruhani yake. Tunamuepusha na kuwa na mtoto kwa vile anajitosha na kila kitu, si muhitaji; na kwa kuwa mtoto anafanana na baba yake na kumrithi na Yeye hana wa kufanana naye wala wa kumrithi.

Tunamwepusha na mshirika kwa vile hiyo ni dalili ya kushindwa:

وَمَا كَانَ اللَّـهُ لِيُعْجِزَهُ مِن شَيْءٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا ﴿٤٤﴾

"Hakuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushindwa na chochote mbinguni wala ardhini; Hakika Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uweza." (35:44).

Kila mwenye nguvu mbele yake ni dhaifu na kila mwenye utukufu kwake ni dhalili; ndio maana inakuwa Mwenyezi Mungu ni mkubwa zaidi na Mwenye shani kiasi wasichoweza kusifu wanaosifu na kutekeleza haki yake wenye kushukuru.

## MWISHO WA SURA YA KUMI NA SABA

12

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

Sura Ya Kumi Na Nane: Surat Al-Kahf

Imeshuka Makka isipokuwa Aya moja tu; kama ilivyoelezwa katika Majmaul-bayan. Ina Aya 111

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu

الْحَمْدُ لِلَّـهِ الَّذِي أَنزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَل لَّهُ عِوَجًا ﴿١﴾

1. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia mja wake Kitabu wala hakukifanya kombo.

قَيِّمًا لِّيُنذِرَ بَأْسًا شَدِيدًا مِّن لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا ﴿٢﴾

2. Kimenyooka ili kitoe onyo kutoka kwake na kiwabashirie waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri.

مَّاكِثِينَ فِيهِ أَبَدًا ﴿٣﴾

3. Wakae humo milele.

وَيُنذِرَ الَّذِينَ قَالُوا اتَّخَذَ اللَّـهُ وَلَدًا ﴿٤﴾

4. Na kiwaonye wale wanaosema Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto.

مَّا لَهُم بِهِ مِنْ عِلْمٍ وَلَا لِآبَائِهِمْ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ إِن يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا ﴿٥﴾

5. Hawana ujuzi wa hili wala baba zao. Ni neno kuu litakalo vinywani mwao, hawasemi ila uongo tu.

فَلَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ عَلَىٰ آثَارِهِمْ إِن لَّمْ يُؤْمِنُوا بِهَـٰذَا الْحَدِيثِ أَسَفًا ﴿٦﴾

6. Huenda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao ikiwa hawataamini mazungumzo haya.

إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ﴿٧﴾

7. Hakika tumevifanya vilivyo katika ardhi kuwa ni pambo lake ili tumjaribu ni nani kati yao mwenye vitendo vizuri zaidi.

وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا جُرُزًا ﴿٨﴾

8. Hakika sisi tutavifanya vilivyo juu yake kuwa nchi iliyo kame.

## AMEMTEREMSHIA KITABU MJA WAKE

**Aya 1 – 8**

### MAANA

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia mja wake- Muhammad- Kitabu wala hakukifanya kombo, kimenyooka ili kitoe onyo kutoka kwake – Yeye Mungu - na kiwabashirie waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri; wakae humo milele.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameiitaja Qur'an katika Aya zake kadhaa kwa sifa za haki uongozi na nuru. Hapa ameiita kwa sifa za msimamo na kutokuwa

kombo na kwamba inambashiria mwema kupata thawabu na neema ya milele na kuwaonya wafisadi kupata adhabu na moto wa milele.
Lengo la yote hayo ni kubainisha kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu amiteremsha Qur'an ili twende na mwongozo wake, sio tuhifadhi Aya zake na matamko yake na kusoma tajwid nzuri na tafsiri tu; kama tulivyo.
Mtume **(s.a.w.w)** alisemana sisi ndio tulikuwa tunaambiwa - "Utakuja wakati kwa watu, dini haitabakia isipokuwa maandishi yake, wala Qur'an isipokuwa darasa yake" Ninaapa kuwa kila ninaposoma makemeo haya kutoka Mtume wa rehema, huwa manywele yananisismka.
Ni makemeo gani yanayotisha kuliko kua miongoni mwa waliokusudiwa na wasifu huu? Sisi hatuna imani isipokuwa jina, wala uislamu isipokuwa maandishi pia hatuna Qur'an isipokuwa kuisoma tu.
Walitia ila Qur'an walioitia na wakaipinga walioipinga tangu mwanzo. Sisi tukaimaini, lakini tunahalifu hukumu zake na mafundisho yake waziwazi. Tofauti yetu sisi na wanaoipinga ni kama ile tofauti baina ya anayesema: Mimi sioni hii kuwa ni haki, lau ningeliijua ni haki basi ningeliifuata na yule asemaye: Bila shaka mimi ninakubali kuwa hii ni haki, lakini sina ulazima nayo wala siiheshimu.

Na kiwaonye wale wanaosema Mwenyezi Mungu amejifanyia motto; Hawana ujuzi wa hili wala baba zao.

Maneno haya yanaungana na ya mwanzo: 'ili kitoe onyo' onyo la kwanza ni kwa kila mwenye kuasi na kustahiki adhabu na onyo la pili linahusu aliyemnasibisha Mungu kuwa ana mtoto. Ametakata Mwenyezi Mungu na hayo kabisa.
Mara nyingi maungano ya mahsusi kwenye ujumla yanafahamisha kuzidi huyo aliye mahasusi; Mfano kuunganisha Jibril na Malaika au kuanganisha waasi na wale wanaosema Mwenyezi Mungu ana mtoto. Kwa sababu kusema kuwa Mwenyezi Mungu ana mtoto ni uasi zaidi.
Razi anasema kuwa waliosema Mungu ana mtoto ni makundi matatu: "Kundi la kwanza ni makafiri wa kiarabu waliosema kuwa Malaika ni mabinti wa Mungu. Kundi la pili ni manaswara (wakiristo) waliosema kuwa Masih ni mwana wa Mungu. Kundi la tatu ni mayahudi waliosema kuwa Uzayr ni mtoto wa Mungu."
Makusudio ya kusema: 'Hawana ujuzi wa hili' ni wao hawategemei dalili yoyote ya hili; bali dalili iko kinyume. Ama kusema wala baba zao ni kusisitiza shutuma tu; kama kusema: Ni mshenzi mtoto wa mshenzi au ni maluuni mtoto wa maluuni.

Ni neno kuu litakalo vinywani mwao, hawasemi ila uongo tu.

Hakuna kitu kikubwa kuliko uongo, Uwongo mkubwa zaidi ni uongo juu ya Mwenyezi Mungu na kunasibisha uhalali na uharamu kwake bila ya dalili. Na mkubwa kuliko yote ni kumnasibishia mtoto.

Huenda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao ikiwa hawataamini mazungumzo haya.

Makusudio ya mazungumzo hapa ni Qur'an, kwa mafikiano ya wote. Kuisifu Qur'an kuwa ni mazungumzo ni dalili ya kuvunja kauli ya wale wasemao kuwa Qur'an ni ya tangu zama.
Hakuna mwenye shaka kuwa Mtume anamtakia heri kila mtu bila ya kubagua; kama vile wewe uanvyomtakia heri mtoto wako na mimi

ninavyomtakia heri mtoto wangu. Mtume alikuwa akihuzunika na kusononeka sana pindi mtu anapofuata njia ya upotevu na maangamizi.

Katika Aya hii Mwenyezi Mungu anamkataza Mtume wake mtukufu kuwa asijitie simanzi, akajiangamiza bure kwa ajili ya wanaopinga uongofu na kufuata haki. Akamwambia usihuzunike:

إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم ﴿٢٦﴾

"Hakika ni kwetu sisi marejeo yao na hakika ni juu yetu hisabu yao." (88:25-26).

Hakika tumevifanya vilivyo katika ardhi kuwa ni pambo lake ili tumjaribu ni nani kati yao mwenye vitendo vizuri zaidi.

Vipambo hapa vinakusanya cheo mali na watoto na kila lile wanalokufia watu na kuvurugana kwa ajili yake. Ghururi hizi ndizo zinazomtambulisha mwema na muovu.

Mwenye kukinai na fungu lake na akaishi kwa jasho lake basi huyo ni mwema aliye karimu.

Na mwenye kujaribu kufanya ulanguzi na kuishi kwa jasho la wengine; hata kama ni kwa kuanzisha vita na kuleta fitna, basi huyo ni muovu mwenye dhambi.

Maana ya majribio ya Mwenyezi Mungu kwa watu katika vipambo vya ardhi ni kuzidhihirisha sababu zake na vitendo vyao ambavyo vitastahiki thawabu au adhabu. Tumezungumzia hilo kwa ufafanuzi Juz. 7 (5:94) kifungu cha 'Maana ya kujaribu kwa Mwenyezi Mungu'.

Hakika sisi tutavifanya vilivyo juu yake kuwa nchi iliyo kame.

Juu yake ni juu ya ardhi; Yaani kila kilicho juu ya ardhi kitatoweka ibaki tupu. Mwema ni yule atakyemtii Mwenyezi Mungu na muovu ni yule atakayetii hawaa yake.

أَمْ حَسِبْتَ أَنَّ أَصْحَابَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿٩﴾

9. Kwani unadhani kwamba watu wa pango na maandishi walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara zetu?

إِذْ أَوَى الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

10. Pale vijana walipokimbilia kwenye pango wakasema: Mola wetu! Tupe rehema itokayo kwako na tutengenezee uongofu katika jambo letu.

فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿١١﴾

11. Basi tukayaziba masikio yao pangoni kwa miaka kadhaa.

ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الْحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُوا أَمَدًا ﴿١٢﴾

12. Kisha tukawazindua ili tujue ni lipi kati ya makundi mawili lililohisabu sawa muda waliokaa.

## WATU WA PANGO

**Aya 9 – 12**

### UTANGULIZI

Tutafisiri Aya zinazofungamana na watu wa pango (As-habulkahf) kutokana na dhahiri ya zinavyofahamisha Aya au kutokana na dalili ya mazingira; kwa mfano kusema kiulize kijiji kwa maana ya waulize watu wa kijiji. Tutaachana na rejea au ngano nyenginezo. Kwani tumesema mara nyingi

kwamba matukio ya historia na mfano wake hayathibiti ila kwa nukuu ya Qur'an au kwa Hadith iliyopokewa kwa njia nyingi (Mutawatir) Na kwamba Hadith iliyopokewa kwa njia moja (Ahad) si kitu, hata kama yakisihi mategemezi yake; isipokuwa katika hukumu ya sharia.

**MAANA**

Kwani unadhani kwamba watu wa pango na maandishi walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara zetu?

Makusudio ya maandishi hapa ni ubao ulioandikwa majina ya watu wa pango. La kushangaza ni kauli ya anayesema kuwa neno raqim, tuliolifasiri kwa maana ya maandishi, ni jina la mbwa wao; na hali inajulikana na ni maarufu kuwa jina la mbwa wao ni Qitmir.

Vyovyote iwavyo ni kuwa kisa cha watu wa pango kilielezwa katika vitabu vya kale na waliokisoma au kukisikia wakashangaa kuwa itakuwaje watu walale usingizi mrefu wa miaka kiasi hicho na wabaki bila ya chakula?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamwambia kila anayeshangazwa na kisa hiki kuwa usistaajabu na hayo, kila ishara ya Mwenyezi Mungu ni ya ajabu. Yule aliyewafanya watu wa pango ndiye yuleyule aliyeufanya ulimwengu na vilivyomo. Kwa hiyo kwake kuwabakisha vijana usingizini kwa mda mrefu kisha kuwaamsha ni jambo rahisi sana, lakini watu wengi hawajui.

Pale vijana walipokimbilia kwenye pango wakasema: Mola wetu! Tupe rehema itokayo kwako na tutengenezee uongofu katika jambo letu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaishria katika Aya hii na nyingine mbili zinazofuatia kuhusu kisa cha watu wa pango kwa ujumla, kisha anaanza kufafanua. Katika Aya hii tuliyonayo anasema kuwa hapo zamani za kale kulikuwa na vijana walioacha kila kitu katika maisha haya na wakakimbilia pangoni; wakamtaka Mwenyezi Mungu awahurumie na awatengenezee mambo yao wakiwa pangoni.

Hakudokeza Mwenyezi Mungu, katika Aya, hii sababu iliyofanya vijana hao waache kila kitu na kujiingiza pangoni, huku wakimtaka Mwenyezi Mungu awaangalilie mambo yao. Tunavyofahamu, kutokana na tafsiri ya mazingira na inavyoashiria Aya inayofuatia, ni kuwa vijana waliongozwa na maumbile yao salama kuwa watu wao wako katika upotevu wa kuabudu masanamu na kwamba wao walikataa kuabudu yale wanayoaabudu wazazi wao.

Kwa hiyo kama kawaida ya wenye siasa kali walitaka kwaua vijana au kuwafitini na dini yao. Vijana walipokosa njia zote waliamua kukimbilia pangoni na kumwambia Mwenyezi Mungu kuwa tumeudhiwa kiasi hiki unachoona nasi tunahitaji sana msaada wako na huruma zako. tunaomba msaada kwako wewe tu, si kwa mwengine.

Basi tukayaziba masikio yao pangoni kwa miaka kadhaa.

Yaani tuliwalaza usingizi ambao hawawezi kusikia chochote kwa muda wa miaka kadhaa, Itaelezwa idadi ya miaka hiyo kwenye Aya ya 25.

Kisha tukawazindua yaani tuliwaamsha ili tujue ni lipi kati ya makundi mawili lililohisabu sawa muda waliokaa.

Watu walijua kisa cha watu wa pango wakiwa bado kwenye usingizi wao. Habari zikaenea na watu wakatofautiana katika muda wa kukaa kwao. Kuna waliosema muda mchache na waliosema mwingi. Mwenyezi Mungu akawainua watu wa pango. Ili makundi mawili yajue muda waliokaa

waweze kuamini awazidishie imani yao kuhusu uweza wa Mwenyezi Mungu wa kuwafufua wafu. Kusema kwake Mwenyezi Mungu “ili tujue’ maana yake ni ili idhihiri elimu yetu kwa watu kiasi cha muda waliokaaa. Umepita mfano wake katika Juz 4. (3:140).

**Unaweza kuuliza**: Watu walijuaje muda wao na hali wenyewe walipoamka hata hawakuujua; bali walianza kuulizana, wengine wakasema tumekaa siku moja tu au nusu siku?

**Jibu**: Watu walijua muda wao kutokana na pesa walizokuwa nazo. Mmoja wao alikwenda mjini kununua chakula na watu wa mji walipoona ile pesa walijua ilikuwa ni wakati wa mmoja wa wafalme waliopita. Utakuja ufafanuzi wake kwenye Aya 19.

نَّحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ ۚ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾

13. Sisi tunakusimulia habari zao kwa haki. Hakika hao ni vijana waliomwamini Mola wao na akawazidisha uongofu.

وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ لَن نَّدْعُوَ مِن دُونِهِ إِلَـٰهًا ۖ لَّقَدْ قُلْنَا إِذًا شَطَطًا ﴿١٤﴾

14. Na tukazitia nguvu nyoyo zao, waliposimama, wakasema: Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi, Hatutamuomba Mungu mwingine badala yake, Hakika tutakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka.

هَـٰؤُلَاءِ قَوْمُنَا اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ آلِهَةً ۖ لَّوْلَا يَأْتُونَ عَلَيْهِم بِسُلْطَانٍ بَيِّنٍ ۖ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّـهِ كَذِبًا ﴿١٥﴾

15. Hawa watu wetu wamefanya waungu badala yake; Kwa nini hawawaletei dalili bayana? Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo?

وَإِذِ اعْتَزَلْتُمُوهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّـهَ فَأْوُوا إِلَى الْكَهْفِ يَنشُرْ لَكُمْ رَبُّكُم مِّن رَّحْمَتِهِ وَيُهَيِّئْ لَكُم مِّنْ أَمْرِكُم مِّرْفَقًا ﴿١٦﴾

16. Na mkijitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Mwenyezi mungu, basi kimbilieni pangoni, atawafungulia Mola wenu rehema yake na atawafanyia wepesi mambo yenu.

وَتَرَى الشَّمْسَ إِذَا طَلَعَت تَّزَاوَرُ عَن كَهْفِهِمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَإِذَا غَرَبَت تَّقْرِضُهُمْ ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِي فَجْوَةٍ مِّنْهُ ۚ ذَٰلِكَ مِنْ آيَاتِ اللَّـهِ ۗ مَن يَهْدِ اللَّـهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۖ وَمَن يُضْلِلْ فَلَن تَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُّرْشِدًا ﴿١٧﴾

17. Na unaliona jua linapochomoza linaelemea kuumeni mwao mbali na pango lao; na lipokuchwa linawahepa kushotoni na wao wamo katika uwazi wake. Hayo ni katika ishara zake. Ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoza basi yeye ndiye aliyeongoka, na anayempoteza hutampatia mlinzi (wala) mwongozi.

وَتَحْسَبُهُمْ أَيْقَاظًا وَهُمْ رُقُودٌ ۚ وَنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَذَاتَ الشِّمَالِ ۖ وَكَلْبُهُم بَاسِطٌ ذِرَاعَيْهِ بِالْوَصِيدِ ۚ لَوِ اطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا وَلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُعْبًا ﴿١٨﴾

18. Utawadhania wako macho na hali wamelala, na tunawageuza kuume na kushoto na mbwa wao amenyoosha miguu yake ya mbele kizingitini lau ungeliwatokea bila shaka ungeligeuka kuwakimbia na ungelijazwa hofu.

## HABARI ZAO ZA KWELI

**Aya 13-18**

### MAANA

Sisi tunakusimulia habari zao kwa haki.

Kabla ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, watu walikuwa wakielezana habari za kisa cha watu wa pango. Kikaandikwa kwenye vitabu na pia kwenye mashairi. Miongoni mwa kaswida ya Umayya bin Abu Swalat:

Hakuna isipokuwa raqimu aliye jirani watu na mbwa wao wamelala pangoni.

Mtume alikuwa akiwataka watu wamsomee shairi la Bin Abu swalat, Basi husikilza kisha anasema, huyu mtu aliamini kwa ulimi wake na akakufuru kwa moyo wake.

Watu walitunga vigano kuhusu watu wa pango; kama walivyotunga kwa watu wengine waliopita. Ndio maana Mwenyezi Mungu akamwabia Mtume wake: 'Sisi tunakusimulia habari zao kwa haki' amabazo hazina shaka. Na ni nani aliye mkweli zaidi wa mazungumzo kumshinda Mwenyezi Mungu?

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuelezea kisa chao kwa ujumla katika Aya iliyotangulia, sasa anaanza kukichambua katika Aya zinazofuatia.

Kisa hiki kinagawanyika mafungu mane: Kwanza, kuelekea watu wa pango kwa Mwenyezi Mungu. Pili, hali yao na ya watu wao pamoja na kukimbia kwao, Tatu, kuamka kwao kutoka kwenye usingizi wao mazito. Nne, kufa kwao na kujengewa. Aya tuliyo nayo imechukua sehemu ya kwanza na ya pili na Aya zinazofuatia zimechukua sehemu mbili za mwisho.

### SEHEMU YA KWANZA

Hakika hao ni vijana waliomwamini Mola wao na akawazidisha uongofu na tukazitia nguvu nyoyo zao.

Katika vijana wako wale ambao wamekomaa kiakili na kifikra; sawa na walivyokomaa kimwili. Aina hii ya vijana, ingawaje ni nadra kupatikana, lakini wapo, miongoni mwao ni watu wa pango. Walikuwa wakiishi katika jamii iliyojaa ufisadi na kuabudu masanamu, lakini wao walikataa na wakajiongoza kwa muwongozo wa usafi wa maumbile yao, Wakajiuliza, vipi mawe yanaweza kuwa miungu? Vipi wapenda anasa wanahodhi utajiri na nguvu na kuzitumia kwa wanyonge?

Shaka hii na maswali haya yaliwapeleka vijana hao kwenye itikadi ya tawhid na ufufuo. Mwenyezi Mungu alipoona ukweli wao wa nia na ikhlasi yao, aliwapa uthabiti katika imani yao na busara katika mambo yao.

Waliposimama.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakubainisha walisimama wapi; Kwa hiyo wafasiri wametofautiana, Kuna waliosema kuwa walisimama mbele ya mfalme wao Decianus aliyejifanya jabari, Wengine wamesema kuwa walisimama kutoka usingizini.

Sio mbali kuwa makusudio ya kusimama kwao ni kutoka kwao kwenye ada ya watu wao na kuasi ushirikina na ufisadi. Hii ndio nembo ya mapinduzi yao.

Wakasema: Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi, Hatutamuomba Mungu mwingine badala yake, Hakika tutakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka. Hawa watu wetu wamefanya waungu badala yake, Kwa nini hawawaletei dalili bayana? Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uongo?

Vijana waliamini Mungu mmoja aliye peke yake, Wakatangaza imani yao kwa watu na wakasema kuwa mataghuti katika watu wao wanamzulia Mwenyezi Mungu uongo na akili zao pia; kwa sababu wameyapa masanamu sifa ya Mungu huku wakijua kuwa hayadhuru wala kunufaisha. Wanawazuga wapumbavu kwamba hayo masanamu ndiyo yaliyowachgua wao na kuwapa nguvu juu ya watu. Na kwamba atakayewakhalifu malipo yake ni kuadhibiwa na kuuawa.

Ni kwa madai haya ndio mataghuti walitaka kuwauwa vijana hao, si kwa lolote ila ni kwa kuwa wao wamemwamini Mwenyezi Mungu na kuayakana masanamu kwa kuwaweka juu mataghuti na kuwakandamiza wanyonge.

Nilizinduka wakati nikiandika maneno haya, kwenye tafsiri ya mfano hai wa kushangaza uliojitokeza katika miji yetu. Nao ni hili jeshi kubwa la masheikh wenye vilemba ambao hawana usheikh hata chembe. Nimegundua kuwa kuna mkono mchafu unaofanya kazi kwa siri. Wanatenga mali za kuwalipa vibaraka na za kuwaingiza kwenye safu ya maulama na kuwavisha vilemba. Wanafanya hivyo kwa ajili ya kulinda masilahi ya mataghuti na wanyonyaji kwa jina la dini; sawa na walivyoyapa masananamu sifa ya Mungu ili wawambie watu mazuzu kuwa hayo masanamu ndiyo yaliyowateua wao kuwa viongozi wao na yakawapa wao mali na kuwanyima wanyonge.

## SEHEMU YA PILI

Na mkijitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Mwenyezi mungu, basi kimbilieni pangoni, atawafungulia Mola wenu rehema yake na atawafanyia wepesi mambo yenu.

Mataghuti waliwabana vijana waumini na wakajaribu kuwatia mtihani na dini yao. Wakaambiana kuwa hatutapona na watu madhalimu isipokuwa tuwakimbie wao na yale wanayoyaabudu na kuyafanya.

Baada ya kubadilishana mawazo na kushauriana waliafikiana wakimbilie Pangoni, Kwani walikuwa hawana pengine zaidi ya hapo. Wakaingia Pangoni na wakamwachia Mungu jambo lao; hata kama watakufa kwa njaa na kiu.

Hivi ndivyo anavyokuwa mumin wa kweli, anabakia na imani yake akiitekeleza kwa hamasa na uthabiti bila ya kujali tatizo litakalomtokea. Mtu akifikia hali hii, basi Mwenyezi Mungu anakuwa pamoja naye popote alipo na atampa faraja haraka sana; hata kama wa mbinguni na ardhini watamkalia vibaya; kama ilivyokuwa kwa watu wa pango, pale Mungu alipowachagulia raha na amani na kuwa huru na dhiki ya maisha, Akawapa usingizi usioweza kuamshwa wala kuhofia chochote.

Na unaliona jua linapochomoza linaelemea kuumeni mwao mbali na pango lao; na lipokuchwa linawahepa kushotoni na wao wamo katika uwazi wake.

Yaani uwazi wa hilo Pango. Lilikuwa ni kubwa lenye uwazi wa kupitisha hewa safi na mwanga wa jua. Miili yao haiweza kufikiwa na jua si wakati wa mawiyo wala machweo. Kwa sababu walikuwa kwenye sehemu ambayo haifikiwi na mwanga wa jua au kwa kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa akiliepusha kwa kudura yake.

Hayo ni katika ishara zake.

Hayo ni pamoja na kutofikiwa na jua, kana kwamba ilikusudiwa kuwa hivyo. Pia kuwekwa katika hali ambayo si kuwa macho, kiasi ambacho wakati ulipita bila ya kujua; wala si mauti kwa kuwa na harakati na pumzi. Hakuna tafsiri ya haya isipokuwa uweza wa Mwenyezi Mungu na hekima yake.

Ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoza basi yeye ndiye aliyeongoka na anayempoteza hutampatia mlinzi (wala) mwongozi.

Makusudio ya ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoza ni watu wa pango na anayempoteza ni wale waliokusudia kuwatesa. Angalia Juz. 9 (7: 178).

Utawadhania wako macho na hali wamelala na tunawageuza kuume na kushoto na mbwa wao amenyoosha miguu yake ya mbele kizingitini.

Macho yao yalikuwa wazi kama vile yanaangalia mbele na damu inatembea mishipani, wanageuka upande huu na huo. Mbwa wao akiwa pembeni au mlangoni mwa pango kama mlinzi.

Lau ungeliwatokea bila shaka ungeligeuka kuwakimbia na ungelijazwa hofu.

Kwa sababu wako katika hali ya kushangaza isiyokuwa na mfano.

13

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَكَذَٰلِكَ بَعَثْنَاهُمْ لِيَتَسَاءَلُوا بَيْنَهُمْ ۚ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ كَمْ لَبِثْتُمْ ۖ قَالُوا لَبِثْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ
قَالُوا رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ فَابْعَثُوا أَحَدَكُم بِوَرِقِكُمْ هَٰذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ فَلْيَنظُرْ أَيُّهَا أَزْكَىٰ طَعَامًا
فَلْيَأْتِكُم بِرِزْقٍ مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا ﴿١٩﴾

19. Na kama hivyo tuliwainua ili waulizane. Alisema msemaji katika wao: Mmekaa muda gani? Wakasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku. Wakasema: Mola wenu anajua zaidi muda mliokaa. Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi pesa zenu aende mjini akaangalie chakula kipi kilicho kisafi zaidi awaletee riziki katika hicho, na awe mwangalifu, wala asiwajulishe kwa yeyote.

إِنَّهُمْ إِن يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِي مِلَّتِهِمْ وَلَن تُفْلِحُوا إِذًا أَبَدًا ﴿٢٠﴾

20. Kwani wao wakiwajua watawapiga mawe au watawarudisha katika mila yao na hamtafaulu kabisa.

وَكَذَٰلِكَ أَعْثَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوا أَنَّ وَعْدَ اللَّـهِ حَقٌّ وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا إِذْ يَتَنَازَعُونَ بَيْنَهُمْ
أَمْرَهُمْ ۖ فَقَالُوا ابْنُوا عَلَيْهِم بُنْيَانًا ۖ رَّبُّهُمْ أَعْلَمُ بِهِمْ ۚ قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم
مَّسْجِدًا ﴿٢١﴾

21. Na kama hivyo tuliwajulisha kwa watu wapate kujua kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli na kwamba saa haina shaka. Walipogombania jambo lao wao kwa wao, walisema: Jengeni jengo juu yao. Mola wao anawajua zaidi, Wakasema wale walioshinda katika shauri lao. Hakika tutawajengea msikiti juu yao.

سَيَقُولُونَ ثَلَاثَةٌ رَّابِعُهُمْ كَلْبُهُمْ وَيَقُولُونَ خَمْسَةٌ سَادِسُهُمْ كَلْبُهُمْ رَجْمًا بِالْغَيْبِ ۖ وَيَقُولُونَ سَبْعَةٌ
وَثَامِنُهُمْ كَلْبُهُمْ ۚ قُل رَّبِّي أَعْلَمُ بِعِدَّتِهِم مَّا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ ۗ فَلَا تُمَارِ فِيهِمْ إِلَّا مِرَاءً ظَاهِرًا وَلَا
تَسْتَفْتِ فِيهِم مِّنْهُمْ أَحَدًا ﴿٢٢﴾

22. Watasema ni watatu na wanne wao ni mbwa wao. Na wanasema ni watano na wa sita wao ni mbwa wao, kwa kuvurumisha ya ghaibu. Na wanasema ni saba na wa nane wao ni mbwa wao. Sema Mola wangu ndiye anayejua zaidi idadi yao, Hawawajui isipokuwa wachache. Basi usibishane juu yao ispokuwa mabishano ya juu juu; wala usiulize habari zao kwa yeyote yule.

## NA KAMA HIVYO TULIWAINUA

**Aya 19 – 22**

### SEHEMU YA TATU

Tumeishiria, katika maelezo yaliyotangulia, kuwa Aya zinazofungamana na watu wa pango zinagawanyika kwenye sehemu nne. Timekwishataja mbili na sasa tunaendelea na sehemu mbili za mwisho. Katika sehemu ya tatu ni kauli yake Mwenyezi Mungu:

Na kama hivyo tuliwainua ili waulizane.

Waliendelea na usingizi wao kwa muda wa miaka 309; kama itakvyoelezwa kwenye Aya ya 25. Kisha akawaamsha kutoka kwenye usingizi mrefu wa ajabu. Dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu aliwaamsha ili waulizane muda wa usingizi wao, na watakapofahamu hakika, imani yao kwa Mwenyezi Mungu na ufufuo itazidi.

**Unaweza kuuliza**: Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema, katika Aya ya 16, kuwa lengo la kuwaamsha ni kuwa wajue muda wao wale waliozozana kabla ya kuamka. Na katika Aya hii anasema kuwa aliwaamsha ili waulizane wao wenyewe. Je kuna wajihi gani wa Aya hizi mbili?

**Jibu**: hakuna kugongana baina ya Aya mbili. Kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwaamsha watu wa pango kwa mambo mawili: moja ameliashiria katika Aya iliyotangulia na jingine akaliashiria katika Aya hii. Kwa hiyo, maana ya Aya zote mbili ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwaamsha ili wajue wao na wengine kuwa Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kufufua wafu hata muda ukirefuka.

Alisema msemaji katika wao: Mmekaa muda gani? Wakasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku. Wakasema: Mola wenu ana- jua zaidi muda mliokaa.

Walipoamka walianza kuulizana, je mnajua mmekaa muda gani? Baadhi yao wakajibu kuwa tumekaa siku moja au baadhi ya siku. Kauli hii ni kuashiria kuwa hakuna kilichobadilika katika vitu vyao; si nguo wala nywele au kucha, nyuso, mili na hata rangi yao; ingawaje walikaaa muda mrefu. Lau kingebadilika kitu katika hivyo basi kingeonekana na wala asingesema msemaji miongoni mwao kuwa tumekaa siku moja au sehemu ya siku; kama asemavyo Razi.

Kisha wakasema tuachane na maswali haya, hakuna ajuae muda tuliokaa ila Mwenyezi Mungu.

Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi pesa zenu aende mjini akaangalie chakula kipi kilicho kisafi zaidi awaletee riziki katika hicho. na awe mwangalifu, wala asiwajulishe kwa yeyote. kwani wao wakiwajua watawapiga mawe au watawarudisha katika mila yao na hamtafaulu kabisa.

Pesa ilikuwa na sura ya mfalme wa wakati wao. inasemekana kuwa jina lake lilikuwa ni Dacianus na jina la mji lilikuwa ni Daqsus.

Waliamka na wakahisi njaa baada ya kukaa muda mrefu. Hivyo wakamtuma mmoja wao awanunulie chakula na wakamuusia awe na hadhari ili asitambuliwe na yeyote wasije wakauawa na mataghuti au wawafitini na dini yao. Hawajui kama wao wako kwenye zama nyingine

## SEHEMU YA NNE

Na kama hivyo tuliwajulisha kwa watu wapate kujua kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli na kwamba saa haina shaka. Walipogombania jambo lao wao kwa wao, walisema: Jengeni jengo juu yao, Mola wao anawajua zaidi. Wakasema wale walioshinda katika shauri lao. Hakika tutawajengea msikiti juu yao.

'Kama hivyo' ni ishara ya kwamba kama tulivyozidisha uongofu na kutia nguvu kwenye nyoyo zao, tukawalaza kisha kuwaamsha, basi vile vile tuliwadhihirisha kwa watu au watu wa mji uliokuwa karibu na pango.

Waliogombania ni watu wa mji uliokuwa karibu na pango. Walihitalifiana watu wa mji huo kuwa je, watu wa pango wamelala au wamekufa? Hiyo ni

baada ya kuona pesa ya zamani aliyokuwa nayo yule aliyetaka kununua chakula. Wakaenda pangoni na wakaona miili imelala chini haitingishiki wala kuzungumza.
Kauli yake Mwenyezi Mungu 'wale walioshinda' inaonyesha kuwa watu wa mji waligawanyika, kuhusiana na watu wa pango. Kuna waliosema tuwaache kama walivyo, waliosema tulizibe pango na wale waliosema tuwajengee msikiti utakoswaliwa na watu; na hili ndilo lililoshinda.
Baada ya kubainisha makusudio ya matamko ya Aya tuanze ufafanuzi:
Ni kawaida ya Qur'an kuacha kutaja kila maneno ambayo yataweza kufahamika kutokana na mfumo wa maneno ulivyo au mambo ambayo yanalazimiana na hali ya tukio. Kwa misingi hii ndio kukawa kuna jumla nyingi hazipo kwa vile zinajulikana kutokana na mazingira yalivyo. Muhtasari wa jumla zisizokuwepo:
Mmoja wao alikwenda mjini kununua chakula na alikuwa na hadhari, kama alivyousiwa na wenzake. Lakini yeye akatokewa na jambo ambalo hakulifikiria; pale alipotoa pesa kwa muuza chakula na akasema hii ni hela ya zamani haitumiki hivi sasa ni ya mfalme Dacianus; kama ilivyosemekana. Yule mwenye hela akasema: itakuwaje jana na leo tu.
Habari zikaanza kuenea mjini, Walipomuuliza kuhusu habari yake na ya pesa aliyokuwa nayo, aliwaambia kuwa yeye na wenzake walikimbia na dini yao kutoka kwa mataghuti na wakaeleka kwenye pango. Mmoja wa waliokuwa pale akasema ndio nimesikia kuwa zamani kuna watu walikimbia na dini yao kwa kumhofia mfalme Dacianus aliyechorwa kwenye pesa hii na wakakimbilia pangoni, Inawezekana ndio hawa. Watu wakamiminika pangoni baada ya yule mwenye pesa kuwahi pangoni na kuwaeleza wenzake.
Hatimaye baada ya kugunduliwa, walinyenyekea kwa Mwenyezi Mungu; kama walivyonyenyekea mwanzo, walipoingia pangoni. Wakamtaka Mwenyezi Mungu awape rehema yake na awachagulie lile ambalo linamridhisha Yeye Mwenyezi Mungu. kabla hawajamaliza dua yao walianguka wote na roho zao takatifu zikahamia kwenye rehema ya Mola wao kwenye neema ya milele, Watu wakawajengea msikiti.
Ushahidi katika kisa hiki ni dalili yake ya hisia kwa yale aliyoyadokeza Mwenyezi Mungu (s.w.t) "watu wapate kujua kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli na kwamba saa haina shaka" na kwamba binadamu ni wa milele akitoka kwenye nyumba hii na kuhamia nyumba nyingine. Ole wake tena ole wake yule anayeicha nyumba isiyoisha kwa nyumba inayoisha.

Watasema ni watatu na wanne wao ni mbwa wao. Na wanasema ni watano na wa sita wao ni mbwa wao, kwa kuvurumisha ya ghaibu. Na wanasema ni saba na wa nane wao ni mbwa wao.

Watu wametofautiana mahali palipokuwa na pango. Ikasemekana lilikuwa Palestina karibu na Baytul-muaqaddas, Ikasemekana lilikuwa Musel. Pia imesemekana lilikuwa Hispania upande wa Granada na kauli nyingi nyenginezo.
Vile vile wametofautiana kuhusu wakati wa tukio, Kuwa je lilikuwa kabla ya Bwana Masih au baada yake? Pia wametofautiana kuhusu chakula alichoambiwa anunue, kuwa je kilikuwa tende, zabibu au nyama? Bali hata

wametofautiana katika rangi ya mbwa kuwa je alikuwa rangi ya kahawia au wa madoadoa, Na tofauti nyingi nyenginezo. Kwa hiyo si ajabu kutokea tofauti katika idadi ya watu wa pango.
Katika Tafsir ya Razi na Tabrasi imeelezwa kuwa ulipokuja ujumbe wa wakristo wa Najrani kwa Mtume **(s.a.w.w)** yalipita mazungumzo kuhusu watu wa pango. Akasema mmoja katika wakiristo, anayeitwa Ya'qubiya: "Walikuwa watatu na wa nne wao ni mbwa wao." Akasema Nasturiya: "Walikuwa ni watano na wa sita wao ni mbwa wao." Wakasema waislamu: "Walikuwa ni saba na wa nane wao ni mbwa."
Kisha Razi akaendelea kusema: Wafasiri wengi wamesema kuwa wao walikuwa saba na wa nane wao ni mbwa. Akataja njia nne za kusihi kauli hii. Tatu katika hizo ni za kuangaliwa na ya nne ina mwelekeo. Kwa ufupi kauli hiyo inasema kuwa kauli ya tatu na ya tano, Mwenyezi Mungu amesema huko ni kuvurumisha yasiyojulikana, lakini alipotaja ya saba akanyamaza, kwa hiyo inawajibisha kuwa ndiyo ya sawa.

Sema: Mola wangu ndiye anayejua zaidi idadi yao, Hawawajui isipokuwa wachache.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuishiria tofauti za watu kuhusu idadi ya watu wa pango na kwamba kauli zote au baadhi yake ni kusema tu bila ya uhakika, sasa anamwambia Mtume wake mtukufu:
Tofauti zote hizi hazina umuhimu; na kwamba ni juu ya kila mtu kumwachia Mungu, kuzingatia yale yaliyowapitia watu wa pango na kuyachukulia kuwa ni dalili ya ufufuo; sio kujadili idadi, mahali au wakati. Kwa sababu lengo la kisa hiki ni mazingatio na mawaidha; bali hili ndilo lengo la visa vyote vya Qur'an; ndilo la kwanza na la mwisho:

لَقَدْ كَانَ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١١١﴾

"Kwa hakika katika simulizi zao mna mazingatio kwa wenye akili," Juz;13 (12:111).

Basi usibishane juu yao ispokuwa mabishano ya juu juu; wala usiulize habari zao kwa yeyote yule.

Juu yao ni kuhusu hao watu wa pango. Yaani ewe Muhammad! Usiwe na haja kabisa ya kujadiliana na yeyote katika watu wa Kitab kuhusu idadi ya watu wa pango wala usimuulize ulama katika wao, kwani suala hilo sio lenyewe hasa; bali yule mwenye kubishana mwambie kwa upole tu; mfano Mungu ndiye ajuaye au mjadala huu hauna faida n.k.

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَيْءٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿٢٣﴾

23. Wala kamwe usiseme kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho;

إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ وَاذْكُر رَّبَّكَ إِذَا نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَن يَهْدِيَنِ رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشَدًا ﴿٢٤﴾

24. Isipokuwa akipenda Mwenyezi Mungu. Na mkumbuke Mola wako pale unaposahahu, na sema: Asaa Mola wangu akaniongoza kwenye uongozi ulio karibu zaidi kuliko huu.

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٢٥﴾

25. Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu na wakazidisha tisa.

قُلِ اللَّـهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا ۖ لَهُ غَيْبُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ أَبْصِرْ بِهِ وَأَسْمِعْ ۚ مَا لَهُم مِّن دُونِهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا يُشْرِكُ فِي حُكْمِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾

26. Sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi muda waliokaa. Ni zake siri za mbingu na za ardhi. Kuona kulikoje kwake na kusikia, Hawana mlinzi isipokuwa Yeye; wala hamshirikishi yeyote katika hukumu yake.

## INSHAALLAH

**Aya 23-26**

### MAANA

Wala kamwe usiseme kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifaya hilo kesho; isipokuwa akipenda Mwenyezi Mungu.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kumwambia usibishane, alimwamrisha afungamanishe kila jambo lake na matakwa ya Mungu.

Mtu anaweza kupitiwa akafanya lile aliloliazimia kuliacha au akaacha lile aliloliazimia kulifanya; Hili linaweza kumtokea hata maasumu, maadamu sio la kumwasi Mungu; kwa sababu isma haiwezi kuwa pamoja na maasi kwa hali yoyote ile; sawa na ambavyo elimu haiwezi kuwa pamoja na ujinga.

### UTASHI MKUU

Mazingira yana athari, hilo halina shaka, lakini sio kila kitu kwa binadamu, Ni mtu gani ambaye kila analolitaka analipata? Hata awe na uwezo au cheo kiasi gani! Ni nani ambaye ameweza kumfanya mkewe au mwanawe vile anavyotaka awe kiumbo na kitabia? Ongezea mifano mingine kadiri unavyotaka, Hakuna yeyote ambaye amenyookewa na kila analolitaka; hata katika mazungumzo na usingizi.

Kwa hiyo utashi wa mtu upo na una athari yake, lakini utashi huu unahukumiwa na utashi wa Mwenyezi Mungu ambaye anasema: ukitaka jambo litafute kwa sababu zake na njia zake za kimaumbile ambazo nimeziweka, lakini angalia usinisahau; Kwani wewe unatembea kwenye njia yangu. Mimi ndiye niliyekuumba, nikakutengenezea njia na nikakupa mwongozo wa njia hiyo, tena nikakuamrisha uifuate.

Vile vile usisahau kuwa njia niliyokutengeneza haiwezi kukufikisha, kwa hali yoyote ile, kwenye matakwa yako; hata ukijitahidi kiasi gani. Kwa sababu mimi vile vile nimetengeneza vikwazo kwenye njia hiyo; Si wewe wala mwingine mwenye uwezo navyo; Kwa sababu viko mikononi mwangu. Ni mimi ndiye ninayevizuia na ni mimi ndiye ninayeviachia. Usikate kabisa kuwa wewe utafika kila unapotaka; isipokuwa kwa matakwa ya juu. Tazama kifungu cha ‘Siri na matukio ya ghafla’ katika Juz.2 (2:210).

Na mkumbuke Mola wako pale unaposahahu.

Kila mtu hutokewa na kusahau; hasa akiwa ametingwa na shughuli na huzuni. Hata imesemekana neno la kiarabu insan lililo na maana ya mtu, linatokana na neno nasiya lenye maana ya mwenye kusahau.

Mwenyezi Mungu ametuamrisha tumkumbuke tunaposahau na akatufundisha namna ya kukumbuka pale aliposema: na sema: Asaa Mola wangu akaniongoza kwenye uongozi ulio karibu zaidi kuliko huu.

Yaani kama Mwenyezi Mungu hatanikumbusha yale niliyoyasahau. Basi yeye atanikumbusha yaliyo na masilahi na manufaa zaidi kuliko haya. Na kusahau baadhi ya mambo kuna faida zake nyingi.
Kwa mnasaba wa Aya hii tutaje kisa ambacho ni nadra kutokea cha kuhusudiana watu wa elimu ya dini; kama wanavyohusudiana wafanyakazi na wafanyabiashara:
Imepokewa riwaya kwamba Mansur alikuwa akimfadhilisha sana Abu Hanifa kuliko wanafiqh wengine. Muhammad bin Is-haq akamuonea wivu. Siku moja wakakutana wote mbele ya Mansur, Muhamad akamuuliza Abu Hanifa akikusudia kumshinda na kumnyamazisha, kama ifuatavyo:-
Muhammad: Unasemaje kuhusu mtu aliyeapa akanyamaza kwa muda, kisha akasema inshaallah.
Abu Hanifa: Kiapo chake kitafaa na atalazimiana nacho, kwa sababu kauli yake ya inshaallah imetengana na kiapo, lau haikutengana basi kiapo hak itafaa.
Muhammad: Vipi na babu wa Amir Al-muminin – akimkusudia Mansur – hasemi hivyo?
Mansur akamgeukia Abu Hanifa: Eti ni kweli babu alisema hivi?
Abu Hanifa: Ndio
Mansur: Sasa unampinga babu yangu ewe Abu hanifa?
Abu Hanifa: Kauli ya babu yako ni sahihi lakina kuna taawili, inayoitoa kwenye ushahihi. Huyu Muhammad na wenzake hawakuoni kuwa wewe unastahiki ukhalifa; Kwa sababu wao wanakubai, kisha wakitoka wanasema inshaallah. Maana yake ni kuwa katika madhehebu yao wao hawakukubali kuwa wewe ni khalifa kwa kuzingatia kuwa Mwenyezi Mungu hakutaka wewe uwe khalifa.
Basi Mansur akakasirika sana akawaambia maaskari wake mchukueni huyu, akimwashiria Muhammad bin Is-haq. Basi ule mtandio wake wakauweka shingoni mwake wakamburura hadi korokoni.
Kwa mnasaba huu tunadokeza kuwa mtu akisema: nimekuuzia kitu, inshaallah au mke wangu nimemtaliki inshaallah au pia kusema: wallahi sitafanya hivi inshaalllah n.k. Basi akisema hivyo ataangaliwa: ikiwa alikusudia kutabaruku na jina tu la Mwenyezi Mungu, basi atalazimiana na aliyoyasema, Itakuwa bei yake, talaka au kiapo chake kimefungika. Ama ikiwa amekusudia kuwa hilo ni sharti basi hatalazimika na kitu kwa sababu hilo sharti litakuwa limevunja alichokisema.
**Unaweza kuuliza**: Je, tutajuaje alichokikusudia?
**Jibu**: hilo litategema msemaje yeye mwenye. Kwa sababu makusudio hayakujulikana isipokuwa kwa yule aliyekusudiwa; na kadhi atachukua kauli yake.

Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu na wakazidisha tisa.

Baada ya kutoka nje kidogo Mwenyezi Mungu amerudia kisa cha watu wa pango na kubainisha kuwa wao walibaki kwenye usingizi kwa muda wa miaka 309.
**Unaweza kuuliza**: Kwa nini akasema na wakazidisha tisa badala ya kusema moja kwa moja, mia tatu na tisa?

**Jibu**: Baadhi ya wafasiri wamejibu kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema miaka 300 kwa hisabu ya miaka ya jua na 309 kwa miaka ya mwezi. Kwa sababu tofauti kati yake ni miaka mitatu kwa kila mia.

Sema: Mwenyezi Mungu anajua zaidi muda waliokaa. Ni zake siri za mbingu na za ardhi.

Ndio anajua; Kwa sababu Yeye ndiye aliyewaumba, akawaongoza, akawalaza na akawaua, Na ametoa habari kuwa walikaa miaka 309. Kauli yake ni haki.

Kuona kulikoje kwake na kusikia.

Yaani anaona sana kila linaloonwa na anasikia sana kila linalosikiwa. Makusudio ni kuwa hakifichiki kwake kitu chochote.

Hawana mlinzi isipokuwa Yeye; wala hamshirikishi yeyote katika hukumu yake.

Viumbe hawana mlinzi yeyote asiyekuwa Mwenyezi Mungu, Maana ni kuwa hakuna wa kumsaidia aliyedhalilishwa na Mungu na hakuna wa kumdhalilisha aliyesaidiwa na Mungu na wala hakuna wa kuzuia alichokitoa na kutoa alichokizuia; Kwa sababu Yeye yuko peke yake hana mshirika. Ufalme uko mikononi mwake na Yeye ni muweza wa kila kitu.

14

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَاتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِن كِتَابِ رَبِّكَ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ وَلَن تَجِدَ مِن دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٢٧﴾

27. Na soma uliyopewa wahyi katika kitabu cha Mola wako, Hapana wa kubadilisha maneno yake, Wala hutapata makimbilio isipokuwa kwake.

وَاصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ
تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

28. Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni, wakitaka radhi yake; wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka mapambo ya maisha ya dunia; wala usimtii tuliyemghafishilisha moyo wake asitukumbuke na akafuata matamanio yake na mambo yake yakawa yamepita kiasi.

وَقُلِ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ فَمَن شَاءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَاءَ فَلْيَكْفُرْ إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ نَارًا أَحَاطَ
بِهِمْ سُرَادِقُهَا وَإِن يَسْتَغِيثُوا يُغَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ بِئْسَ الشَّرَابُ وَسَاءَتْ مُرْتَفَقًا
﴿٢٩﴾

29. Sema hii ni kweli itokayo kwa Mola wenu, basi atakaye aamini na atakaye akufuru. Hakika sisi tumewaandalia wenye kudhulumu moto ambao hema lake litawazunguka, Na wakiomba msaada watapewa maji kama mafuta yaliyotibuka yanayobabua nyuso. Kinywaji kibaya kilioje na mahali pabaya palioje pa kupumzika!

## SOMA ULIYOPEWA WAHYI

**Aya 27 -29**

### MAANA

Na soma uliyopewa wahyi katika kitabu cha Mola wako, Hapana wa kubadilisha maneno yake.

Anasema Mwenyezi Mungu kumwambia Mtume wake mtukufu: Fikisha tuliyokuteremshia yanayohusiana na watu wa pango na wengineo katika yaliyokuja kwenye Qur'an Tukufu. Kuwa na yakini na yale tunayokupa habari. Amesema kweli Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake.

Siku na matukio yamethibitisha kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** ni rehema iliyoongozwa kutoka mbinguni kwa ajili ya watu. Kila zama zinavyozidi kuendelea ndio unapatikana ushahidi wa hakika hii.

Wala hutapata makimbilio isipokuwa kwake.

Yaani huna pa kumkimbia Mungu, Maneno anaambiwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Maana yake ya dhahiri ni kuwa wewe Muhammad una majukumu mbele ya Mwenyezi Mungu wala hutapona ukiwa utatia shaka katika haki- ka ya Qur'an au kufanya uzembe katika kuifikisha.

Hasha! Haiwezekani kwa Mtume wa rehema kutia shaka au kufanya uzembe. Vipi iwe hivyo na hali Mwenyezi Mungu anajua zaidi pa kuuweka ujumbe wake! Isipokuwa makusudio ni kumweleza yule anayetia shaka katika utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** au kuhalifu aliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni, wakitaka radhi yake; wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka mapambo ya maisha ya dunia; wala usimtii tuliyemghafishilisha moyo wake asitukumbuke na akafuata matamanio yake na mambo yake yakawa yamepita kiasi.

Ikisemwa isuburishe nafsi yako pamoja na fulani; yaani kuwa naye. Makusudio ya wanaomuomba Mola wao ni wale waumini wenye ikhlasi. Asubuhi na jioni ni fumbo la kudumu kwenye twaa ya Mungu. macho yako yasiwaruke kwa kutaka mapambo ya dunia; yaani usigeuze umuhimu wako kutoka kwa watu wa dini ukaenda kwa watu wa dunia. Waliogahafishilishwa ni makafiri na wenye makosa. Kupita kiasi mambo ni kauli na vitendo kupituka haki na uadilifu.

Imepokewa kuwa Uyayna - mmoja wa viongozi wa washirikina - alikwenda kwa Mtume **(s.a.w.w)** akaona mafukara wamekaa naye, akiwemo Salmani Farisi akiwa na kilemba kilichojaa jasho na mkononi akiwa na jani la mtende.

Uyayna akasema: “Huu uvundo wa hawa haukusumbui wewe. Sisi vigogo wa Mudhar tukisilimu watasilimu watu wengi, Hakuna kinachotuzuia isipokuwa wafuasi wako hawa tu, Hebu achana nao tukufuate sisi au uwafanyie kikao chao na sisi tuwe na kikao chetu” Ndipo ikashuka Aya hiyo.

Sisi hatujui usahihi wa mategemezi ya riwaya hii, lakini tunaitilia nguvu kwa sababu inaenda na muktadha wa hali; yaani hali ya wapenda makuu na kujifanya wakubwa wakiwadharau wanyonge. Hilo limenukuliwa na Qur’an:

وَمَا نَرَاكَ اتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَاذِلُنَا بَادِيَ الرَّأْيِ ﴿٢٧﴾

“Wala hatukuoni wamekufuata ila wale wanaonekana dhahiri kwetu kuwa ni watu duni” Juz; 12, (11:27).

Kabla ya Mtume **(s.a.w.w)** kumjibu Uyayna na mfano wake kuwa ndio au hapana, aliye Mtukufu na kutuka akamwambia: kuwa pamoja na waumini, kwa vile wao wako pamoja nami, nami niko pamoja nao na uvumilie na wanayoyasema wapenda makuu. Kwa sababu subira yako kwao ni subira ya Mwenyezi Mungu na utiifu wake. Kwani huoni imani yao na ikhlasi yao kwangu na kwako katika kila kitu, wakitaka radhi yangu na thawabu zangu?

Ama waovu waliopofushwa na matamanio ya nyoyo zao, wanaofanya mambo kwa masilahi yao tu, wakikataa kuishi na wengine kwa haki na uadilifu, isipokuwa kiburi na kujikweza na kupituka mipaka yote ya Mwenyezi Mungu na ya binadamu, Hawa usiwasikilize. Kwani kauli yao hiyo ni ushenzi, uongo na upotevu; bali ni juu yako kupambana nao na kuwawekea ngumu kwa kauli na vitendo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قَاتِلُوا الَّذِينَ يَلُونَكُم مِّنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّـهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٢٣﴾

“Enyi mlioamini! Piganeni na wale walio karibu yenu katika makafiri na wakute kwenu ugumu; na jueni kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye takua.” Juz, 11 (9:123).

Sema hii ni kweli itokayo kwa Mola wenu.

Anaambiwa Mtume awaambie wale walioghafilishwa nyoyo zao au watu wote. Hii ni usisitizo wa kauli iliyotangulia ya wasomee uliyopewa wahyi

Basi atakaye aamini na atakaye akufuru.

Hii ni sawa na kauli yake Mungu:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

"Hakika sisi tumembainishia njia, Ama ni mwenye kushukuru au mwenye kukufuru" (76:3).

Aya hii inafahamisha kuwa mtu ana hiyari sio mwenye kuendeshwa, Lakini Razi amemrudi mwenye kutoa dalili kwa Aya hii kwamba utashi wa mtu haufanyi yeye mwenyewe, bali unafanywa na Mungu kwa hiyo kwake yeye mtu ni mwenye kuendeshwa hana hiyari.

Nasi tunamjibu: Hakika utashi wa mtu unatokana na sababu na mazingira yanayomzunguka. Mfano mtu kumuona mwanamke mzuri nafsi yake ikampondokea, na hali dini imewajibisha mtu kuizuiwa nafsi yake, katika hali hii.

Hakuna mwenye shaka kwamba hili liko chini ya uwezo wake mtu (anaweza kulizuia), Mtume wa Mwenyezi Mungu ameliita hilo 'Jihadi kubwa' Kuna riwaya isemayo kuwa Mtume alituma kikosi cha wapiganaji.

Kiliporudi, akasema: Karibuni watu waliomaliza jihadi ndogo na kubakiwa na jihadi kubwa." Akaulizwa ni ipi jihadi kubwa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Jihadi ya nafsi. Hakika jihadi bora ni ya yule mwenye kufanya jihadi ya nafsi yake ambayo iko baina ya mbavu zake.

Hakika sisi tumewaaandalia wenye kudhulumu moto ambao hema lake litawazunguka. Na wakiomba msaada watapewa maji kama mafuta yaliyotibuka yanayobabua nyuso. Kinywaji kibaya kilioje na mahali pabaya palioje pa kupumzika!

Hili ni onyo na hadhari kwa kwa yule anayeathirika na ukafiri kuliko imani na batili kuliko haki, kwamba adhabu itazunguka pande zote; sawa na hema linavyomzunguka mtu, na watendela kupata kila aina ya dhabu.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٣٠﴾

30. Hakika wale ambao wameamini na wakatenda mema, hakika sisi hatupotezi ujira wa anayefanya mazuri

أُولَـٰئِكَ لَهُمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِن ذَهَبٍ وَيَلْبَسُونَ

ثِيَابًا خُضْرًا مِّن سُندُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُّتَّكِئِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ نِعْمَ الثَّوَابُ وَحَسُنَتْ مُرْتَفَقًا ﴿٣١﴾

31. Hao wana bustani za milele zinazopita mito chini yake, watavaa nguo za kijani za hariri na atlasi, Huku wakiegemea juu ya makochi. Ni malipo bora yalioje na mahali pazuri palioje pa kupumzika.

## UJIRA WA WATENDAO MEMA HAUPOTEI

**Aya 30 – 31**

### MAANA

Hakika wale ambao wameamini na wakatenda mema, hakika sisi hatupotezi ujira wa anayefanya mazuri.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwataja madhalimu na adhabu yao, sasa anataja wema na malipo yao. Akabainisha aina hii ya thawabu kwa kauli yake:

Hao wana bustani za milele zinazopita mito chini yake, watavaa nguo za kijani za hariri na atlasi, Huku wakiegemea juu ya makochi. Ni malipo bora yalioje na mahali pazuri palioje pa kupumzika.

Katika Aya nyingine Mwenyezi Mungu anasema:

وَفِيهَا مَا تَشْتَهِيهِ الْأَنفُسُ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ﴿٧١﴾

"Na humo vitakuwemo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia" (43:71).

Imam Ali (a.s) anasema: "Kila neema isiyokuwa Pepo ni ya kudharauliwa na kila balaa isiyokuwa moto ni raha." Umepita mfano wake katika Aya nyingi ikiwemo Juz. 1 (2: 82), Juz.4 (3:171) na Juz.5 (4:57).

Kauli ya kushangaza ni ile ya badhi ya masufi, kwamba makusudio ya kivazi ni tawhid, nguo za kijani ni sifa zinazoleta furaha, hariri ni vipawa, atlasi ni maadili na makochi ni majina ya Mwenyezi Mungu.

Wala hakuna ujeuri mkubwa kwa Mungu kuliko kutafsiri makusudio yake kwa njozi na mawazo au kwa hawaa na malengo mengine.

وَاضْرِبْ لَهُم مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ أَعْنَابٍ وَحَفَفْنَاهُمَا بِنَخْلٍ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا زَرْعًا ﴿٣٢﴾

32. Na wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao tulimjalia vitalu viwili vya mizabibu na tukavizunguushia mitende na kati yake tukajaalia mimea ya nafaka.

كِلْتَا الْجَنَّتَيْنِ آتَتْ أُكُلَهَا وَلَمْ تَظْلِم مِّنْهُ شَيْئًا وَفَجَّرْنَا خِلَالَهُمَا نَهَرًا ﴿٣٣﴾

33. Hivyo vitalu viwili vikitoa mazao yake, wala hapana kitu katika hivyo kilichotindika. Na ndani yake tukapasua mito.

وَكَانَ لَهُ ثَمَرٌ فَقَالَ لِصَاحِبِهِ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَنَا أَكْثَرُ مِنكَ مَالًا وَأَعَزُّ نَفَرًا ﴿٣٤﴾

34. Naye alikuwa na mazao. Basi akamwambia mwenzake naye akibishana naye: Mimi nimekushinda kwa mali na nguvu za watu.

وَدَخَلَ جَنَّتَهُ وَهُوَ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ قَالَ مَا أَظُنُّ أَن تَبِيدَ هَـٰذِهِ أَبَدًا ﴿٣٥﴾

35. Akaingia kitaluni kwake, naye ameidhulumu nafsi yake, akasema: Sidhani kuwa haya yataharibika milele.

وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَئِن رُّدِدتُّ إِلَىٰ رَبِّي لَأَجِدَنَّ خَيْرًا مِّنْهَا مُنقَلَبًا ﴿٣٦﴾

36. Wala sidhani kuwa hiyo saa (ya Kiyama) itatokea, Na kama nitarudishwa kwa Mola wangu bila shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.

قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَكَفَرْتَ بِالَّذِي خَلَقَكَ مِن تُرَابٍ ثُمَّ مِن نُّطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّاكَ رَجُلًا ﴿٣٧﴾

37. Mwenzake akamwambia kwa kubishana naye: Je, umemkufuru ambaye amekuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha akakufanya kuwa mtu kamili?

لَّـٰكِنَّا هُوَ اللَّـهُ رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٣٨﴾

38. Lakini Yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu, wala si mshirikishi na yeyote.

وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّـهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّـهِ ۚ إِن تَرَنِ أَنَا أَقَلَّ مِنكَ مَالًا وَوَلَدًا
﴿٣٩﴾

39. Na lau ulipoingi kitaluni kwako ungelisema, alitakalo Mwenyezi Mungu huwa (mashaallah!), hapana nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu. Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe.

فَعَسَىٰ رَبِّي أَن يُؤْتِيَنِ خَيْرًا مِّن جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَانًا مِّنَ السَّمَاءِ فَتُصْبِحَ صَعِيدًا زَلَقًا
﴿٤٠﴾

40. Basi huenda Mwenyezi Mungu akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako na kukipelekea maafa kutoka mbinguni na kugeuka ardhi tupu inayoteleza.

أَوْ يُصْبِحَ مَاؤُهَا غَوْرًا فَلَن تَسْتَطِيعَ لَهُ طَلَبًا ﴿٤١﴾

41. Au maji yake yadidimie usiweze kuyagundua.

وَأُحِيطَ بِثَمَرِهِ فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ عَلَىٰ مَا أَنفَقَ فِيهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَقُولُ يَا لَيْتَنِي
لَمْ أُشْرِكْ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٤٢﴾

42. Yakaangamizwa matunda, akabaki anapinduapindua viganja vyake, kwa vile alivy - oyagharimia, nayo imeanguka juu ya chanja zake. Akawa anasema: Laiti nisingelimshirikisha Mola wangu na yoyote.

وَلَمْ تَكُن لَّهُ فِئَةٌ يَنصُرُونَهُ مِن دُونِ اللَّـهِ وَمَا كَانَ مُنتَصِرًا ﴿٤٣﴾

43. Wala hakuwa na kundi la kumsadia kinyume na Mwenyezi Mungu wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.

هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلَّـهِ الْحَقِّ ۚ هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا وَخَيْرٌ عُقْبًا ﴿٤٤﴾

44. Huko usaidizi ni wa Mwenyezi Mungu, Mkweli. Yeye ni Mbora kwa malipo na mbora wa matokeo.

## BAINA YA KAFIRI TAJIRI NA MUMIN FUKARA

**Aya 32 – 44**

### MUHTASARI WA KISA

Tulipofasiri Aya 27 ya Sura hii tulitaja kuwa vigogo wa kishirikina walitoa sharti la kumwamini kwao Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuwa awafukuze mafukara au awatengee vikao vyao ili wasichanganyike na mafakura, kwa vile wao ni mabwana na viongozi na watu wengine ni watumwa wao tu.

Aya tulizo nazo sasa zinaleta picha ya matajiri wenye kiburi, kwa mtu mmoja tajiri mwenye mali na mashamba na picha ya mafukara waumini, kwa mtu mmoja fukara asiye na chochote, lakini anajitukuza kwa maadili yake na tajiri anajitukuza kwa mali yake. Yanapita majibizano baina yao yanayowakilisha mvutano baina ya haki na batili. Hatimaye haki inashinda na batili inaanguka. Amesema kweli mwenye hekima aliyesema: "Mwenye kupigana na haki itampiga mweleka"

Kwa ufupi, maana ya Aya hizo ni: Yule anayejitukuza kwa mali yake, anamiliki mashamba mawili makubwa yenye miche ya ngano na nafaka nyinginezo. Pia mna miti mingi ya mitende na mizabibu. Mashamba yote mawili yana chemchem ya maji; mavuno yake ni mazuri na kamili. Ama yule anayejitukuza kwa maadili yake, hana kitu chochote.

Mwenye mashamba akamwambia yule fukara kwa kujisifu na kujinaki: Mimi nimekushinda na kila kitu – mali na jaha. Angalia mimea, miti, matunda na mito ya maji niliyo nayo. Hii ndio milki ya kudumu itakayokuja wafaa watoto na wajukuu; sio pepo mnayodai nyinyi masikini. Hivi baada ya mauti kweli kuna pepo na moto? Kama itakuwa ni kweli basi hadhi yangu huko itakuwa kubwa kuliko hapa duniani. Kwa sababu aliye tajiri hapa huko pia atakuwa tajiri .

Yule mumin akamjibu kwa kumjadili na kumlaumu: Hivi unasema haya kwa kumbughudhi na kumkufuru ambaye amekufanya uwe mtu? Umesahau asili yako? Wewe si umetokana na Adamu na Adam akatokana na mchanga? Hukuwa wewe ni tone la manii? Mimi mwenzako ninamwamini Mwenyezi Mungu na ninampwekesha, ninamsifu kwa kuniongoza kwenye njia yake na radhi zake. Kama ungekuwa na busara basi ungelimnyenyekea Mwenyezi Mungu na kumshukuru badala ya kujitia ujuvi kwa dhambi. Ni lipi liliokufanya ujiaminishe na mambo ya kushtukiza ya ghafla? Mungu akiwapa muda waasi kwa huruma zake huwa amewapa muda wa hasira zake na nakama yake.

Kabla ya hata kumaliza maneno yake yule mumin, mara miti ikaanza kuanguka, mito ikakauka, mimea ikateketea na kila kitu shambani kikaharibika. Mwenye shamba akasema: “Sikufikira kabisa itaharibika hii.” Baada ya kuona alivyofanya Mwenyezi Mungu na kukata tamaa ya mimea yake na miti yake alisema kwa masikitiko: “Laitani nisingemshirikisha Mola wangu na yeyote.” Lakini wapi! Hivi sasa na hali hapo mwanzo umemuasi na ukawa katika wafisadi?

Huu ndio muhtasari wa kisa. Na makusudio ya kisa hicho ni kuwa mtu aamini kwa kauli na vitendo kuwa hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu mmoja mwenye kushinda. Na kwamba Yeye ambaye imetukuka hekima yake saa yoyote anayotaka anaweza kumgeuza mtukufu kuwa dhalili na dhalili kuwa mtukufu. Vilevile tajiri kuwa fukara na fukara kuwa tajiri na afya kuwa ugonjwa na maumivu na kinyume chake. Vile vile mtu aamini kuwa milki ya mwenye kuumbwa si chochote kadiri itakavyokuwa ila akiibadilisha katika kazi za kheri.

Baada ya muhtasari huu sasa tuingilie ufafanuzi wa na tafsiri ya Aya ingawaje nyingi ziko wazi zisizohitaji ufafanuzi.

## MAANA

Na wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao tulimjalia vitalu viwili vya mizabibu na tukavizunguushia mitende na kati yake tukajaalia mimea ya nafaka, Hivyo vitalu viwili vikitoa mazao yake, wala hapana kitu katika hivyo kilichotindika. Na ndani yake tukapasua mito.

Anaambiwa Muhammad **(s.a.w.w)** awambie washirikina waliosema kuwa awafukuze mafukara au amwambie kila mpenda makuu mwenye kiburi, Makusudio ya watu wawili ni tajiri na fukara ambao walikuwa na majibizano.

Ni maarufu Qur’an kuwa mara nyingi inaleta mifano ya fikra na misingi ya kiujmla na kufananisha na vitu vyenye kuhisiwa; kama kufananisha imani na nuru na ukafiri na giza. Pia mara nyingine inafananisha chenye kuhisiwa na chenye kuhisiwa kingine kilichowazi zaidi na kilicho na ubainifu zaidi; kama kufananisha mwenye kurtadi na mbwa mwenye kuhema kwa nguvu.

Lengo la yote hayo ni kufafanua na kuweka wazi, kuongezea mazingatio na mawaidha:

وَعَادًا وَثَمُودَ وَأَصْحَابَ الرَّسِّ وَقُرُونًا بَيْنَ ذَٰلِكَ كَثِيرًا ﴿٣٨﴾ وَكُلًّا ضَرَبْنَا لَهُ الْأَمْثَالَ وَكُلًّا تَبَّرْنَا تَتْبِيرًا ﴿٣٩﴾

"Na tuliwaangamiza kina watu A'd na Thamud na watu wa Rass na vizazi vingi vilivyokuwa kati yao na wote tuliwapigia mifano." (25:38-39).

Mwenyezi Mungu (s.w.t) hapa amefananisha hali ya mataghuti wapenda makuu wenye kiburi na mtu mmoa kafiri mwenye kiburi mjinga aliye na vitalu viwiwili ambavyo ndani yake mna mto, mimea ya nafaka na miti inayobeba matunda bora ya wakati huo, ambayo ni tende na zabibu.

Mimea yote inatoa mazao kwa wakati wake kwa ukamilifu. Na akamfananisha mumin na mtu mmoja mnyeneykevu mwenye maarifa, lakini hana chochote ni fukara. Yakatokea majibizano baina ya wawili hao; kama ifuatavyo:-

Basi akmwambia mwenzake naye akibishana naye.

Aliyesema ni yule tajiri mwenye kiburi kumwambia mwenzake mumin mwenye adabu

Mimi nimekushinda kwa mali na nguvu za watu.

Aliona kuwa mali na jaha ndio kipimo cha utukufu, lakini imani na ikhlasi ni maneno matupu tu yasiyokuwa na maana. Hii ndio mantiki ya mafasiki na wovu, tangu zamani hadi leo. Thamani ya mtu kwao ni kile anachokimiliki, sio matendo mema wala elimu nzuri.

Mali ndiyo inayosababisha matatizo ya binadamu, Ndio kichocheo cha kwanza cha fitina ya silaha za maangamizi na kutumia mamilioni ya walalahoi kutengenezea silaha hizo. Wanyonyaji wanaiba mali ya wananchi na kuigeuza mabomu na maroketi kisha wayatupe kwa hao hao wananchi waliowanyanganya riziki zao na maliasili zao.

Akaingia kitaluni kwake, naye ameidhulumu nafsi yake kwa sababu aliyaitikia matamanio yake akaitia hatarini nafsi yake; sawa na anayemkubalia mwanawe mambo yatakayomdhuru na kumwangamiza.

Akasema: Sidhani kuwa haya yataharibika milele.

Razi anasema: "Vipi alisema kuwa sidhani kuwa haya yataharibika milele pamoja na kuwa hisia zinafahamisha kuwa dunia si yenye kubakia? Tunasema: alikusudia kuwa havitaharibika katika uhai wake"

Jibu sahihi ni kuwa ujinga na ghururi zilimpofusha mwenye shamba na kila kitu hata na vitu waziwazi na vyenye kuhisiwa. Anasema Mtukufu wa wasemao: "Wana nyonyo, lakini hawafahamu kwazo, na wana macho, lakini hawaoni kwayo, na wanayo masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama bali wao ni wapotevu zaidi, Hao ndio walioghafilika." Juz. 9 (7:179).

Wala sidhani kuwa hiyo saa (ya Kiyama) itatokea.

Dhana hii haitegemei chochote isipokuwa majivuno ghururi na mambo ya kuwazia tu, kwamba neema yake ni ya milele haitaisha. Hii ndio tafsiri ya mataghuti wajivuni wanaokana hisabu na ufufuo.

Na kama nikirudishwa kwa Mola wangu bila shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.

Kwa fikra yake anaona kuwa wapenda makuu huko pia wana nafasi, Anakisia ya ghaibu kwa ya sasa. Hajui kwamba uokovu kesho ni wa wamchao Mungu, sio mataghuti na wajivuni:

مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَهْ ﴿٢٨﴾ هَلَكَ عَنِّي سُلْطَانِيَهْ ﴿٢٩﴾

"Mali yangu hayakunifaa, Madaraka yangu yamenipotea" (69:28-29).

Mwenzake akamwambia kwa kubishana naye: Je, umemkufuru ambaye amekuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha akakufanya mtu kamili?

Mumini alimwambia kafiri kwa kumlaumu, kuwa unamkana aliyekuumba na dalili zake ziko wazi kwako? Umepata vipi uhai pamoja na akili yake na uoni wake? Si ulikuwa si chochote?

Lakini Yeye Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu, wala si mshirikishi na yoyote.

Anaendelea kusema mumin, ama mimi nimeongoka kwa umbile langu na akili yangu kwa muumba wangu na muumba wa kila kitu na nimeamini kuwa Yeye pekee ndiye muumba mwenye kuruzuku.

Kisha muumin akamkumbusha yule kafiri neema ya Mwenyezi Mungu kwake na wajibu wa kumshukuru na kumsifu kwa kumwambia:

Na lau ulipoingia kitaluni kwako ungelisema alitakalo Mwenyezi Mungu huwa (mashaallah!), hapana nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu.

Yaani lau ungelikuwa una busara ungelitambua kuwa kheri na fadhila ni kuongezeka ujuzi wako sio mali yako, ungeshindana na watu kwa maadili yako sio kwa jaha yako na kujua kuwa hapana hila wala nguvu isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu mmoja mwenye nguvu na kushinda.

Ni Yeye pekee ndiye anayetoa enzi na jahaa na kubadilisha utajiri kwa ufukara na ufukara kwa utajiri; alitakalo huwa na asilolitaka haliwi.

Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe, basi huenda Mwenyezi Mungu akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako na kukipelekea maafa kutoka mbinguni na kugeuka ardhi tupu inayoteleza; au maji yake yadidimie usiweze kuyagundua.

Mumin aliendelea kumjia juu kafiri kwa mali yake, akamwambia kuwa utajiri na ufukara unatoka kwa Mungu na wewe hujui mimi nina utajiri zaidi wa kukushinda wewe alioniwekea akiba Mwenyezi Mungu kwenye nyumba ya milele kushinda hivi vitalu vyako unavyojifaharisha navyo.

Hujui wewe kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kunifanya tajiri mimi na kukufanya fukara wewe baina ya asubuhi na jioni.

Wewe unajigamba na mali yako, kwa sababu watu wanakusifia. Je sifa hizi ndio zitakukinga na mambo yanayofichwa na nyakati? Je, umejiaminisha na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu? Huogopi wewe na hivyo vitalu vyako kushukiwa na majanga kutoka mbinguni na ukabaki mtupu?

Yakaangamizwa matunda, akabaki anapinduapindua viganja vyake kwa vile alivyoyagharimia nayo imeanguka juu ya chanja zake.

Kupinduapindua viganja ni fumbo la kujuta. Mimea iliangamia, miti ikaanguka kila upande na maji yakauka mpaka tone la mwisho. Ardhi ikawa inateleza; kama kwamba hakukuwa na chochote.

Ufukara ukachukua nafasi ya utajiri, dhiki mahali pa faraja na udhalili na kuvunjikiwa mahali pa kujitukuza na kiburi. Haya ndio matunda ya ukafiri, dhulma na ufisadi – hasara na majuto ya juhudi na mali.

Akawa anasema: Laiti nisingelimshirikisha Mola wangu na yoyote.
Kama kwamba anakusudia, kwa kauli hii, kurudi kitalu chake, lakini wapi?

﴿لَا يَنفَعُ نَفْسًا إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي إِيمَانِهَا خَيْرًا ﴿١٥٨﴾

"Basi nafsi haitaifaa imani yake ambayo haikuiamini zamani, au hakuchuma kheri kwa imani yake" Juz; 8 (6:158).

Wala hakuwa na kundi la kumsadia kinyume na Mwenyezi Mungu wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.
Kabisa! Hakuna ndugu wala rafiki au jaha wala mali, isipokuwa Mwenyezi Mungu.

﴿قُلْ إِنِّي لَن يُجِيرَنِي مِنَ اللَّـهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِن دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٢٢﴾

"Sema: Hakika hakuna yeyote awezaye kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa kwake tu." (72:22).

Huko usaidizi ni wa Mwenyezi Mungu, Mkweli. Yeye ni Mbora kwa malipo na mbora wa matokeo.
Huko ni ishara ya siku ya kiyama; yaani, ikiwa mtu katika maisha haya anapata wa kumtetea na kumsaidia, basi siku ya kiyama hatapata isipokuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) peke yake.
Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye takua na amewaandalia ujira mwema na mahali pazuri.

15

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَاضْرِبْ لَهُم مَّثَلَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيَاحُ ۗ وَكَانَ اللَّـهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

45. Na wapigie mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyoyateremsha kutoka mbinguni yakachanganyika na mimea ya ardhi ikawa majani makavu yaliyokatikakatika yanayopepeprushwa na upepo, Na Mwenyezi Mungu ana uwezo juu ya kila kitu.

الْمَالُ وَالْبَنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَالْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ عِندَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَخَيْرٌ أَمَلًا ﴿٤٦﴾

46. Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia. Na vibakiavyo vizuri ndivyo bora mbele ya Mola wako na kwa malipo na tumaini bora.

## PAMBO LA MAISHA YA DUNIA

**Aya 45 – 46**

### MAANA

Na wapigie mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyoyateremsha kutoka mbinguni yakachanganyika na mimea ya ardhi ikawa majani makavu yaliyokatikakatika yanayopepeprushwa na upepo.

Dunia ni nzuri yenye mandhari ya kijani ya kupendeza, lakini ina ghururi na madhara. Haina kheri katika akiba yake isipokuwa takua; kama alivyosema Imam Ali (a.s).

Haya ndiyo maana ya Aya; ambapo Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameifananisha dunia, katika uzuri wake, na mvua iliyonyesha kwenye ardhi ikairutubisha na ikaota miti ya kila aina, lakini mara inageuka na kuwa kame, majani yakawa makavu yanayopukusika yakirushwa na upepo. Hivi ndivyo yalivyo maisha ya dunia, ni mazuri lakini yameficha ubaya.

Na Mwenyezi Mungu ana uwezo juu ya kila kitu.

Anaweza kuuondoa ulimwengu na kuumaliza kabisa; kama alivyoweza kuumba na kuuleta. Anasema Ibnul Arabi katika kitabu Futahitl-Makkiyya "Mwenyezi Mungu ni muweza wa mambo na ana uwezo wa kuumba" Anakusudia kuwa Mwenyezi Mungu anasifika kuwa ni muweza pale anapotaka kitu kuwa kikawa, ni sawa aseme au asieme na anasifika kuwa ana uweza pale anaposema na kitu kikawa vilevile.

### MALI NA WATOTO NI PAMBO LA MAISHA YA DUNIA

Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia.

Pambo la maisha liko aina mbili: La umma na la kibinafsi. La umma ni kama vile kujenga njia za mawasiliano; mfano barabara n.k. Au taasisi; mfano kujenga vyuo vikuu, vituo vya malezi ya watoto viwanda n.k.

Na la kibinafsi ni kama nyumba, gari, mtoto mtiifu aliyefaulu, viwanda, umaarufu katika jamii n.k. Vipambo hivi sio haramu. Vitakuwaje haramu na hali Yeye ndiye aliyesema:

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِينَةَ اللَّـهِ الَّتِي أَخْرَجَ لِعِبَادِهِ وَالطَّيِّبَاتِ مِنَ الرِّزْقِ ﴿٣٢﴾

"Sema: Ni nani aliyeharamisha pambo la Mwenyezi Mungu ambalo amewatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki?" Juz. 8 (7:32).

Lakini pambo binafsi halistahili mtu kujitukuza na kujifaharisha nalo. Kwa sababu kipimo cha kutukuzwa pambo ni kwa manufaa ya umma na kubakia vizazi na vizazi. Hili ndilo alilolikusudia Mwenyezi Mungu pale aliposema:

Na vibakiavyo vizuri ndivyo bora mbele ya Mola wako na kwa malipo na tumaini bora.

Kwa sababu mwenye kutekeleza atapata huko Akhera yale aliyoyatumai, mbali ya kupata heshima na kuendelea kutajika katika maisha haya ya dunia.

Kwa ufupi ni kuwa mali ni nyenzo sio lengo. Inapimwa na kukadiriwa kwa natija yake na athari yake. Ikiwa ni kheri itakuwa kheri na ikiwa ni shari basi itakuwa shari. Ikitumika kwa njia ya shari na ufisadi, kama vile mashindano ya silaha, basi itakuwa mali ni shari na ikitumika katika kutekeleza mahitaji, basi mali itkuwa ni kheri.

Na kheri hiyo iko aina mbili: Ikiwa itamletea manufaa mwenye nayo au kumkinga na madhara basi itakuwa ya binafsi na itaisha kwa kuisha. Lakini ikiwa manufaa yake ni kwa umma basi itakuwa ni katika vibakiavyo vizuri.

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾

47. Na siku tutakayoipitisha milima na utaiona ardhi iwazi. tutawafufua wala hatuta- muacha yeyote katika wao.

وَعُرِضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًّا لَّقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّن نَّجْعَلَ لَكُم
مَّوْعِدًا ﴿٤٨﴾

48. Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako kwa safu. Hakika mmetufikia kama tulivyowaumba mara ya kwanza; bali mlidai kuwa hatutawawekea miadi.

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَـٰذَا الْكِتَابِ لَا
يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

49. Na kitabu kitawekwa ndipo utawaona waovu wakiogopa kwa sababu ya yale yaliyomo. Na watasema: "Ole wetu! Kina nini kitabu hiki hakiachi dogo wala kubwa ila kinalihesabu? Na watakuta waliyoyafanya yamehudhurishwa, Na Mola wako hadhulumu yoyote.

## TUTAWAFUFUA WALA HATUTAMUACHA YEYOTE

**Aya 47 -49**

### MAANA

Na siku tutakayoipitisha milima na utaiona ardhi i wazi.

Ardhi hii tunayoishi leo, Mwenyezi Mungu ameitaja katika Aya nyingi, miongoni mwazo ni hii tuliyo nayo. Hapa Mwenyezi Mungu ameisifu kwa sifa mbili:

Kwanza, kuwa Mwenyezi Mungu ataing'oa milima mahali ilipo na aipeleke kama mawingu, Sifa ya pili, kwamba ardhi yote kuanzia pembe hadi pembe itakuwa wazi bila ya kuweko kizuizi chochote. Hapo ndio itakuwa ufufuo ambao Mungu ameuashiria kwa kusema:

Na tutawafufua wala hatutamuacha yeyote katika wao.

Mwenyezi Mungu atawafufua wote, kuanzia wa kwanza hadi wa mwisho, kwa ajili ya hisabu.

Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako kwa safu.

Huko nyuma tumetaja kuwa hisabu na malipo ni kweli isiyokuwa na shaka. Tumelithibitisha hilo kwa dalili mkataa, katika kufasiri Aya zinazoonyesha hivyo; miogoni mwazo ni, Juz; 11 (10:4) kifungu cha 'Hisabu na malipo ni lazima'.

Aya tuliyo nayo inasema kuwa viumbe watahudhurishwa kwa Mungu kesho wakiwa wamepiga safu. Makusudio ya kuhudhurishwa hapa ni kusimama kwa Mungu kwa ajili ya hisabu.

Ama kuhusu neno safu, wafasiri wametofautiana; wengine wameliacha neno na dhahiri yake, wengine wakaleta sarufi na kulichukulia tamko yale yasiyowezekana. Tuonavyo sisi ni kuwa safu ni fumbo la utaratibu na nidhamu, kwamba viumbe watahudhurishwa kwa mola wao kwa mpangilio madhubuti.

Hakika mmetufikia kama tulivyowaumba mara ya kwanza; bali mlidai kuwa hatutawawekea miadi.

Hivi ndivyo atakavyoanza Mwenyezi Mungu kuwahukumu wale waliokuwa wakipinga ufufuo: Tuliwatoa matumboni mwa mama zetu mkiwa uchi hamna chochote; vilevile leo tumewatoa makaburini mwenu. Hakuna tofauti isipokuwa pale mwanzo mlikuwa hamuulizwi chochote na leo mmetolewa ili muulizwe yale mliyokuwa mkiyafanya, kuyaamini na kuyasema. Miongoni mwayo ni kusema kwenu kuwa ufufuo ni uzushi na vigano. Je, mmeona leo?

Na kitabu kitawekwa ndipo utawaona waovu wakiogopa kwa sababu ya yale yaliyomo.

Hii ndiyo Siku ya Ufufuo mliyokuwa mkiikadhibisha, Kila mmoja atapewa daftari la matendo yake na aambiwe:

اقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٤﴾

"Soma kitabu chako! Nafsi yako leo inakutosha kukuhisabu" (17:14)

Yaani soma daftari la matendo yako na ujipigie mahisabu wewe mwenyewe. Atasoma huku akitetemeka kwa hofu isiyokuwa na matumini yoyote wala matarajio ya kuokoka. Lau angeliogopa adhabu tangu mwanzo na kajiepusha na njia yake, angelikuwa leo yuko kwenye amani na sala- ma. Lakini alijiaminisha huko na anahofu hapa.

Na watasema: ole wetu! Kina nini kitabu hiki hakiachi dogo wala kubwa ila kinalihesabu?

Hapo mwanzo walikuwa wakisema hakuna kitabu wala hisabu.

Na watakuta waliyoyafanya yamehudhurishwa, bila ya kuzidi wala kupungua; Kwanini isiwe hivyo na Mola wako hadhulumu yoyote? Si kwenye thawabu wala adhabu; bali huwa zikaongezwa thawabu kwa mwenye kufanya wema na kusamehewa mwenye kufanya uovu.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

50. Na tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipokuwa Iblis. Alikuwa miongni mwa majini akatoka kwenye amri ya

Mola wake. Je, mnamfanya yeye na dhuria zake kuwa mawalii badala yangu, hali wao ni adui zenu? Ni uovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.

مَّا أَشْهَدتُّهُمْ خَلْقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَا خَلْقَ أَنفُسِهِمْ وَمَا كُنتُ مُتَّخِذَ الْمُضِلِّينَ عَضُدًا ﴿٥١﴾

51. Si kuwashuhudisha kuumbwa kwa mbingu na ardhi wala kuumbwa kwa nafsi zao. Wala sikuwafanya wapotezao kuwa ni mkono.

وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُوا شُرَكَائِيَ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُم مَّوْبِقًا ﴿٥٢﴾

52. Na siku atakaposema waiteni hao mliodai kuwa ni washirika wangu, Basi watawaita nao hawatawaitikia. Nasi tutaweka baina yao maangamizi.

وَرَأَى الْمُجْرِمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُم مُّوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿٥٣﴾

53. Na wahalifu wataona moto na watadhani kuwa wao watauingia wala hawatapata pa kuepukia.

## WALISUJUDI ISIPOKUWA IBLISI

**Aya 50 – 53**

### MAANA

Na tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipokuwa Iblis;

Umetangulia mfano wake katika Juz. 1(2:11), Juz. 8 (7:11) na Juzuu hii ya 15 (17: 61).

Alikuwa miongoni mwa majini akatoka kwenye amri ya Mola wake.

Yaani alitoka kwenye twaa ya mola wake. Mara nyingi tumesema kuwa sisi tunaamini kuweko majini, kwa sababu wahyi unathibitisha hilo na akili haipingi hilo; na kwamba ufafanuzi wake tunamwachia Mjuzi wa ghaibu.

Je, mnamfanya yeye na dhuria zake kuwa mawalii badala yangu?

Qur'an huwa inajifasiri yenyewe na sehemu moja inaitolea ushahidi sehemu nyingine. Katika Aya nyingi imeleta ibara ya kuwa wale wanaoichanganya haki na batili kuwa ni askari wa Iblisi na mawalii wake.

Kwa hiyo hapa inafaa kufasiri kuwa dhuria za Iblisi ni askari wake na wazaidizi wake na kwamba kizazi cha Ibilisi, askari wake na mawalii wake, ni wale wanaoichanganya batili na uongo na kuzulia haki. Sio mbali kwamba ibara ya kuwa hao ni dhuria za Ibilisi, ni kufanana vitendo vyao na vyake.

La kushangaza ni kauli ya asemaye kuwa Ibilisi ana tupu ya kiume katika paja lake la kuume na tupu ya kike katika paja lake la kushoto. Kwa hiyo aniingiza ya kiume kwenye hiyo ya kike na anapata kizazi na dhuria

Hali wao ni adui zenu?

Kila anayekupambapamba na kukudanganya na mambo ya batili au kukusifia mambo usiyokuwa nayo, basi huyo ni adui yako, ujue hilo au usijue.

Ama yule anayezua vigano juu ya Ibilisi na wengineo, basi huyo ni adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na pia wa ubinadamu.

Ni uovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.

Madhalimu ni wale wanaobadilsha twaa ya Mwenyezi Mungu kuwa twaa ya shetani; miongoni mwao ni wale wanaowachagua wafisadi kwenye vyeo na kuwafidhilisha kuliko watu wema.

Si kuwashuhudisha kuumbwa kwa mbingu na ardhi wala kuumbwa kwa nafsi zao. Wala sikuwafanya wapotezao kuwa ni mkono.

Ambao hawakushuhudishwa ni ibilisi na dhuria zake. Makusudio ya mkono hapa ni usaidizi. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) akilitaka jambo ni kuliambia kuwa kisha likawa, hamshauri wala hamtaki msaada yeyote, kwa sababu yeye hawahitajii walimwengu.

Na wakati alipoumba vitu hakumuhudhurisha yeyote katika wao, hata kama ni mwenye takua zaidi ya wote; sikwambii tena akiwa ni mpotezaji; kama vile Ibiisi na askari wake. Madamu mambo yako hivyo, imekuwaje kuasiwa muumbaji na kutiiwa yule ambaye hawezi kujisaidia hata yeye mwenyewe au kujikinga na madhara?

Na siku atakaposema waiteni hao mliodai kuwa ni washirika wangu, Basi watawaita nao hawatawaitikia. Nasi tutaweka baina yao maangamizi.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu kesho atawaambia wale waliokuwa wakimfanyia washirika katika twaa yake: wako wapi wale ambao mliwatii na mkadai kuwa wao watawapa manufaa siku hii ya lo ngumu? Hebu waiteni tuone kama watawaitikia. Hapana! Wenyewe wana shughuli inayowashughulisha; wako katika adhabu ya moto, Kauli yake Mwenyezi Mungu kuwa watawaita na wasiwasikie ni fumbo la kukata kwao tamaa kwa matarajio waliyokuwa wakiyatarajia.

Na wahalifu wataona moto na watadhani kuwa wao watauingia wala hawatapata pa kuepukia.

Makusudio ya kudhani hapa ni kujua na kuwa na yakini. Pia kuepukia ni kuepuka na moto. Kukimbia kesho ni sawa na kujaribu kuyakimbia mauti leo hapa duniani.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَـٰذَا الْقُرْآنِ لِلنَّاسِ مِن كُلِّ مَثَلٍ ۚ وَكَانَ الْإِنسَانُ أَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ﴿٥٤﴾

54. Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'an kila aina ya mifano. Lakini mtu amezidi kila kitu kwa ubishi.

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَن يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ وَيَسْتَغْفِرُوا رَبَّهُمْ إِلَّا أَن تَأْتِيَهُمْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ﴿٥٥﴾

55. Na hapana kilichowazuia watu kuamini ulipowajia uongofu na kuomba maghu- fira kwa Mola wao; isipokuwa yawafikie ya wale wa zamani au iwajie adhabu waziwazi.

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۚ وَيُجَادِلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ ۖ وَاتَّخَذُوا آيَاتِي وَمَا أُنذِرُوا هُزُوًا ﴿٥٦﴾

56. Na hatuwatumi Mitume ila wawe wabashiri na waonyaji. Na waliokufuru wanabishana kwa batili, ili waivunje haki kwayo, na wanazifanya ishara zangu na yale waliyoonywa, kuwa ni mzaha.

## MTU NI MBISHI SANA

**Aya 54 – 56**

### MAANA

Na hakika tumewaeleza watu katika hii Qur'an kila aina ya mifano, Lakini mtu amezidi kila kitu kwa ubishi.

Makusudio ya mtu hapa sio kila mtu bali ni watu wengi zaidi, kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu kwenye Aya kadhaa: "Watu wengi hawana akili" "watu wengi hawajui" watu wengi hawaamini" n.k. Qur'an ni kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa waja wake, kinachowaongoza kwa dalili zake na mawaidha yake na kuhimiza kushikamana na hukumu zake na mafundisho yake.

Mwenyezi Mungu amefafanua mawaidha na dalilil hizi kwa mifumo mbalimbali na akazipigia mifano mbalimbali; ikiwemo ile ya watu wawili waliotajwa katika Aya ya 32 ya Sura hii na kufananisha maisha na maji katika Aya ya 54. lakini watu hawatii akilini na wanabishana katika mambo yaliyo wazi, wakijaribu kubatishilisha haki kwa mambo ya uongo na ya kupambamba.

Na hapana kilichowazuia watu kuamini ulipowajia uongofu na kuomba maghufira kwa Mola wao; isipokuwa yawafikie ya wale wa zamani au iwajie adhabu waziwazi.

Makusudio ya uongofu ni Qur'an na ubanifu wake ulio wazi. kuomba maghufira ni kutubia na yaliyowafikia wa zamani ni maangamivu; kama yaliyowafikia kaumu ya Nuh, Lut, A'd na Thamud.

Maana ni kuwa washirikina hawajaribu kuamni au kufikiria kuamni mpaka wapatikane na moja wapo ya mambo mawili: Kwanza ni kushukiwa na adhabu ya kuwafyeka; kama ilivyowashukia waliokuwa kabla yao; ndipo wataamni; ambapo imani, wakati huo, haifai kitu; kama Firauni ambaye aliamini alipoona maangamizi na kufa maji kunafika. Jambo la pili ni kuiona adhabu ana kwa ana.

Kwa maneno mengine ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) alipobainisha, katika aya zilizotangulia, kuwa Yeye ameleta dalii zilizo waziwazi na watu wengi wakakataa isipokuwa ubishi, sasa anasema kuwa dalili hizi hazifai kitu kwa watu wasioamini isipokuwa wakati wa kukata roho au wanapotishika na adhabu wanapoiona kwa macho yao au wanapoamini kuwa itawafikia tu.

Na hatuwatumi Mitume ila wawe wabashiri na waonyaji.

Huu ndio umuhimu wa Mtume kumpa habari njema ya neema yule mwenye kutii na kumuonya na adhabu yule mwenye kuasi, Maana haya yamekaririka mara nyingi. Tazama Juz. 6 (4:165).

Na waliokufuru wanabishana kwa batili, ili waivunje haki kwayo na wanazifanya ishara zangu na yale waliyoonywa, kuwa ni mzaha.

Ameziweka wazi ishara na akazithibitisha kwa ubainifu na dalili, lakini waliokufuru wakabishana na wakajaribu kuzibatilisha kwa uongo na mizaha. Makusudio ya kuzifanyia mizaha ishara za Mwenyezi Mungu hapa sio mizaha ya kusema tu; bali ni kuwa kila mweye kuijua hukumu, miogoni mwa hukumu za Mwenyezi Mungu, na asiitumie, basi yeye ni katika walioifanya Qur'an na dini ya Mwenyezi Mungu kuwa ni mchezo.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Mwenye kuisoma Qur'an, kisha akafa akaingia motoni – kwa kutoitumia Qur'an – basi huyo ni katika waliozifanyia mzaha ishara za Mwenyezi Mungu.**

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ فَأَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ ۚ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۖ وَإِن تَدْعُهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ فَلَن يَهْتَدُوا إِذًا أَبَدًا ﴿٥٧﴾

57. Na ni nani dhalimu zaidi kuliko yule anayekumbushwa ishara za Mola wake na akazipuuza na akasahau yaliyotangulizwa na mikono yake? Hakika tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu, na tumeweka kwenye masikio yao uziwi, Na ukiwaita kwenye uongofu hawataongoka kabisa.

وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو الرَّحْمَةِ ۖ لَوْ يُؤَاخِذُهُم بِمَا كَسَبُوا لَعَجَّلَ لَهُمُ الْعَذَابَ ۚ بَل لَّهُم مَّوْعِدٌ لَّن يَجِدُوا مِن دُونِهِ مَوْئِلًا ﴿٥٨﴾

58. Na Mola wako ni mwenye maghufira na mwenye rehema, lau angeliwachukulia kwa walioyachuma, bila shaka angeliwafanyia haraka kuwaadhibu, Lakini wana miadi ambayo hawatapata kimbilio la kuepukana nayo.

وَتِلْكَ الْقُرَىٰ أَهْلَكْنَاهُمْ لَمَّا ظَلَمُوا وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِم مَّوْعِدًا ﴿٥٩﴾

59. Na miji hiyo tuliwaangamiza walipodhulumu na tukawawekea miadi ya maangamizo yao.

## ALIYEKUMBUSHWA ISHARA ZA MOLA WAKE AKAZIKATAA

**Aya 57 – 59**

### MAANA

Na ni nani dhalimu zaidi kuliko yule anayekumbushwa ishara za Mola wake na akazipuuza na akasahau yaliyotangulizwa na mikono yake?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameziweka wazi dalili za kuweko kwake na wajibu wa kumtii Yeye kwa mifumo mbali mbali; kisha akapiga mifano mingi ya hayo. Akamwamrisha mtu kufanya kheri na kutubia dhambi zake zilizopita, akamkataza shari na akamuhadharisha kukhalifu amri na makatazo na kuendelea na dhambi. Lakini mtu ameyapuuza yote hayo na akaitia nafsi yake kwenye maangamivu.

Hakika tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu na tumeweka kwenye masikio yao uziwi.

Umetangula mfano wake pamoja na tafsiri katika Juz. 7 (6:25) na Juz. hii ya 15 (17: 46).

Na ukiwaita kwenye uongofu hawataongoka kabisa.

Wataongoka vipi na hali kwenye nyoyo zao kuna vifuniko na kwenye masikio yao kuna uziwi. Kila asiyenufaika na mawaidha mazuri, basi huyo ni sawa na kipofu wa moyo na macho na ni kiziwi.

Na Mola wako ni mwenye maghufira na mwenye rehema, lau angeliwachukulia kwa walioyachuma, bila shaka angeliwafanyia haraka kuwaadhibu.

Umetangula mfano wake pamoja na tafsiri katika Juz. 14 (16:61).

Lakini wana miadi ambayo hawatapata kimbilio la kuepukana nayo.

Mausudio ya miadi hapa ni wakati wa kufika mbele ya Mwenyezi Mungu, Ni miadi isiyovunjwa wala kukimbiwa.

Imam Ali (a.s) anasema kumwambia Mola wake: "Wewe ni wa milele huna muda na wewe ni mwishilio usioepukwa na wewe ni ahadi isiyokimbiwa. Uko mikononi mwako utosi wa kila mnyama na kwako ni marejeo ya kila nafsi."

Na miji hiyo tuliwaangamiza walipodhulumu na tukawawekea miadi ya maangamizo yao.

Makusudio ya miji hapa ni ya kina A'd,Thamud na wengineo katika umma zilizopita. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu alijaalia wakati maalum wa kuaangamia madhalimu, ukifika hawatachelewa hata saa moja wala hawatatangulizwa.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO

وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِفَتَاهُ لَا أَبْرَحُ حَتَّىٰ أَبْلُغَ مَجْمَعَ الْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِيَ حُقُبًا ﴿٦٠﴾

60. Na pale Musa alipomwambia kijana wake: Sitaacha kuendelea mpaka nifike makutano ya bahari mbili au nitaendelea kwa muda mrefu.

فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنِهِمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦١﴾

61. Basi wawili hao walipofika makutano ya bahari mbili, walimsahau samaki wao, naye akashika njia yake kuponyokea baharini.

فَلَمَّا جَاوَزَا قَالَ لِفَتَاهُ آتِنَا غَدَاءَنَا لَقَدْ لَقِينَا مِن سَفَرِنَا هَٰذَا نَصَبًا ﴿٦٢﴾

62. Waliopokwishapita alimwambia kijana wake: Tupe chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata machovu sana kwa hii safari yetu.

قَالَ أَرَأَيْتَ إِذْ أَوَيْنَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَسِيتُ الْحُوتَ وَمَا أَنسَانِيهُ إِلَّا الشَّيْطَانُ أَنْ أَذْكُرَهُ وَاتَّخَذَ
سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ عَجَبًا ﴿٦٣﴾

63. Akasema: Waona! Pale tulipopumzika penye jabali basi mimi nilimsahau samaki, na hapana aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila shetani tu. Naye akashika njia yake baharini kwa ajabu

قَالَ ذَٰلِكَ مَا كُنَّا نَبْغِ فَارْتَدَّا عَلَىٰ آثَارِهِمَا قَصَصًا ﴿٦٤﴾

64. Akasema: Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka. Basi wakarudi kwa kufuata nyayo zao.

## MUSA NA MAKUTANO YA BAHARI MBILI

**Aya 60 – 64**

### LUGHA

Kijana wake, anaweza kuwa mwenzake au mtumishi wae, Makutano ya bahari mbili ni mahali zinapokutana bahari mbili na kuwa moja. Inasemekana hapo palikuwa ni makutano ya bahari nyeupe na bahari nyekundu. Kama ningekuwa mtalamu wa jografia, ningelichanganya kauli zote kisha nikachagua iliyo sahihi zaidi.

### MAANA

Na pale Musa alipomwambia kijana wake: Sitacha kuendelea mpaka nifike makutano ya bahari mbili au nitaendelea kwa muda mrefu, Basi wawili hao walipofika makutano ya bahari mbili, walimsahau samaki wao, naye akashika njia yake kuponyokea baharini.

Wametofautiana kuhusu Musa, mhusika mkuu wa kisa hiki; kuwa je, ni Musa bin Imran au ni mwenginewe. Amenukuu Razi kutoka kwa Mayahudi kwamba ni Musa bin Misha bin Yusuf bin Ya'qub. Huyo ni wa mbele kuliko Musa bin Imran. Wafasiri wengi wamesema kuwa ni yule mashuhuri, Musa bin Imran, Hiyo ndiyo kauli iliyo dhahiri.

Kuhusu kijana wake, kauli iliyo maarufu ni Yoshua bin Nun, mtoto wa dada yake Musa bin Imran, mwanaafunzi wake wa karibu na khalifa wake kwa wana wa Israil. Ama yule aliyeambiwa na Musa kuwa nikufuate, kauli maarufu ni Khidhr. Lakini Mwenyezi Mungu amelinyamazia jina la kijana

na la aliyemfuata. Kwa hiyo sisi tutajumlisha kwa kusema huyu ni kijana wake na yule ni swahibu wake.

Imesemekana kuwa Khidhr sio jina lake hasa bali ni msimbo. Jina lake hasa ni Fabiliya bin Malkan, Wametofautiana kuhusu kuwa je, yeye alikuwa Mtume au walii? Pia imesemekana kuwa yeye ni katika waliope- wa umri mrefu na kwamba yuko hai hadi siku ya ufufuo.

Ama sisi tunalazimika kunyamaza kuhusu utume wake na uhai wake, kwa vile hakuna dalili ya kukata shaka kutoka katika Qur'an wala Hadithi inayohusiana na mojawapo ya hayo mawili. Wala hayo hayahusiki na itikadi yetu au maisha yetu. Wengine wamesema kuwa ni Malaika. Hiyo ni kauli ya mbali sana.

Kuna riwaya inayosema kuwa mtu mmoja alimuuliza Musa: "Ni nani mwenye elimu zaidi?" Musa akasema ni mimi.

Ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) akataka kumfundisha kuwa juu ya kila mjuzi kuna mjuzi zidi; Kwa hiyo akampa wahyi kwamba katika makutano ya bahari mbili kuna mtu anajua ambayo huyajui, Musa akasema nitakutana naye vipi? Mungu akasema, chukua samaki asiyekuwa na uhai na utakapomkosa samaki huyo, basi hapo ndio kuna huyo mjuzi.

Basi Musa akamchukua samaki na akongozana na kijana wake. Akaenda mpaka Musa akachoka, akapumzika na akapata lepe la usingizi. Wakati akiwa amelala yule samaki akapata uhai na akaingia baharini. Hii ni katika miujiza ya Mwenyezi Mungu kwa Musa.

Ikiwa riwaya hii imetegema hali halisi au imetolewa kwenye maelezo ya Aya, lakini inatoa mwanga wa Aya za kisa hiki.

Walipokwishapita alimwambia kijana wake: Tupe chakula chetu cha machana. Kwa hakika tumepata machovu sana kwa hii safari yetu.

Baada ya Musa na kijana wake kupumzika kidogo kwenye makutano ya bahari mbili, walianza upya safari yao. Mpaka wakachoka na kuhisi njaa. Musa akataka chakula kutoka kwa kijana wake. Yule kijana alishuhudia miujiza ya samaki kupata uhai na kuingia baharini, lakini akasahau kumwambia Musa. Musa alipomtaka chakula ndio akakumbuka na akasema:

Waona! Pale tulipopumzika penye jabali basi mimi nilimsahau samaki, na hapana aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila shetani tu. Naye akashika njia yake baharini kwa ajabu.

Musa aliposikia maneno hayo akaona dalili za kupata yale aliyoyataka na akasema: Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka. Basi wakarudi kwa kufuata nyayo zao. Yaani Musa na kijana wake wakarudi nyuma pale alipoingia baharini kwa kufuata ile njia yao ya kwanza.

فَوَجَدَا عَبْدًا مِّنْ عِبَادِنَا آتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِّنْ عِندِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِن لَّدُنَّا عِلْمًا ﴿٦٥﴾

65. Basi wakamkuta mja miongoni mwa waja wetu tuliyempa rehema kutoka kwetu na tukamfunza elimu kutoka kwetu.

قَالَ لَهُ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَىٰ أَن تُعَلِّمَنِ مِمَّا عُلِّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٦﴾

66. Musa akamwambia: Je, nikufuate ili unifunze katika ule uongofu uliofunzwa?

قَالَ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٦٧﴾

67. Akasema: Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami.

وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْرًا ﴿٦٨﴾

68. Na utawezaje kuvumilia yale usiyokuwa na habari nayo?

قَالَ سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ اللَّـهُ صَابِرًا وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾

69. Akasema: Inshallah utaniona ni mvumilivu wala sitoasi amri yako.

قَالَ فَإِنِ اتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَن شَيْءٍ حَتَّىٰ أُحْدِثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾

70. Akasema: Basi ukinifuata, usiniulize kitu mpaka nianze kukutajia.

## MUSA ANAKUTANA NA SWAHIBU YAKE

**Aya 65 – 70**

### MAANA

Basi wakamkuta mja miongoni mwa waja wetu tuliyempa rehema kutoka kwetu na tukamfunza elimu kutoka kwetu. Musa akamwambia: Je, nikufuate ili unifunze katika ule uongofu uliofun- zwa?

Makusudio ya 'elimu kutoka kwetu' ni baadhi ya elimu. Na makusudio ya elimu ni elimu ya ghaibu; yaani tulimpa kitu katika elimu ya ghaibu, akiishiria hilo kwa kuitoboa safina, na kumuua kijana. Masufi wanategemea Aya hii kusahihisha madhehebu yao wanaposema elimu ya kupewa; yaani kuwa na elimu bila ya kusoma.

Maana ni kuwa Musa na kijana wake waliporudi mpaka mahali walipopumzika mwanzo, walimkuta mtu mingoni mwa waja wema wa Mwenyezi Mungu, aliyepewa rehema na Mwenyezi Mungu na akamneemesha elimu ya kutosha yenye kunufaisha, Musa akamwamkia, naye akamrudishia salam. Musa akamuambia wewe ndiye niliyekuwa nakutaka je, utaniruhusu niandamane nawe na unifundishe uongofu uliofunzwa ninufaike nao?

Wanodai kuwa mtu huyo alikuwa Mtume, wanatoa dalii kwa kauli hii ya Mwenyezi Mungu: 'tuliyempa rehema kutoka kwetu' kwa sababu rehema ni utume.

Lakini wamesahau kuwa rehema inaenea kwenye mambo mengine zaidi ya utume; na kupatikana inayoenea zaidi haifahamishi kupatikana mahsusi. Ukisema nimekula tunda, haifahamishi kuwa lazima uwe umekula zabibu, inawezekana ni aina nyingine ya tunda.

Akasema: Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami. Na utawezaje kuvumilia yale usiyokuwa na habari nayo?

Yule mtu mwema alimwambia Musa kuwa lau utafuatana nami utaonamaajabu yatakayokufanya ushindwe kunyamaza, kwa sababu, kwa dhahiri yake yataonekana kuwa ni mambo mabaya na undani wake utakuwa huujui, nawe utakuwa huwezi kuyanyamazia mambo yanayonekana kuwa ni mabaya.

Akasema Musa inshallah utaniona ni mvumilivu wala sitoasi amri yako.

Musa alijitoa kwa kusema inshaalah, kuhofia asije akashindwa kujizuia; kama ilivyotokea.

Akasema: Basi ukinifuata, usiniulize kitu mpaka nianze kukutajia.

Yule mtu mwema alimpa sharti Musa kuwa asimuulize kitu kwa yale atakayoyafanya, kwa hali yoyote itakayokuwa. Musa alikubali lile sharti, kwa sababu aliondoka naye; kama unavyoonyesha ufafanuzi ufuatao:

فَانطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا رَكِبَا فِي السَّفِينَةِ خَرَقَهَا قَالَ أَخَرَقْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا لَقَدْ جِئْتَ شَيْـًٔا إِمْرًا
﴿٧١﴾

71. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka walipopanda jahazi akailtoboa, Akasema: Unalitoboa ili uwazamishe watu wake? Hakika umefanya jambo baya.

قَالَ أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٢﴾

72. Akasema: Sikukuambia kuwa wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?

قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ وَلَا تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْرًا ﴿٧٣﴾

73. Akasema: Usinichukulie kwa niliyosahau, wala usinipe uzito kwa jambo langu.

فَانطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا لَقِيَا غُلَامًا فَقَتَلَهُ قَالَ أَقَتَلْتَ نَفْسًا زَكِيَّةً بِغَيْرِ نَفْسٍ لَّقَدْ جِئْتَ شَيْـًٔا نُّكْرًا
﴿٧٤﴾

74. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka wakamkuta kijana; akamuua. Akasema: Umemuua mtu asiye na kosa na hakuua! Hakikia umefanya jambo baya kabisa!

## WAKAONDOKA

**Aya 71 – 74**

### KUJIZUIA NA YANAYOTATIZA

Aya hizi zinafahamisha kuwa kuna mambo amabayo dhahiri ni rehema na undani wake ni adhabu na mengine ni kinyume. Na kwamba hukumu kwenye mambo ya namna hiyo ni kungoja kuyaamulia mpaka upatikane uhakika.

Imepokewa Hadithi mutawwatir, Kutoka kwa Mtume mtukufu **(s.a.w.w)** kuwa yeye amasema: "Halali iko wazi na haramu iko wazi na baina ya halali na haramu kuna mambo yenye kutatiza."

Watu wengi hawajui ni halali au ni haramu. Mwenye kuyaaacha kwa kuilinda dini yake na heshima yake, atakuwa amesalimika, Na mwenye kuijingiza kwenye kitu chochote katika hivyo, basi atakuwa anakurubia kuingia katika haramu" Hadithi nyingine inasema: "Kujizuia na yenye kutatiza ni bora kuliko kujiingiza kwenye maangamizi."

Kuna mapokezi yanayosema kwamba Luqman, mwenye hekima, aliingia kwa Daud akamkuta anatengeneza deraya, naye alikuwa hajapata kuiona. Akataka kumuuliza, lakini akaona bora angoje, Daud alipomaliza kuitengeza, aliivaa huku akisema: nguo nzuri sana hii ya vita. Akafahamu Luqman kuwa ile nguo ni ya vita. Akasema: "Kunyamaza ni hekima."

Ni wachache sana wanoweza kuvumilia hivyo. Yule mtu mwema ameleta mambo matatu ya ushahidi wa hakika hii, kama ifuatavyo:

1. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka walipopanda jahazi akalitoboa.

Musa alikwenda na yule mwenzake kwenye ufuo wa bahari, Walipokuta jahazi, wakamwomba mwenyewe awachukue, akakubali.

Walipofika katikati ya bahari, yule mja mwema alilitoboa, kiasi ambacho wangeweza kuzama na kufa maji. Musa akashtuka na jambo hili baya na akasema: Unalitoboa ili uwazamishe watu wake? Hakika umefanya jambo

baya kabisa, Musa akachukua nguo yake akaziba ile tundu; kama wanavyodai wafasiri.

Akasema: Sikukuambia kuwa wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?

Hapo anamkumbusha lile sharti la kutomuuliza kitu, Musa akaomba msamaha na akasema: Usinichukulie kwa niliyosahau. Kwa sababu kusahau hakuna neno wala usinipe uzito kwa jambo langu. Yaani usinid- hikishe kwa kusuhubiana na wewe.

2. Basi wawili hao wakaondoka, mpaka wakamkuta kijana; akamuua.

Moyo wa Musa ukafazaika kutokana na mauaji, akasema: Umemuua mtu asiye na kosa na hakuua! Hakikia umefanya jambo baya. Huyu maskini amefanya nini? Unamuua bure tu. Huu ni ubaya wa wazi.

### SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)
Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

### MWISHO WA WA JUZUU YA KUMI NA TANO

## YALIYOMO


**1 TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA 1
1 ................. IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA
1 ........ IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED
1 IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU
1 ................................. UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI
2 ............................................... MAKOSA YA CHAPA
**3 TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
3 ............................................................... ISRAI
3 ............................................................... MAANA
3 ..........................................MAANA YA NEON ISRAI
4 .................................... ISRAI KWA ROHO NA MWILI
5 .....................MASJIDUL-HARAM NA MASJIDUL-AQSWA
7 ..............................................SOMO KATIKA ISRAI
8 ..................................... NA TUKAMPA MUSA KITABU
8 ............................................................... MAANA
**9 TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
9 ............................. WAISRAILI NA UFISADI MARA MBILI
9 ............................................................... LUGHA
9 ............................................................... MAANA
13 ......KUELEZEA MWENYEZI MUNGU NA DOLA YA ISRAIL
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**16** ...............................................................
16 ............ QUR'ANI INAONGOZA KWENYE YALIYONYOOKA
16 ............................................................... MAANA
17 .................................. 1. Uislamu Ni Dini Ya Maumbile
17 ................................2. Imani Ya Uislamu Kwenye Elimu
17 ...............................................3. Kuiachia Huru Akili
17 ............................................... 4. Uhuru Wa Kufikiri
18 ......................................................5. Wigo Mpana
18 ............................................................... 6. Jihadi
18 .....................................7. Mali Ni Ya Mwenyezi Mungu
18 ................................................ 8. Uislamu Na Maisha
20 .................................................. NDEGE SHINGONI
21 ............................................................... LUGHA

21 ............................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**22** ..................................................................
22 .................TUNAWAAMRISHA WAPENDA ANASA WAKE
22 ............................................................ LUGHA
22 ............................................................ MAANA
26 ................................................. USIWAMBIE AH!
26 ............................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**28** ..................................................................
29 ............................................................ WASIA 10
29 ............................................................ MAANA
30 .................................... WAKO WAPI WAADILIFU?
31 .......................UISLAMU NA NADHARIA YA MAADILI
33 ...................................... KUSEMA BILA YA UJUZI
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**36** ..................................................................
36 .......... JE, MOLA WENU AMEWACHAGULIA WAVULANA?
36 ............................................................ MAANA
37 ................KILA KITU KINAMTAKASA (KINAMSABBIH)
39 ..............................................UNAPOSOMA QUR'AN
39 ............................................................ MAANA
40 ..TUTAKAPOKUWA MIFUPA NA MAPANDE YALIYOSAGIKA
40 ............................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**42** ..................................................................
42 .......WAAMBIE WAJA WANGU WASEME MANENO MAZURI
42 ............................................................ MAANA
45 ........................................................MJI WOWOTE
45 ............................................................ MAANA
45 ............................................. Mahdiy Anayengojewa
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**48** ..................................................................
48 ......................................................WAKASUJUDU
48 ............................................................ MAANA
48 ........KUMTANGULIZA ALIYEZIDI JUU YA ALIYEZIDIWA
50 ................................. ANAWAENDESHEA MAJAHAZI

51 ............................................................ MAANA
52 ................................WANAADAMU TUMEWATUKUZA
52 ............................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**55** ..............................................................................
55 .......................JE MTUME ANAHADAIKA NA DINI YAKE
55 ............................................................ MAANA
56 ..................... SIMAMISHA SWALA LINAPOPINDUKA JUA
57 ............................................................ MAANA
59 ......................NGUVU YA HAKI NA NGUVU YA BATILI
60 ................................................. QUR’ANI NI PONYO
60 ............................................................ MAANA
61 .......... ROHO INATOKANA NA AMRI YA MOLA WANGU
62 .......... MWENYEZI MUNGU NA ELIMU YA CHEMBE HAI
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**64** ..............................................................................
64 ................................TUNGELIPENDA TUNGELIONDOA
64 ............................................................ MAANA
65 ....................................................KUFIKIRIA MALI
65 ....................................................KUJIPENDA
68 ......................................ALIYEONGOZWA NA MUNGU
68 ............................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**71** ..............................................................................
71 ..................................... TULIMPA MUSA ISHARA TISA
71 ............................................................ MAANA
74 .....................................KWA HAKI TUMEITEREMSHA
74 ............................................................ MAANA
75 ....................JE, QUR’ANI ILISHUKA KIDOGO KIDOGO?
76 .......................................................WANYOOFU
78 ....................... MWISHO WA SURA YA KUMI NA SABA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**79** ..............................................................................
79 .........................AMEMTEREMSHIA KITABU MJA WAKE
79 ............................................................ MAANA
81 ..................................................WATU WA PANGO
81 ....................................................... UTANGULIZI

82 ........................................................... MAANA
84 ...........................................HABARI ZAO ZA KWELI
84 ........................................................... MAANA
84 .......................................... SEHEMU YA KWANZA
85 ................................................. SEHEMU YA PILI
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**87** ..........................................................................
87 .................................NA KAMA HIVYO TULIWAINUA
87 ............................................... SEHEMU YA TATU
88 ..................................................SEHEMU YA NNE
91 .........................................................INSHAALLAH
91 ........................................................... MAANA
91 ...................................................UTASHI MKUU
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**94** ..........................................................................
94 .......................................SOMA ULIYOPEWA WAHYI
94 ........................................................... MAANA
96 ......................UJIRA WA WATENDAO MEMA HAUPOTEI
96 ........................................................... MAANA
98 ................BAINA YA KAFIRI TAJIRI NA MUMIN FUKARA
98 .......................................... MUHTASARI WA KISA
99 ........................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**
**103**.........................................................................
103 ................................PAMBO LA MAISHA YA DUNIA
103 ......................................................... MAANA
103 ... MALI NA WATOTO NI PAMBO LA MAISHA YA DUNIA
104 .........TUTAWAFUFUA WALA HATUTAMUACHA YEYOTE
104 ......................................................... MAANA
106 ...............................WALISUJUDI ISIPOKUWA IBLISI
106 ......................................................... MAANA
107 ............................................MTU NI MBISHI SANA
108 ......................................................... MAANA
ALIYEKUMBUSHWA ISHARA ZA MOLA WAKE AKAZIKATAA 109
109 ......................................................... MAANA

**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA KUMI NA TANO**

**111**........................................................................
111 ......................MUSA NA MAKUTANO YA BAHARI MBILI
111 ........................................................... LUGHA
111 .......................................................... MAANA
113 .......................MUSA ANAKUTANA NA SWAHIBU YAKE
113 .......................................................... MAANA
114 ................................................... WAKAONDOKA
114 ................................KUJIZUIA NA YANAYOTATIZA
115 ..........................................SHARTI YA KUCHAPA
115 ...............MWISHO WA WA JUZUU YA KUMI NA TANO
116 ......................................................YALIYOMO